*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

## Kikao cha Kumi na Sita– Tarehe 24 Aprili, 2018

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndungai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Moja leo ni Kikao cha Kumi na Sita, Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Tunaanza na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, swali la kwanza linaulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Babati Mjini, Mheshimiwa Pauline Gekul.

Na. 125

### Hitaji la Maji Safi na Salama Kata ya Sigino - Babati

**MHE. PAULINE P. GEKUL** aliuliza:-

Kata ya Sigino na Vijiji vyake vyote katika Jimbo la Babati Mjini haina kabisa maji safi na salama:-

Je, ni nini mkakati wa Serikali wa kuipatia maji safi na salama Kata hiyo pamoja na Vijiji vyake?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pauline Philip Gekul, Mbunge wa Babati Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba vijiji vyote vinne katika Kata ya Sigino ndani ya Halmashauri ya Mji wa Babati vyenye wakazi 11,895 havina huduma ya maji safi na salama. Hata hivyo ziko hatua mahsusi zinazoendele. Mnamo tarehe 29 Mei, 2017, Halmashauri ya Mji wa Babati ilisaini mkataba wa Sh.487,470,000 kujenga mradi wa maji katika Kijiji cha Imbilili ambao ulipangwa kukamilika tarehe 30 Juni, 2018 lakini Mkandarasi *Black Lion Limited* amebainika kuwa na uwezo mdogo kwani hadi sasa ametekeleza kazi kwa asilimia saba tu. Naishauri Halmashauri ambapo Mheshimiwa Pauline Gekul ni Diwani, itathmini haraka hali hiyo na ichukue hatua haraka kwa manufaa ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine kubwa inayoendela ni utekelezaji wa mkataba kati ya Halmashauri na Mkandarasi Maswi *Drilling Company Limited* kuchimba visima virefu katika Vijiji vya Sigino, Singu na Haraa kwa shilingi milioni 94.5 ambao umefikia asilimia 25 na utakamilika tarehe 30 Juni, 2018. Usanifu na ulazaji wa mabomba yakayosambaza huduma za maji safi na salama kwa wananchi utaanza mwaka 2018/2019 kwa kutumia Sh.611,137,000 ambazo zimetengwa kutekeleza mradi huo. Ahsante.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Pauline Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni kweli majibu hayo aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri ni ya kweli kabisa kwa hatua ambazo zinaendelea katika Halmashauri, lakini huyu Mkandarasi Maswi kimsingi amekuwa akitusumbua sasa

muda mrefu kweli amekuwa akitoa sababu mbalimbali kwamba sijui ni masika hawezi kutafuta haya maji. Sasa naomba kwa sababu ilikuwa ni *commitment* ya Waziri wa Maji alifika katika Kata hii na katika kijiji hiki, je, Wizara hii pamoja na Wizara ya Maji wanaweza wakatupa ushirikiano *DDCA* wakatusaidia, kwa sababu wao wanafahamu ni wapi maji yanapatikana badala ya huyu Maswi akaendelea kutusumbua na wananchi wale wakapata maji?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nakubaliana na Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba huyu Mkandarasi wa awali anayechimba maji katika Kijiji cha Imbilili kwa kweli amekuwa akitusumbua sana, lakini hayo tutayafanyia kazi kwenye Baraza letu kama alivyoshauri. Naomba nifahamu Wizara iko tayari sasa kuangalia bili tunazolipa za maji katika Mji wetu wa Babati kwa sababu wananchi wetu wakilalamika sana, pamoja na upungufu wa maji lakini wanatozwa bili kubwa sana za maji. Je, Wizara hii na Wizara ya Maji mko tayari ku-*review* bili ambazo wananchi wa Babati wanalipa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Pauline maswali yako mengi ni yenu wenyewe Halmashauri, kwani Wizara ya Maji ndiyo inapanga bei za maji kwenye huko Halmashauri? Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kitaalam ni kweli kwamba huwezi kufanya utafiti mpya wa maji chini ya ardhi hasa kama unataka kuchimba visima wakati huu wa masika. Kwa hiyo, kama Mkandarasi ameomba muda kidogo apewe ambapo yupo asilimia 25 kwa sasa hivi, kama anapewa muda wa mwezi wa Tano anaweza akachukua muda wa mwezi mmoja kumalizia visima vile ambavyo alikuwa anachimba kwenye vile vijiji na ikiwezekana mwezi wa Sita au mwezi wa Saba akamaliza kazi ya kuchimba visima. Nashauri kitaalam apewe muda wa mwezi wa Tano na Sita ili kusudi aweze kukamilisha kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, kama Mkandarasi huyu Maswi

ataondolewa sasa hivi halafu wakaanza mchakato mpya wa kumpata kazi mtu mwingine wanaweza wakachukua miezi sita kukamilisha kumpata Mkandarasi ambayo itakuwa ni siyo faida sana kwa wananchi. Kwa hiyo, nashauri avumiliwe kidogo kwa kipindi hiki cha miezi miwili ama mitatu ili aweze kukamilisha kazi yake. Wizarani tutasukuma ili kusudi aweze kufanya kazi yake kitaalam zaidi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ningependa kuisifu sana Mamlaka ya Maji Mjini Babati, kama ambavyo imesifiwa pale ambapo Waziri Mkuu aliendа mwaka juzi waliisifu wao wenyewe BUWASA kwamba inafanya kazi nzuri na hata Mheshimiwa Diwani Sumaye ambaye anatoka kwenye Kata ile ya Sigino ambako hakuna maji kabisa, mbele ya Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema kwamba bwana kwa kweli tunashukuru wenzetu wa Mjini Babati wanapata maji vizuri, tatizo hapo ni bili.

Mheshimiwa Spika, ili kusudi ianzishwe bili, *EWURA* kabla hawajaidhinisha huwa wanafanya kitu kinaitwa mkutano wa wadau, wanajadili, wakishakubaliana wadau ndiyo bili ile inaidhinishwa. Kwa hiyo, nashauri Halmashauri kama inaona kwamba bili ni kubwa basi wawasiliane na *EWURA* kwa barua rasmi ili kusudi suala hilo liweze kutatuliwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, swali la Mheshimiwa Pascal Yohana Haonga Mbunge wa Mbozi kwa niaba yake, Mheshimiwa Selasini.

Na. 126

**Changamoto Zinazokabili Shule za Watu Binafsi**

**MHE. JOESPH R. SELASINI (K.n.y. MHE. PASCAL Y. HAONGA)** aliuliza:-

Shule za Watu Binafsi zinatoa huduma ya elimu kama

zilivyo Shule za Umma, lakini kwa muda mrefu zimekuwa zikikabiliwa na changamoto nyingi sana ikiwa ni pamoja na kodi ya majengo *(property tax)*, tozo ya *fire*, kodi ya ardhi na kodi nyinginezo:-

(a) Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuondoa baadhi ya kodi zisizokuwa na tija ambazo zimekuwa kero kwa shule za watu binafsi?

(b) Je, Serikali haioni ni wakati sasa wa kuzipatia ruzuku shule binafsi kwa sababu zinashirikiana na Serikali kupunguza tatizo la ajira?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pascal Yohana Hasunga, Mbunge wa Mbozi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua na kuthamini mchango wa sekta binafsi katika maendeleo ya elimu nchini ambapo hadi sasa jumla ya shule za msingi 1,432 kati ya shule 17,583 zinamilikiwa na sekta binafsi. Aidha jumla ya shule za sekondari 1,250 kati ya shule 4,885 zinamilikiwa na sekta binafsi. Vilevile kati ya vyuo vikuu 34, vyuo 22 vinamilikiwa na sekta binafsi. Kwa mchanganuo huo ni dhahiri kuwa sekta binafsi ina mchango mkubwa katika kuongeza fursa na ubora wa elimu nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikishirikiana na wamiliki wa shule binafsi kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili ikiwemo kodi na tozo. Katika kutatua changamoto hizo hadi kufikia sasa Serikali imeweza kuondoa tozo ya uendelezaji ujuzi *(Skills Development Levy-SDL)* tozo ya zimamoto, kodi ya mabango na tozo ya usalama mahali pa kazi *(OSHA)*.

Mheshimiwa Spika, hii ikiwa ni hatua ya Serikali

kuhakikisha kuwa sekta binafsi inakuwa na mazingira rafiki na wezeshi katika kuwaletea Watanzania maendeleo. Hivyo, Serikali kwa kushirikiana na umoja wa wamiliki wa shule binafsi itaendelea kujadiliana na kutatua changamoto zinawakabili ili kuvutia uwekezaji katika sekta ya elimu nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuzipatia ruzuku shule binafsi, Serikali itaendela kuboresha mazingira ya Taasisi za Fedha ili sekta binafsi iweze kupata mitaji kwa gharama nafuu huku Serikali ikiendelea kupunguza changamoto zilizopo katika shule za umma.

**SPIKA:** Mheshimiwa Selasini nilikuona.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, nnakushukuru na nashukuru kwa majibu ya Serikali. Kabla sijauliza maswali mawili ya nyongeza naomba tu jina la muuliza swali lisomeke kama Pascal Yohana Haonga siyo Pascal Yohana Hasunga. Baada ya masahihisho hayo kidogo naomba niulize maswali yangu mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, mara nyingi Serikali imekuwa ikizungumzia na kutoa matamko kuhusu ada zinazopangwa na shule za binafsi ikionesha kana kwamba Serikali ina mpango wa kuweka kiwango fulani cha ada bila kuzingatia gharama ambazo shule hizi zinaingia katika kusomesha wale watoto na kuendesha shule zao. Je, kwa nini Serikali isiwaachie wamiliki wakapanga hizi ada wenyewe ili wazazi ambao wanaweza wakamudu ada hizo waenda kwenye shule bila kikwazo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, mara nyingi shule zinapanga taratibu zao za namna ya kuwafanya hawa watoto waweze kufaulu, kwa mfano, kuwawekea mitihani kutoka kwenye daraja fulani kwenda kwenye daraja fulani, lakini Serikali pia inaonesha haifurahishwi na jambo hili. Je, kwa nini Serikali isiache hizi shule zikapanga utaratibu wa kuwafanya hawa watoto waweze kufaulu kulingana na sera na taratibu za shule zenyewe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa William Ole Nasha, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Serikali kutoingilia maamuzi ya shule za binafsi katika kuamua ada. Naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa Serikali inaendelea na majadiliano na sekta binafsi ya namna bora ya kuratibu suala hilo badala ya Serikali yenyewe kutoa maelekezo ya gharama ambazo zinatakiwa zilipwe.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu shule za binafsi zinaendeshwa na watu binafsi, lakini vilevile kwa sababu ni biashara na ni biashara ambayo maana yake mtu anayetaka kwenda kununua au kupata hiyo huduma yeye ndiyo aangalie uwezo wake, tunafikiri bado kuna busara ya kuendelea kujadiliana nao namna bora ya kuhakikisha kwamba kunakuwa na gharama ambazo zinahimilika badala ya Serikali yenyewe kuanza kutoa bei au gharama elekezi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili kwamba Serikali isiingilie taratibu za shule binafsi za kuweka viwango vya ufaulu. Wakati tunatambua kwamba ni kweli ni vizuri sekta binafsi katika uendeshaji wa shule ikaachiwa nafasi ya kuamua wenyewe namna wanavyodhibiti ubora. Ni kweli kwamba udhibiti wa ubora ni suala la kisera na kisheria, kwa hiyo, haiwezekani Serikali ikakaa moja kwa moja ikaruhusu kila mtu ajiamulie namna anavyodhibiti ubora katika shule yake.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa sasa ilichoamua ni kwamba tutaendelea kushirikiana na Umoja wa Wamiliki wa Shule Binafsi ili kuangalia namna ya kuboresha sheria na taratibu zilizopo ili ziwawezeshe kupata ubora ule, lakini bila kuvunja sheria za elimu kwa sababu hata kama shule ni za binafsi, lakini ni nchi moja, Serikali ni ile ile, sheria ni zilezile,

hatuwezi tukaruhusu kila mtu akajiamulia anavyotaka kwa sababu siyo kila mwenye shule binafsi amekuwa akitumia uhuru huo vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya wanafunzi wamefukuzwa shule kinyume na sheria, kuna wengine wanakaririshwa kwa kuonewa, kuna wanafunzi unakuta wa *Form Four* wanafukuzwa shule tu kwa sababu hajafikia kiwango fulani. Tunachosema ni kwamba tutaendelea kuwaruhusu kuboresha hayo mazingira, lakini sheria na taratibu lazima tuzifuate na ndiyo maana tunaendelea kufanya nao mjadala kwa pamoja.

**SPIKA:** Tunahamia Wizara ya Madini, Mheshimiwa Mpakate kwa swali linalofuata.

Na. 127

**Kutenga Maeneo kwa Wachimbaji Wadogo**

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza:-

Katika Mji wa Tunduru yako mabango mengi yanayoelezea ununuzi wa madini jambo linaloashiria upatikanaji mkubwa wa madini kutoka kwa Wachimbaji wadogo wadogo ambao hawatambuliwi kwa mujibu wa sheria:-

Je, ni lini Serikali itawatengea maeneo ya kuchimba madini na kuwatambua Kisheria Wachimbaji hao wadogo wadogo?

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. DOTTO M. BITEKO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini na kabla sijajibu swali hili naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Profesa Idris Kikula kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Tume mpya ya Madini.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Madini ya mwaka 2010 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2017 inawatambua wachimbaji wadogo. Kwa kutumia sheria hiyo Serikali inatoa leseni za uchimbaji za madini *(Primary Mining Licenses)* kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa kuna mabango na maduka mengi yanayotangaza uwepo wa madini ya vito katikati ya Mji wa Tunduru huko Mkoani Ruvuma. Baadhi ya madini ya vito hayo yaliyopo Wilaya ya Tunduru ni pamoja na *Sapphire, Ruby, Garnet* na kadhalika. Maduka ya madini yenye mabango ni ya wafanyabiashara wakubwa wenye leseni kubwa *(Dealers License)* ambazo huhuishwa kila mwaka kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013 Serikali ilitenga eneo la Mbesa, Wilaya ya Tunduru, lenye ukubwa wa hekta 15,605.3 kwa tangazo la Serikali Namba tano la tarehe 22 Februari, 2013, kwa ajili ya uchimbaji mdogo wa madini ya shaba. Hadi Aprili, 2018 jumla ya leseni hai 649 za wachimbaji wadogo wa madini yaani *(PML)* zimetolewa Wilaya ya Tunduru.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo kadri taarifa za utafiti katika maeneo hayo zitakavyoandaliwa na Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* kwa kushirikiana na Wakala wa Jiolojia Tanzania *(GST)* ili wachimbaji wadogo hao waweze kuchimba madini siyo kwa kubahatisha.

Mheshimiwa Spika, aidha, wachimbaji wadogo wanahimizwa kuomba leseni ili wafanye shughuli za utafutaji wa madini kwa mujibu wa sheria za nchi ili kuinua vipato vyao kutoa ajira kwa Watanzania, kuchangia pato la Taifa kupitia tozo mbalimbali zinazotokana na shughuli za madini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Tunduru, swali tafadhali.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pia nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, naishukuru Serikali kwa kutenga eneo la Mbesa kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Je, Serikali ina mpango gani ya kuwasaidia wale wachimbaji wadogo kwa maana ya kuwawezesha kimtaji na kuwajengea mtambo wa kuchenjulia madini ya shaba ili waweze kusafirisha yakiwa yamechenjuliwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Halmashauri ya Tunduru kama alivyojibu kwenye swali la msingi ina mabango mengi sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka mtaalam wa kufanya *valuation* ya madini haya ya *sapphire* ili Halmashauri ipate takwimu sahihi za usafirishaji wa madini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dotto Biteko.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. DOTTO M. BITEKO):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wachimbaji wengi wa madini wanahitaji kusaidiwa kimtaji kama alivyosema na hasa kwenye mnyororo mzima wa uongezaji thamani wa madini *(value addition)*. Nataka nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi hii Serikali inaifanya kwa umakini kwa sababu tuna historia mbaya hapo nyuma.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo walivyopatiwa mitaji kupitia ruzuku fedha nyingi sana hazikutumika kwa malengo yaliyokuwa yamekusudiwa. Kwa hiyo tunaangalia utaratibu mzuri zaidi kupitia mradi wetu wa *SMRP* kuona kwamba tunawasaidia wachimbaji wadogo nchini wakiwemo wachimbaji wa Tunduru.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kwamba tupeleke Mtaalam wa *valuation* Tunduru kwa ajili ya kufanya uthamini

wa madini ya vito, tunalichukua jambo hili na tunalifanyia kazi. Vile vile tutaandaa watu baada ya Tume ikishakuwa imekamilisha kazi zake za kuchukua watalaam ili tuweze ku-*station* mtu mmoja kwa ajili ya kufanya *valuation* pale Tunduru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vicky Kamata, swali linalofuata.

Na.128

**Mchango wa Makampuni ya Madini kwa Jamii**

**MHE. VICKY P. KAMATA** aliuliza:-

Kampuni kubwa za uchimbaji madini kama vile *GGM,* Buzwagi *Gold Mine* na North Mara *Gold Mine* licha ya kulipa kodi kwa Serikali kuu pia zinawajibika kuhudumia jamii inayozunguka migodi kwa utaratibu wa uwajibikaji kwa jamii kwa kutoa fedha au kufadhili miradi ya kijamii au maendeleo:-

(a) Je, kwa mwaka 2017 Kampuni hizo kila moja ilitoa fedha kiasi gani?

(b) Je, hadi kufikia Januari mwaka 2018, Kampuni hizo zimetoa kiasi gani.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Madini, napenda nijibu swali la Mheshimiwa Vicky Kamata, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 105(1) na (2) cha Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na marekebisho yake ya mwaka 2017, kinamtaka mmiliki wa leseni kuandaa mpango wa mwaka wa utaratibu wa uwajibikaji kwa jamii *(corporate social responsibility).* Mpango huo lazima ukubalike kwa

pamoja na Mamlaka ya Serikali ya Mtaa husika kwa kushauriana na Halmashauri ulipo mgodi kwa kuzingatia vipaumbele vya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya mpango huo yanapaswa kumshirikisha Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kabla ya kuidhinishwa na Baraza la Madiwani la Halmashauri husika. Aidha, kila Halmashauri ulipo mgodi inapaswa kuandaa mwongozo wa uwajibikaji kwa jamii kwenye Halmashauri yao, kusimamia utekelezaji wake na kutoa elimu kwa wananchi wa Wilaya husika juu ya huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu zilizopo, migodi ya Geita *Gold Mine,* Buzwagi *Gold Mine* na North Mara *Gold Mine* imekuwa inatekeleza jukumu hili la kutoa huduma za jamii zinazozunguka migodi hiyo. Huduma ambazo zimekuwa zinatolewa ni kwa maeneo ya afya, elimu, maji, mazingira, ujasiriamali, miundombinu na jamii kama vile barabara, majengo na masuala ya sanaa na utamaduni.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2017, mgodi wa North Mara ulitumia dola za Marekani 1,837,495, sawa na takribani shilingi bilioni 4.25 kwenye huduma za jamii. Mgodi wa Buzwagi ulitumia dola za Kimarekani 595,658.47, sawa na shilingi bilioni 1.38 na mgodi wa Geita *Gold Mine,* dola za Kimarekani 6,358,542.24 sawa na shilingi bilioni 14.45.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kumekuwa na changamoto za gharama halisi za miradi hiyo. Kunaonekana ziko juu sana ukilinganisha na gharama halisi ya kile kilichotekelezwa. Marekebisho ya Sheria ya Madini ya mwaka 2017 yaliyofanyika yanataka sasa Halmashauri zihusishwe katika kufanya maamuzi kuhusiana na mipango ya uwajibikaji kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2018, migodi hiyo mitatu imekwishaandaa mpango kazi wa utekelezaji wa uwajibikaji kwa jamii. Maandalizi ya mpango yameshirikisha

Serikali za Mitaa kama sheria inayowataka na kuwasilishwa kwa Halmashauri husika kwa ajili ya utekelezaji. Hadi kufikia Juni, 2018 mgodi wa Geita *Gold Mine* unatarajiwa kutumia kiasi cha dola za Kimarekani 1,932,142 na mgodi wa *North* Mara jumla ya dola za Kimarekani 333,111.39 na mgodi wa Buzwagi jumla ya Dola za Kimarekani 224,215.24

**SPIKA:** Mheshimiwa muuliza swali, Mheshimiwa Vicky Kamata.

**MHE. VICKY P. KAMATA:** Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Pamoja na majibu mazuri, nina swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa, *GGM* imekuwa ikitoa hili fungu la *CSR* kila mwezi kwa ajili ya kuhudumia hayo maeneo ambayo ameyataja katika maelezo yake ya msingi kwa maana ya elimu, afya, mazingira pamoja na wajasiriamali.

Mheshimiwa Spika, pia kwa kuwa, wamekuwa wakitoa kila mwezi hili fungu la *CSR* na kwa majibu haya inaonekana kwamba tangu Januari mpaka sasa *GGM* hawajatoa fungu hilo la *CSR* kwa maeneo hayo, nataka kujua kauli ya Serikali kwa wakati huu wa mpito kuhusiana na hawa waliokuwa wakisaidiwa na *GGM* kwa mfano, kituo cha Watoto Yatima cha Moyo wa Huruma wamekuwa wakisaidiwa pesa kila mwezi kwa ajili ya malazi ya wale watoto yatima, chakula, kuna mradi wa maji ambao kimsingi ni wa Serikali lakini *GGM* walikuwa bado wanaendelea kuutunza pamoja na ile hospitali inayotembea majini inayosaidia wanawake na watoto katika Visiwa kwa kuwa tangu Januari mpaka sasa pesa hazijatoka na imezoeleka kila mwezi huwa inatoka. Je, ni nini kauli ya Serikali katika kipindi hiki cha mpito?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa mnauliza maswali *very specific*, Waziri atajua kweli kama kampuni binafsi imetoa msaada kwenye eneo fulani *specific?* Mheshimiwa Naibu Waziri labda una picha ya kinachoendelea.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba baada ya marekebisho ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na marekebisho yake ya mwaka 2017, tulisimamisha utoaji wa fedha hizi mpaka pale Baraza la Madiwani katika Halmashauri husika wakae, wakubaliane utekelezaji sawasawa wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo *GGM,* pia nimeongea na *RAS* wa Mkoa wa Geita, ule mpango wa kupitia kwa Madiwani umeshakamilika na kuanzia leo wanaanza kuzitumia zile fedha kutokana na jinsi walivyokubaliana na Halmashauri husika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Wengine jamani hamna hata madini yenyewe sasa! Nitamchukua Mbunge wa Tarime Vijijini na Mbunge wa Geita Vijijini. Mheshimiwa Heche. *(Kicheko)*

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona. *CSR* ipo kwa mujibu wa sheria, lakini hii migodi wamekuwa wakionyesha kama ni hisani fulani wanawapatia wananchi. Kwa nini sasa Serikali isiwaagize hizi pesa zipelekwe moja kwa moja kwenye Halmashauri na zisimamiwe na Madiwani wetu katika kutekeleza miradi hii, kwa sababu unaona gharama zinazoandikwa ni kubwa kweli ukilinganisha na kazi halisi ambazo zinakuwa zinafanyika, yaani ziende kama vile kodi zingine zinavyoenda lakini zikiwa *specific* kama *CSR* ili zisimamiwe na Baraza la Madiwani? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Stanslaus Nyongo.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba hesabu zinazoonekana ni hesabu kubwa sana zilizotumika kuliko miradi yenyewe ilivyo, hilo tunakubaliana kabisa. Nimepita baadhi ya maeneo kwa mfano, *GGM* na *North Mara* tumewaagiza kwanza watupe taarifa ya utekelezaji wa zile fedha zilizotengwa kwa miaka miwili iliyopita ili

tujiridhishe tuone zile fedha zilizotengwa na wamepeleka wapi na nini kimefanyika. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kwa sababu hizi fedha za *corporate social responsibility* huwa zinatolewa kutokana na jinsi wao wanavyotengeneza faida na kwa sasa hivi ni sheria lazima watoe zile fedha. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na Madiwani husika wakakae na zile Kampuni waamue kwamba watekeleze miradi ile kwa jinsi wao walivyoweka kipaumbele chao.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna fedha ambayo inakwenda moja kwa moja kwenye Halmashauri, fedha hiyo ni *service levy* ambayo ni asilimia 0.3 ya mauzo ya madini wanayoyapata. Kwa hiyo, nadhani tu kwamba tuendelee kutoa ushirikiano na sisi kama Wizara ambayo tunasimamia Sheria ya Madini tutahakikisha kwamba zile fedha zinazotengwa zinakwenda zinavyostahili na Madiwani wasimamie utekelezaji wa miradi ambayo wamejipangia.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Madini nimekuona.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Napenda kuongezea majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini. Napenda kusema kwamba sheria ya sasa na kanuni kuhusiana na uwajibikaji kwa jamii ziko wazi.

Mheshimiwa Spika, niombe tu ushirikiano Waheshimiwa Wabunge pamoja na Halmashauri zetu za Wilaya na Miji waweze kutoa ushirikiano na kutupatia taarifa endapo wanaona kuna miradi imetekelezwa ipo chini ya viwango, lakini kiwango ambacho kimekuwa-*declared* ni kidogo kuliko fedha halisi ambayo inatamkwa kwamba imetumika.

Mheshimiwa Spika, pili; pamoja na maelezo aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba tumewataka *GGM* waweze kutoa maelezo na taarifa zao za miaka miwili,

tutaenda kwa migodi yote ambayo imekuwa ikifanya uwajibikaji kwa jamii na tutapitia na kukagua na yeyote ambaye ataonekana alifanya udanganyifu, hatua kazi za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Musukuma, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ni hivi juzi tu siku mbili, tatu zilizopita Wabunge wa Geita tumeletewa barua inayoonesha *CSR* iliyotolewa na *GGM* 2017/2018 dola 9,600,000 lakini katika majibu ya Waziri amesema ni dola milioni 6.5 na hizi barua ambazo tumeletewa tayari ziko kwa Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya na baadhi ya wananchi wameshazipata, lakini kwa majibu ya Wizara ina maana tunachanganyikiwa tujue ipi ni sahihi na ipi siyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, sasa ni nini kauli ya Wizara kuweza kuisaidia Halmashauri angalau kufanya *auditing* kujua uongo uko Wizarani au uongo uko mgodini. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusiana na takwimu

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba *GGM* tuliwaeleza tarehe 27 Februari, 2018 watuandikie *breakdown* ya kuonesha ni jinsi gani wametumia fedha za *CSR* na majibu waliyonipa ni kwamba kwa mwaka 2017 wametumia kama nilivyosema katika jibu la msingi dola 6,358,000. Mheshimiwa Musukuma anachosema dola milioni 9.7 ni jumla ya miaka miwili yaani mwaka 2016 na 2017 kajumlisha kapata 9.7 lakini swali la msingi limeuliza mwaka 2017 jibu ni milioni 6.358

Mheshimiwa Spika, ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Hawa Mchafu.

Na. 129

**Urithi wa Dunia-Kilwa Kisiwani**

**MHE. HAWA M. CHAKOMA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani juu ya urithi wa Dunia wa Kisiwa cha Kilwa Kisiwani?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kisiwa cha Kilwa Kisiwani kinapatikana katika Wilaya ya Kilwa Mkoa wa Lindi. Kisiwa hiki kina utajiri wa magofu ya kale yaliyoorodheshwa kwenye orodha ya Urithi wa Dunia mwaka 1981 na Shirika la Umoja wa Mataifa la Sayansi, Elimu na Utamaduni yaani *UNESCO.*

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha urithi wa Dunia wa Kilwa Kisiwani unaendelea kuwepo, Serikali imetekeleza mipango ifuatayo:-

(a) Kukarabati majenzi yaliyoorodheshwa kwenye Urithi wa Dunia. Ukarabati unafanywa na vijana wa Kitanzania kutoka Kisiwa cha Kilwa Kisiwani ambao wamepata mafunzo kutoka kwa wataalam wa *UNESCO.* Aidha, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara itajenga Ofisi itakayotumiwa na watumishi wa Urithi wa Dunia wa Kituo cha Magofu ya Kilwa Ksiwani na Songo Mnara.

(b) Kutangaza magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara ndani na nje ya nchi ili kuvutia watalii. Serikali imeandaa jarida la karibu Kilwa *(Kilwa District heritage resources)* linaloonyesha picha na maelezo ya vivutio vya utalii vilivyopo Wilayani Kilwa yakiwemo magofu ya Kilwa Kisiwani.

Jarida hili linatolewa kwa wageni wanaotembelea Kilwa pamoja na kutumika kutangaza utalii wa Kilwa katika maonyesho ya ndani ya Sabasaba na Nanenane.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali sasa imeandaa mpango wa kuuza utalii wa malikale na wanyamapori kwa pamoja yaani *one package*. Kilwa Kisiwani itanufaika na mpango huu kwa kuunganishwa na *package* ya Pori la Akiba la Selou.

(c) Kushirikisha jamii ya Kilwa Kisiwani kuhifadhi na kujipatia kipato kupitia malikale zilizopo kwenye Urithi wa Dunia. Serikali itawapa fursa za ajira na mafunzo katika fani ya ukarabati wa majenzi, kuongoza wageni, huduma za chakula na fani nyingine za ujasiriamali. Elimu waliyoipata itawasaidia kuanzisha ofisi ya kuongoza wageni Kilwa Masoko na wengine wanafanya kazi za ukarabati wa magofu ya Urithi wa Dunia Kilwa Kisiwani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. La kwanza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, atakumbuka mnamo mwaka 1981 Serikali ilikitangaza Kisiwa hiki cha Kilwa Kisiwani kuwa Urithi wa Dunia. Hadi kufikia mwaka jana Serikali ilipokea bilioni saba kutoka kwa wafadhili kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa miundombinu iliyopo Kilwa Kisiwani ili kuvutia watalii wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, nitapenda kupata majibu ya Serikali ni kwa nini sasa ujenzi wa miundombinu hii haujafanyika ilhali wameshapokea bilioni saba kutoka kwa wafadhali na pengine Serikali ingeweza kuongeza fedha ili huu ukarabati wa magofu unaoendelea uweze kwenda sambamba na ukarabati wa miundombinu?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi, watalii wengi zaidi

kutoka nchi mbalimbali duniani wangependa kutembelea urithi huu wa dunia, lakini hadi hivi tunavyozungumza hakuna kivuko cha kueleweka cha kuwavusha watalii kutoka Kilwa Masoko kwenda Kilwa Kisiwani, kitu ambacho kingeweza kuingizia mapato Serikali yetu. Nataka kujua sasa ni lini kivuko hicho kitajengwa kutoka Kilwa Masoko kwenda Kilwa Kisiwani ili kuinua kasi ya uchumi katika sekta hii ya utalii?

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo muhimu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii tafadhali. Bilioni saba mnayo iko wapi?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Kilwa Kisiwani tumepokea fedha zaidi ya bilioni saba kwa ajili ya ukarabati wa majenzi yaani ukarabati wa magofu yote ambayo yapo Kilwa Kisiwani. Naomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Kisiwa cha Kilwa Kisiwani kina magofu mengi sana na hizo bilioni saba bado ni kidogo.

Mheshimiwa Spika, hizi tulishaanza kuzifanyia kazi tayari, tumeanza ukarabati na hao vijana ambao wameshapata mafunzo mbalimbali kwa ajili ya kukarabati hayo majenzi wako kazini. Mimi mwenyewe tarehe 9 Machi, nilikuwa kule nikashuhudia jinsi kazi nzuri ambayo inaendelea kufanywa na wale vijana. Kwa hiyo, siyo kwamba zile fedha zimekaa, fedha zile zinaendelea tayari kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuhusu kivuko ni kweli kabisa nimeshuhudia katika lile eneo kwamba tukipata kivuko cha kisasa, kizuri kinaweza kikasaidia sana katika kuwavutia watalii ili waweze kufika katika lile eneo. Hivi sasa Serikali inaendelea kujipanga pale hali itakaporuhusu ya kifedha basi tutaweza kupata kivuko hicho ili kiweze ku-*promote* utalii katika aneo hilo la Kilwa Kisiwani.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza, tafadhali.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Mkutano wa *World Heritage* ambao ulifanyika nchini *Qatar,* Pori la Akiba la Selou na lenyewe lilitangazwa kama urithi wa dunia na nchi mbalimbali zilikubaliana kuisaidia Tanzania takribani dola milioni mbili kwa ajili ya kupambana na ujangili wa tembo. Nataka kujua *status* ya hali ya ujangili wa tembo katika Pori la Akiba la Selous?

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester umeleta swali jipya kabisa, hapa tunazungumzia utalii wa visiwani, majibu kama unayo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli kwa sasa hivi hali kidogo ni nzuri, hakuna tena ujangili kama ambavyo umekuwepo na ndiyo maana matukio mbalimbali yale ambayo tulikuwa tunapotelewa na tembo na maeneo mengine yamepungua kwa kiwango kikubwa sana katika hili eneo.

**SPIKA:** Nashukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, bado tuko Wizara hiyo ya Maliasili na Utalii, swali linaulizwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mbunge wa Kaliua.

Na. 130

**Hadhi za Hifadhi za Taifa**

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA** aliuliza:-

Serikali imeunda timu ya wataalam kutoka Wizara nne kupitia nchi nzima kuangalia hadhi za hifadhi zetu (Mapori ya Akiba na Hifadhi za Msitu) ili kuja na mpango utakaondoa kabisa migogoro ya ardhi inayotokea kati ya Hifadhi na Wafugaji, Wakulima na Hifadhi na watumiaji wengine.

(a) Je, ni lini kazi hiyo itakamilika?

(b) Je, mpaka sasa Timu hiyo imetembelea maeneo mangapi na ni mikoa gani?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Kaliua, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali iliunda timu ya Kitaifa kwa ajili ya kushughulikia migogoro ya ardhi hapa nchini. Timu hiyo ilijumuisha wataalam kutoka Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Maliasili na Utalii, Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Tume ya Taifa ya Takwimu.

Mheshimiwa Spika, kazi ya timu hii ni pamoja na kutembelea mikoa yote yenye migogoro; Kupitia na kuchambua kwa kina taarifa na mapendekezo yaliyowahi kutolewa na Kamati, Tume au timu mbalimbali kuhusu utatuzi wa migogoro nchini; Kuainisha vyanzo vya migogoro iliyopo; Kutembelea baadhi ya maeneo yenye migogoro ya muda mrefu pamoja na kukutana na wadau mbalimbali katika maeneo hayo; na Kutoa ushauri na mapendekezo ya utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa timu imefanikiwa kupitia taarifa mbalimbali za migogoro; kutembelea Wilaya 20, Halmashauri 24, Kata 40, Vijiji 74 na kufanya majadiliano na wadau 1,106 katika Mikoa ya Morogoro, Kagera, Geita, Tabora na Katavi. Taarifa ya Timu imekamilika na mapendekezo yamewasilishwa katika Wizara husika kwa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, jumla ya migogoro 1,750 ilifanyiwa uchambuzi. Kati ya hiyo 564 ilihusu uvamizi wa maeneo ya hifadhi; 218 mwingiliano wa mipaka ya kiutawala; 366 uanzishwaji wa vijiji ndani ya maeneo ya hifadhi; 204 migogoro ya matumizi ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji;

migogoro 206 ilihusu wananchi na wawekezaji kwenye maeneo ya ranchi, mashamba na migodi; na migogoro 115 inatokana na madai ya fidia. Vilevile kulikuwa na migogoro 77 ambayo inatokana na mchanganyiko wa vyanzo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara husika itaendelea kushirikiana na wadau wakiwemo wananchi kufanyia kazi mapendekezo ya timu ili kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi iliyopo na inayoendelea kujitokeza nchini. Ni matumaini yangu kwamba utatuzi wa migogoro kwa njia shirikishi utasaidia kuondoa migogoro iliyopo kati ya wananchi, maeneo yaliyohifadhiwa na wawekezaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sakaya, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kutokana na jibu la msingi tumeona namna gani ambavyo migogoro ni mingi hapa nchini. Migogoro hii inapoteza maisha ya Watanzania, migogoro hii inapoteza mali za Watanzania, watu wanafilisiwa mifugo yao, wanaharibiwa nyumba zao, wanachomewa vitu vyao, lakini pia migogoro hii inadumaza uchumi kwa kuwa watu wana - *concentrate* kwenye migogoro wanashindwa kufanya masuala ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nategemea Mheshimiwa Waziri baada ya kubaini matatizo haya aje na mpango mkakati, namna gani za haraka kutatua migogoro hii, tofauti anavyosema hapa wataendelea kushirikiana na wadau. Wakati timu zinaendelea kufanya kazi kubaini migogoro hii, bado Watanzania wameendelea kunyanyasika, wakati huu tunapoongea bado watu wanaendelea kunyanyaswa kwenye maeneo ya hifadhi, mipaka, mifugo yao inaendelea kupigwa mnada, vyanzo vinazidi kuharibiwa, nilitegemea wakati Serikali haijaja na mpango wa kutatua matatizo haya, wangesitisha kuendelea kunyanyasa watu ili wenyewe

wafanye kazi yao, ndiyo waendelee kushughulikia watu ambao wako ndani ya hifadhi ambapo wamesajiliwa kisheria?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, mwaka 2012/2013, Wizara ya Maliasili na Utalii ilinyang'anya vijiji 26 vyeti vya usajili kutoka Wilaya ya Kaliua kwa madai kwamba vimesajiliwa kinyume na utaratibu wakati walisajiliwa kisheria chini ya Wizara ya TAMISEMI, suala ambalo sasa hivi limeenda kuumiza uchumi wa wananchi wale kwa sababu makampuni ya tumbaku yamesema hayataingia mikataba ya biashara kununua tumbaku kwenye vijiji 26 kwa sababu havina vyeti vya usajili wa vijiji.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ya Maliasili ituambie itarudisha lini vyeti vya usajili kwa vijiji 26 ambavyo leo wanaenda kuathirika kiuchumi kwa kuwa walisajiliwa kisheria, wanaishi kisheria, kama lilifanyika kosa ni suala la Serikali?

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Magdalena Sakaya, majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nitoe taarifa kwamba siyo lengo la watumishi wetu walioko kwenye hifadhi kuwanyanyasa wananchi, kwa mujibu wa kanuni na taratibu hawaruhusiwi kufanya hivyo, kazi yao kubwa ni kuhakikisha wanalinda hifadhi na siyo kuwanyanyasa wananchi wanaozunguka katika maeneo hayo. Kwa hiyo kama kuna kesi kama hizo naomba tuwasiliane na Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kuwachukulia hatua stahiki hao ambao wanawanyanyasa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza kuhusu mpango mkakati nimeeleza kwamba timu hiyo baada ya kukamilisha hilo zoezi Wizara zote zinazohusika zimepewa hii taarifa kwa ajili ya kuanza kuweka mkakati wa makusudi kabisa wa

kutekeleza na kutatua migogoro ya namna hiyo. Hiyo kazi imeshaanza na kila Wizara ina mpango wake inatekeleza, sisi kama Maliasili na Utalii tumejipanga kwa ajili ya hiyo.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ni kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu alituagiza kuweka mipaka katika maeneo yote yenye migogoro, mipaka ile baada ya kuwekwa sasa Serikali inatathmini ni maeneo yapi yana migogoro, yapi yapo ndani ya hifadhi, yapi tunaweza kuyaachia, yapi lazima tuwape fidia wananchi na yapi tuwaondoe wananchi. Baada ya hiyo yote kukamilika, hatua stahiki zitafanyika na Mheshimiwa Mbunge atapata ule mpango wa Serikali kwa ujumla katika maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wananchi ambao Mheshimiwa Mbunge anasema walinyanga'anywa vyeti vyao wa usajili wa vijiji, hiyo taarifa naomba niseme bado sina lakini nitaifuatilia, nitashirikiana na Mheshimiwa Mbunge kuhakikisha kwamba angalau tunapitia na tuone tunashirikiana pamoja na Wizara zingine ili katika hivi vijiji 366 ambavyo viko ndani ya hifadhi tuone kama na hivyo navyo vipo ili kusudi tuone hatua itakayochukuliwa na Serikali, basi itahusu maeneo yote hayo pamoja na vijiji alivyovisema. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda tuvumiliane. Sasa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, swali linaulizwa na Mheshimiwa Almas Athumani Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini.

Na. 131

**Ujenzi wa Barabra ya Tabora- Mambali- Bukumbi- Shitage- Tulole- Kahama**

**MHE. ALMAS A. MAIGE** aliuliza:-

Barabara ya Tabora – Mambali – Bukumbi – Shitage - Tulole mpaka Kahama ipo katika mpango wa Serikali wa kujenga barabara za lami nchini:-

(a) Je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo utaanza?

(b) Kumekuwa na mvutano wa wapi barabara hiyo ingepita baada ya kufika Mambali, mapendekezo ya Bodi ya Barabara ya Mkoa ni kuwa barabara hiyo ipite Bukumbi, Shitage, Tulole na kuunga Kahama; Je, Serikali inatoa msimamo gani baada ya mapendekezo hayo ya Bodi ya Mkoa wa Tabora?

(c) Je, ni lini kipande cha barabara hiyo kitachukuliwa na *TANROADS*?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la Wanyamwezi. Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Almas Athuman Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ambayo ipo katika mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami ni ya Tabora – Mambali – Itobo - Kagongwa - Kahama yenye urefu wa kilometa 180. Barabara hii ipo katika hatua za mwisho za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ambapo kazi ya usanifu inafanywa na Mhandisi Mshauri *NIMETA Consult* na inatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Julai mwaka 2018. Baada ya kazi ya usanifu kukamilika Serikali itatafuta fedha ili kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupandishwa hadhi kwa barabara ya Mambali – Bukumbi - Shitage na Tulole tayari sehemu ya barabara ya Mambali hadi Bukumbi yenye urefu wa kilometa 28.5 ni barabara ya mkoa inayohudumiwa na

*TANROADS* na sehemu ya Bukumbi - Mhulidede kilometa 24.7 imekasimiwa kufanyiwa matengenezo na *TANROADS* kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya Mhulidede – Tulole kilometa 21 imeanza kuhudumiwa na *TANROADS* kuanzia mwaka huu wa fedha 2017/2018 na kufanya barabara yote ya Mambali – Bukumbi – Mulidede - Tulole - Kahama kuhudumiwa na *TANROADS*. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Maige, umeridhika tunaendelea.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa vile kipande cha barabara hiki cha Mambali – Bukumbi – Shitage - Mhulidede mpaka Kahama kupitia Tulole ni muhimu sana kiuchumi kwa sababu ya biashara ya mikoa miwili hiyo; Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami?

Swali la pili, ni lini uchambuzi yakinifu na usanifu utaanza kwa ajili ya barabara hiyo?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Elias Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia hii barabara, barabara hii ambayo anaizungumza kutoka Mambali – Bukumbi- inakwenda mpaka Mhulidede ni barabara ambayo inapakana na Jimbo la kwangu kule Ushetu. Kwa vile amekuwa akifuatilia barabara hii imewezesha hata kile kipande cha kilometa 21 nilichokitaja kwenda Tulole hadi Kahama Mjini ili kuleta ulinganifu na kuleta maana kimeanza kuhudumiwa.

Mheshimiwa Spika, namwomba tu Mheshimiwa Mbunge kwamba avute subira, Serikali imefanya juhudi kubwa sana kuunganisha mikoa na mikoa na kuunganisha mikoa na nchi jirani. Kwa vile kazi inaendelea vizuri nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote wa maeneo ya Bukumbi, Mhulidede, Mambali na majirani zake kule upande wa Bukene kwamba baada ya kazi nzuri ya kuunganisha mikoa sasa nguvu kubwa itaelekezwa kuunganisha barabara hizi ambazo zinaunganisha wilaya na mikoa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge avute subira baada ya kuwa kazi nzuri ya kuunganisha mikoa na nchi za jirani ikikamilika basi zoezi la usanifu kwa kipande hiki cha barabara kutoka Mambali ambacho kimsingi kitapunguza umbali wa mtu anayetoka Tabora kwenda Kahama kwa takribani kilometa 50.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuvute subira tutakuja kufanya usanifu na kuweza kujenga barabara hii. Usanifu utaanza baada ya kuwa tumejipanga vizuri na kuhakikisha kwamba, sasa tunafanya muunganiko wa sehemu hii ya barabara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Busokelo Fredy Atupele Mwakibete, uliza swali lako.

Na. 132

**Ukusanyaji wa Kodi na Malipo Mengine kwa Njia ya Mtandao**

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE** aliuliza:-

Hapa nchini kumekuwepo na ukuaji na utumiaji wa mifumo mingi mipya ya teknolojia kwa ukusanyaji wa kodi na malipo mengine kwa njia ya mtandao *(electronic)*:-

(a) Je, Serikali imejipangaje kukabiliana na wizi wa kimtandao kwa wananchi?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuundwa kwa Bodi ya wana TEHAMA nchini ili kuwa na udhibiti na ufanisi wa watumiaji wa mitandao nchini wanataaluma wa TEHAMA waweze kuwa na Bodi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, Mbunge wa Busokelo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua kadhaa kwa ajili ya kuweka mazingira salama kwa wananchi hususani kwenye mitandao kama ifuatavyo:-

(i) Mwaka 2015 ilitungwa Sheria ya Makosa ya Mtandao na Sheria ya Miamala ya kielektroniki kwa lengo la kutambua miamala inayofanyika kimtandao pia kutambua makosa yanayofanyika kwenye mtandao ili kuweza kuchukua hatua stahiki yanapobainika makosa hayo.

(ii) Kimeanzishwa kitengo cha uhalifu wa mitandao chini ya Jeshi la Polisi kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa makosa ya mitandao ikiwemo wizi kwenye mitandao na kuandaa majalada ya kufungulia mashtaka kwa kusaidiana na Kurugenzi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali.

(iii) Kupitia Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kimeanzishwa kitengo cha uratibu, ufuatiliaji na usimamizi wa matukio yanayotokea kwenye anga ya mtandao *TzCERT.* Kitengo cha *TzCERT* kinashirikiana kwa ukaribu na taasisi mbalimbali kama vile sekta ya fedha, mawasiliano, nishati , uchukuzi na jamii. Pia kinashirikiana na taasisi za kiintelijensia na kuhakikisha anga ya mtandao inakuwa salama.

(iv) Imeandaliwa mikakati ya Taifa ya usalama wa mitandao ambao unaweka bayana muundo wa Serikali kukabiliana na uhalifu wa mitandao.

(v) Mwisho elimu kwa umma imeendelea kutolewa.

(b) Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa matumizi ya TEHAMA nchini yemeongezeka ikiwa ni sambasamba na ukuaji wa sekta ya TEHAMA kama mojawapo ya sekta zinazokuwa kwa kasi. Kwa kutambua changamoto ya kutotambuliwa kwa wataalam wa TEHAMA nchini Serikali imefanya yafuatayo:-

(i) Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016 ambayo inaatamka kuwepo kwa mfumo wa kuwatambua na kuwaendeleza wataalam wa TEHAMA ili kuwa na rasilimali watu ya kutosha nchini ambayo inazingatia maadili na yenye uwezo wa kufanikisha jitihada za TEHAMA katika kujenga jamii maarifa na;

(ii) Kwa tamko la Rais la mwezi Novemba 2015 imeanzishwa Taasisi ya Tume ya TEHAMA *(ICT Commission)* ikiwa na lengo kuu la kukuza TEHAMA ambapo moja ya majukumu yake ni kusajili, kusimamia na kuendeleza utaalam wa wataalam wa TEHAMA nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Rungwe, swali la nyongeza.

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kabla sijauliza maswali yangu mawili ya nyongeza nataka niweke kumbukumbu sahihi kwamba mimi ni Mbunge wa Busokelo ambayo iko ndani ya Wilaya ya Rungwe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba kuna sera, kuna miongozo kuna vitengo mbalimbali vya kufuatilia *forensic* wizi wa mitandaoni, lakini bado wizi unaendelea; Je, Serikali

haioni sasa kuna umuhimu wa kuwatumia wataalam wetu wa ndani kushirikiana na nchi ambazo zimefanikiwa kutatua tatizo hili la wizi wa mtandaoni ikiwemo Israel ama India?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, sekta ya mawasiliano inachangia asilimia 13 ya pato la Taifa. Kwa msingi huo sekta hii ni muhimu sana, lakini Serikali bado haijaanzisha Bodi ya TEHAMA. Nchi ambazo zimefanikiwa katika TEHAMA kwa mfano Finland wamefanikiwa kugundua *Nokia* ukienda Korea Kusini kuna *Samsung*, ukienda Marekani akina Job Steve - *Apple* na Mataifa mengine mbalimbali. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuanzisha hii Bodi ya TEHAMA ili *professionals* ambao wamesoma hii TEHAMA waweze kutambulikana na kuongeza Pato la Taifa zaidi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo ya Mbunge Busokelo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mhandisi Atashasta Nditiye, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ni kweli kwamba wizi au uhalifu wa kimatandao bado unaendelea na kwa msingi huo Serikali tumejipanga kwamba tutawashirikisha wataalam wetu wa ndani.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitambue kwamba Mheshimiwa Mwakibete ni mtaalam sana wa mambo ya *ICT* na TEHAMA ambaye amefanya kazi maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi na hasa nchi za Ulaya ili kutengeneza *software* au *programs* ambazo zinaweza kupunguza au kumaliza kabisa tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa-*support* wataalam wetu kwenda kujifunza nje ya nchi kwa nchi ambazo zimefanikiwa tatua tatizo hili, nchi kama Israel, India na Marekani. Tutambue tu kwamba uhalifu wa mtandao ni kitu ambacho kipo dunia nzima na jinsia ambavyo siku zinakwenda watu wanagundua njia mpya na Serikali

tunawa-*support* wananchi na wataalam mbalimbali kuhakikisha kwamba wanatafuta *programs* za kuzuia uhalifu huo.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, ni kweli kwamba kumekuwa na utitiri wa watu wengi sana wanaojifanya kwamba ni wataalam wa TEHAMA na kwa sasa kuna umuhimu kama Serikali wa kuunda bodi ya kusimamia wataalam wa TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo kupitia Kamisheni ya TEHAMA ambayo ilitangwazwa na Mheshimiwa Rais mwaka 2015 tunaamini ndani yake tutaunda Bodi ambayo itawatambua wataalam wa TEHAMA kwa elimu zao, lakini tutahakikisha vilevile wanafanya mitihani ili kuwa *competitive* katika masuala mazima ya TEHAMA kama ilivyo Bodi ya Uhasibu *NBAA* au Bodi ya Wahandisi ya *ERB*.

**SPIKA:** Tunaendelea na maswali ya mwisho kwa siku ya leo. Waheshimiwa Wabunge, hata ninyi wenyewe mkijisikiliza tu hapo mtasikia jinsi ambavyo kuna kelele nyingi sana humu ndani. Nawaombeni sana mpunguze sauti wale ambao mnaongea.

Tunaendelea na Wizara ya Nishati, swali linaulizwa na Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Busega tafadhali.

Na. 133

**Kuwapatia Umeme Wananchi wa Vijiji vya Jimbo la Busega**

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI** aliuliza:-

Vijiji vya Nyakaboja, Kabita, Chumve, Kalemela, Kalago, Badugu na Nyaluhande vimepitiwa na nguzo na nyaya za umeme, lakini wananchi hao hawana huduma ya umeme:-

Je, ni lini Serikali itawapatia umeme wananchi wa maeneo hayo ili wasiendelee kuwa walinzi wa nguzo za *TANESCO?*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Busega ina Vijiji 59, kati ya vijiji hivyo vijiji 18 vimepatiwa umeme kupitia miradi ya *Electricity V* na *REA* Awamu ya II. Kijiji cha Kalemela kilipatiwa umeme kupitia *REA* Awamu ya Kwanza. Kijiji cha Badugu kimepatiwa umeme kupitia mradi wa *Electricity V* na baadhi ya maeneo ya Kijiji cha Nyaluhande vimepitiwa umeme kupitia mradi wa *REA* Awamu ya Pili.

Mheshimiwa Spika, Vijiji vya Kabita, Nyakaboja na Kalago vitapatiwa umeme kupitia mradi wa *REA* Awamu ya Tatu mzunguko wa kwanza ambao utekelezaji wake umekwishaanza kupitia Mkandarasi *White City Guangdong* JV *Limited.* Kazi za mradi wa kupeleka umeme katika Wilaya ya Busega zinajumuisha ujenzi wa kilometa 49.7 za njia ya umeme, msongo wa kilovoti 33, kilometa 116 za njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 0.4, ufungaji wa *transforma* 58 na kuunganisha wateja wa awali 1,783. Gharama za mradi ni shilingi bilioni 5.5. Mradi unatarajiwa kukamilika Julai, 2019.

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Chumve pamoja na vijiji vingine vilivyobaki vitapatiwa umeme kupitia mradi wa *REA* Awamu ya Tatu mzunguko wa pili unaotarajiwa kuanza mwezi Julai, 2019 na kukamilika mwezi Juni, 2021.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chegeni, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza napenda

nipongeze majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na kazi inayofanywa na Wizara hii ya Nishati katika kuwapatia umeme Watanzania. Hata hivyo, nina maswali madogo mawili:

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; pamoja na jitihada hizi kuna vijiji 10 vimesahaulika, Vijiji hivi ni kama Mwamigongwa, Rwangwe, Ilumya, Igabulilo, Mwamalole, Mwabayanda, tayari tulishaongea na Wizara kwamba kuna vijiji ambavyo katika mzunguko huu vimerudiwa kutajwa majina tena, tukasema wafanye *substitution*; Je, Wizara inalifanyaje suala hili ili kusudi vijiji hivi ambavyo vimerudiwa visirudiwe tena na ambavyo havina umeme viweze kupatiwa umeme? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa umeme unasambazwa na moja ya agizo ni kwamba Taasisi za Serikali ziweze kupata umeme huu ikiwemo zahanati, shule na kadhalika na kuna baadhi ya maeneo ambayo umeme hu unasambazwa kwa mitaa michache. Je, nini kauli ya Serikali kuhakikisha kwamba umeme unasambazwa kulingana na mahitaji ya watumiaji? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa. Kwanza nimpongeze sana kwa kazi nzuri ya kufuatilia miradi ya nishati katika Jimbo lake, lakini la pili amevitaja vijiji kumi ambavyo kwa maelezo yake vimesahaulika na ameunganisha hapo na vijiji ambavyo vimetajwa kwenye *REA* Awamu ya Tatu mzunguko wa kwanza ambapo inaonekana vina miundombinu ya umeme.

Mheshimiwa Spika, msimamo wetu wa Wizara ni kwamba vijiji vyote vyenye miundombinu ya umeme ambavyo vipo kwenye Awamu ya Tatu mzunguko wa kwanza vifanyiwe marekebisho na vijiji ambavyo havina miundombinu ya umeme. Kwa kuwa, amevitaja vijiji vyake

kumi na kwa kuwa ameshafanya mawasiliano na Wizara na *REA* kwamba nia ya mradi huu wa Awamu ya Tatu ni kupeleka umeme kwenye maeneo ambayo hakuna miundombinu. Kwa hiyo, nataka niwaelekeze *REA* kwamba wafanye *substitution* kwa sababu ni jambo la kawaida na tumekuwa tukifanya katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, ametaka tamko la Serikali juu ya maeneo ya Taasisi za Umma, ni kweli tumetoa tamko, tulitazama upungufu wa *REA* awamu zilizopita kwamba Taasisi nyingi za umma ikiwemo miradi ya maji, ikiwemo zahanati, vituo vya afya zilirukwa. Kwa hiyo, mradi wa *REA* Awamu ya Tatu tuliona tusirejee changamoto za *REA* awamu zilizopita.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naendelea kusisitiza agizo la Wizara na Serikali kwamba maeneo ya Taasisi za Umma yapatiwe vipaumbele katika kupeleka miundombinu ya umeme. Naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo hili la Busega na maeneo yote kwamba hilo ndiyo tamko la Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Swali la mwisho kwa siku ya leo Waheshimiwa Wabunge linaulizwa na Mheshimiwa Philipo Augustino Mulugo, Mbunge wa Songwe, kwa niaba yake Mbunge wa Mbeya Vijiji, tafadhali.

Na. 134

**Usambazaji Umeme – Vijiji vya Wilaya ya Songwe**

**MHE. ORAN M. NJEZA (K.n.y. MHE. PHILIPO A. MULUGO)** aliuliza:-

Wilaya ya Songwe ina jumla ya vijiji 43 lakini mpaka sasa hakuna kijiji hata kimoja chenye umeme kwa mpango wa umeme wa *REA* toka awamu ya kwanza na ya pili:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inatoa upendeleo maalum kwa vijiji vya wilaya hii mpya katika awamu ya tatu ya *REA?*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Philipo Augustino Mulugo, Mbunge wa Songwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Songwe lina jumla ya vijiji 43 ambapo kati ya vijiji hivyo, sita vilipatiwa umeme kupitia mradi wa *REA* awamu ya kwanza na Vijiji 14 vya Ilasilo, Galula, Kanga, Mbala, Iseche, Majengo, Tete, Ifenkenya, Nahalyongo, Chang'ombe, Ifuko, Maamba, Songambele, Totowe na Mbuyuni vilipatiwa umeme kupitia mradi wa *REA* Awamu ya Pili.

Mheshimiwa Spika, Vijiji vya Itiziro, Undinde, Mbangala, *CHUDECO,* Kambarage, Ilasilo, Kaloleni, Ndanga na Mwagala ni miongoni mwa vijiji 14 vinavyotarajiwa kunufaika na utekelezaji wa mradi wa *REA* awamu ya tatu mzunguko wa kwanza. Utekelezaji wa mradi huu ulianza mwezi Julai, 2017 ambapo Mkandarasi *M/S STEG International Services* alipewa kazi za mradi katika Mkoa wa Songwe. Kazi zinazofanyika kwa sasa ni pamoja na kuleta vifaa katika maeneo ya mradi. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2019.

Mheshimiwa Spika, wigo wa mradi katika Jimbo la Songwe unajumuisha ujenzi wa kilometa 46.64 za njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 na kilometa 52.09 za njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4, ufungaji wa transforma 14 na kuunganisha wateja wa awali 3,980. Gharama za mradi ni shilingi bilioni 13.05.

Mheshimiwa Spika, vijiji vilivyobaki vitapatiwa umeme kupitia mradi wa *REA* Awamu ya Tatu mzunguko wa pili unaotarajiwa kuanza kutekelezwa mwezi Julai, 2019 na kukamilika mwezi Juni, 2021.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oran Njeza nilikuona. Swali la nyongeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Wizara. Nikiri kweli kuwa wamefanya kazi nzuri ila katika haya majibu kuna Kijiji cha Mbuyuni bado hakijapata umeme pamoja na kuwa kimeorodheshwa kuwa kimo kwenye orodha ya vilivyopatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni umeme uliokwenda Idunde umeruka Vijiji vya Rukwa na Kapalala; Je, ni lini Serikali itahakikisha hivi vijiji vilivyobaki vya Kapalala, Mbuyuni na Rukwa vitapatiwa umeme ikiwa ni pamoja na vijiji vya Kata ya Ikukwa ambayo ni karibu sana na Jimbo la Songwe navyo vitapatiwa umeme?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nakiri kuwa Serikali imefanya kazi nzuri ya kupeleka umeme vijijini, lakini kwa mazingira ya vijijini wanahitaji vilevile huduma kutoka *TANESCO;* Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kuwa kutakuwa na huduma kwa wateja ambazo zitakuwa karibu huko vijijini ili waweze kupata huduma pamoja na hii huduma nzuri iliyofanyika kwa mpango wa *REA?*

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Oran. Majibu ya maswali hayo kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Subira.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na namshukuru sana Mheshimiwa Njeza kwa maswali yake mawili ya nyongeza. Nampongeza pia kwa kazi nzuri kwenye Jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, katika maswali yake la kwanza amejielekeza kwenye Kijiji cha Mbuyuni ambacho anasema

kiko kwenye orodha ya vijiji vyenye umeme, lakini pia hakina umeme. Naomba hili nilichukue ili tuweze kufuatilia takwimu hii na nitampa majibu ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, pia, katika swali lake hilo alielekeza vijiji ambavyo vimerukwa ikiwemo vijiji vya Kata ya Ikukwe. Naomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi vijiji vyote vilivyosalia 7,873 nchi nzima vitapata miundombinu ya umeme kwa mizunguko. Mzunguko wa kwanza na mzunguko wa pili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, vile 3,559 vya mzunguko wa kwanza kazi inaendelea mpaka Julai, 2019 kisha tunaanza mradi wa *REA* awamu ya tatu mzunguko wa pili. Kwa hiyo naomba nimthibitishe Mbunge maeneo ambayo yaliyosalia yatapatiwa miundombinu ya umeme kupitia *REA* awamu ya tatu mzunguko wa pili.

Mheshimiwa Spika, ameuliza suala la namna gani wananchi wa maeneo ya vijijini watapata huduma ya *TANESCO.* Naomba nilithibitishie Bunge lako Tukufu kuwa, kazi ya kupeleka miundombinu ya umeme inahusu vijiji vyote na tunatambua baadhi ya vijiji viko mbali na ofisi zetu za *TANESCO* ambazo ziko kila Wilaya, tumeielekeza *TANESCO* kufungua ofisi ndogo ndogo kwenye miji mikubwa na miji ambayo iko karibu na maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nikuthibitishie hilo linafanyika na tumeshapokea orodha ya ofisi za *TANESCO* ndogondogo mpya ambazo zingine zitajengwa lakini pia tumeomba pale ambapo, maana yake ujenzi ni suala la muda mrefu, lakini pale ambapo kuna maeneo ya vijiji kwenye Kata kuna Ofisi za Watendaji wa Kata, basi kipindi ambacho wataanza kuunganisha wateja tumeomba *TANESCO* waende kutumia hizo ofisi kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi wetu na nia ni kurahisisha utoaji wa huduma hizi kwa wananchi wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge. Swali la Mheshimiwa Njeza linakuwa ndiyo la mwisho, Mheshimiwa Njeza, hapa Dodoma jina lako tafsiri yake ni 'nimeonja' sijui Mbeya tafsiri yake ni nini?

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Naomba niwatambulishe wageni walioko katika *Gallery* ya Spika ambao ni Viongozi wa Kamati ya Hesabu za Serikali, *(Public Accounts Committee)* kutoka Bunge la Malawi. Tunaye Mwenyekiti wa Kamati hiyo Ndugu Alekeni Menyani, *Chairperson of PAC* Malawi *Parliament.* Hawapo? Wageni wetu wa kutoka Malawi hawapo? Amenyanyua mkono eeh? Ah! Basi vizuri sana.

Pia yuko Makamu wa Mwenyekiti wa *PAC,* Kamlepo Kaluwa, *thank you.* Mkaguzi Mkuu, Gerald Pute, Mkaguzi Mwandamizi na Afisa Uhusiano Rabson Kagwamminga lakini pia Katibu wa Kamati ya *Public Accounts Committee* Fredrick Kamwani. Ahsanteni sana na karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia, kwenye jukwaa hilo tuna wageni waliotutembelea ambao ni ndugu Joseph Kusaga, Mkurugenzi Mtendaji wa *Clouds Media Group;* pia ndugu Maharage Chande, Afisa Mtendaji Mkuu wa *Multichoice* Tanzania. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni wageni sita wa Katibu wa Bunge ambao ni Madaktari kutoka hospitali ya Saratani ya *Ocean Road* wakiwemo pia wale wa kutoka Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili walioletwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF)* kwa ajili ya uchunguzi wa afya za Waheshimiwa Wabunge. Karibuni sana popote pale mlipo. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa William Tate Ole Nasha, Naibu Waziri, Elimu, Sayansi na Teknolojia ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimboni kwake Ngorongoro. Karibuni sana ndugu zetu wa kutoka kule Ngorongoro. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Elias Kwandikwa, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambao ni ndugu zake walioambatana na Mke wake Dkt. Merceline Mumbee. Karibu sana shemeji. *(Makofi)*

Pia kuna wageni nane wa Mheshimiwa Daniel Mtuka ambao ni Wajumbe wa Bodi ya *CoST* kutoka Dar es Salaam na London wakiongozwa na Mwenyekiti wa *CoST* ndugu Christiaan Poortman. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 12 wa Mheshimiwa Allan Kiula ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM kutoka Mkalama, Mkoani Singida, wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya ndugu Jackson Masaka. Karibu sana popote pale mlipo. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Hassan E. Masala ambaye ni ndugu yake kutoka Nachingwea Mkoa wa Lindi ndugu Abdallah Lilunguzu. *(Makofi)*

Tuna wageni 21 wa Mheshimiwa Esther L. Midimu ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Daimu I. Mpakate ambaye ni mke wake, ndugu Happiness Ngwango kutoka Tunduru Mkoa wa Ruvuma. Ahsante sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Marwa Chacha ambao ni wananchi kutoka Serengeti Mkoa wa Mara. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Mendrad Kigola ambao ni Viongozi wa Wilaya ya Mufindi Mkoa wa Iringa. Karibuni pia. *(Makofi)*

Wageni 35 wa Mheshimiwa Omary Badwel ambao ni wanafunzi 29 na Walimu sita kutoka shule ya sekondari Mtitaa iliyopo Bahi Mkoani Dodoma. Ahsante. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni watatu

wa Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika ambao ni watoto wake kutoka Zanzibar. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliotutembelea kwa ajili ya mafunzo ambao ni wanafunzi 80 kutoka Chuo cha Afya na Maendeleo ya Jamii kilichoko Mkoani Dodoma. Karibuni sana wanachuo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Anna Lupembe anawataarifu wana maombi kwamba leo hakutakuwa na shughuli ya ibada badala yake itafanyika siku ya Ijumaa.

Pia Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi anawakumbusha Waheshimiwa Wabunge wote kwamba lile zoezi la kupata *passport* za kisasa hizi, lile zoezi litaendelea na mashine zinazohusika na zoezi hilo ziko kwenye Ofisi ya Uhamiaji za Mkoa, lakini ili upate *passport* hiyo Waheshimiwa Wabunge unatakiwa uende na viambatanisho kama vinne hivi.

Kwanza, barua ya utambulisho au kitambulisho cha Mbunge, kama huna kitambulisho umekisahau mahali unachukua barua kwa Katibu wa Bunge pale. Kingine unachotakiwa uwe nacho, cheti za kuzaliwa...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**SPIKA:** Ah! Bado tunaendelea mbona mnaguna Waheshimiwa? Kama huna cheti za kuzaliwa basi kiapo kutoka kwa Wakili au Mahakamani huko. Halafu upeleke cheti za kuzaliwa cha mmoja wa wazazi wako. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri, kama rafiki zangu Wasukuma sasa wanatoa wapi cheti za kuzaliwa cha wazazi wao. Halafu kivuli cha *passport* uliyonayo. Mheshimiwa Waziri haya masharti mengine kwa mazingira ya Tanzania hasa ya wazazi tabu kweli. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tuendelee na shughuli zetu.

## MWONGOZO WA SPIKA

**SPIKA:** Leo Mbarouk sitakuruhusu kwa sababu umegeuza sasa kuwa mchezo wa kila siku. Mheshimiwa Waitara tuanze na wewe.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, natumia kanuni ya 68(7). Naomba mwongozo wako kwa sababu kwenye gazeti la leo Mtanzania tarehe 24 Aprili, 2018 na hata hivyo jana pia Mheshimiwa Waziri wa Nchi, alikuwa anaongea na waandishi wa habari, ambayo imetokea sana kwenye magazeti ya leo, Kauli za Mawaziri na...

**SPIKA:** Waziri wa Nchi kwa maana ya...

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**SPIKA:** Okay, ahsante.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, alikuwa anaongea na waandishi wa habari kama ilivyokuwa ni mwendelezo wa Mawaziri mbalimbali wanazungumza habari ya taarifa ya CAG. Sasa naomba mwongozo wako kwa sababu ukiuliza wanasema taarifa hizi zikishatoka inabidi ziende Serikalini, Serikali watafute majibu kwa maana ya wahusika waende kwa zile Kamati husika za Kisekta za Bunge hili na baadaye taarifa hiyo itakuja tujadili kama Bunge na kutoa maelekezo kwa Serikali kwa mujibu wa Katiba.

Mheshimiwa Spika, lakini mijadala inayoendelea ya juu ya fedha trilioni 1.5 maana yake ni kama Wabunge tumechanganywa na wananchi pia wamechanganywa. Sasa ni utaratibu upi unapaswa kufuatwa katika kujadili mambo haya? Ni kila Waziri anajibu na baadaye itakuja taarifa au kila mtu anasema la kwake?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba mwongozo wako kwa sababu Kamati ya *PAC* ipo ambayo inafanya kazi

kwa niaba ya Bunge zima, wangefanya mchakato huu ili sote tujue; kwa sababu wapo wanaosema fedha zimeibiwa na wengine wanasema fedha hazijaibiwa, kwa hiyo kuna mkanganyiko mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba mwongozo wako, kwa sababu tunaendelea kusoma hizi taarifa; kwa mfano jana, Mheshimiwa Jenista Mhagama yeye alijikita sana kuzungumza habari ya vyama na hasa CHADEMA kwamba fedha zimeibiwa; lakini ukisoma humu vyama vimetajwa tisa na ameandika ukurasa anazungumza Chama cha Mapinduzi na mikopo iliyotolewa bila viambatisho.

Mheshimiwa Spika, sasa hatusemi fedha zimeibiwa lakini utaratibu upi ufuatwe? Haya mambo yaliyozungumzwa kwenye vyama, kwenye idara mbalimbali, amefanya kazi kubwa sana, wamekagua kila mahali, ukiangalia hata kwenye Balozi zetu, Balozi 21 zimekusanya fedha anasema hazikupelekwa kwenye Mfuko Mkuu. Sasa ili tusichanganye wananchi tungepata mwongozo wako, utaratibu wa kufuatwa, kauli ya Serikali ni ipi, Wabunge waseme nini kama Taifa tusimamie kitu gani?

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako katika jambo hili. Ahsante sana.

**SPIKA:** Nadhani hili Mheshimiwa Naibu Spika aliwahi kutoa mwongozo wake hapa nyuma na maelezo ni haya haya hatuwezi kuwafunga midomo Mawaziri, wanatoa maoni yao. Hawajasema hapa, wamezungumza huko walikozungumza. Kwa hiyo wanaendelea tu wala hamna shida na utaratibu wetu wa kawaida unaendelea tu na Mwenyekiti wa *PAC* yupo.

Waheshimiwa Wabunge, hapa hakuna tatizo, Bunge linaendelea na mchakato wake kama kawaida, anayeamua kuzungumzia naye anazungumzia kama kawaida wala hamna shida. Kama CHADEMA imetajwa, basi nimemsikia hata mwakilishi wa CHADEMA naye akieleza kwamba

hawajala hela, hawajafanya hivi, kwa hiyo wote wanaendelea tu, hakuna shida, hakuna mgongano.

Mheshimiwa Amina Mollel

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nasimama kwa kanuni ya 68(7) na ni kuhusu tangazo ulilotoa hivi sasa kuhusu upatikanaji wa *passport* kwa Waheshimiwa Wabunge pia hata wananchi wengine wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, kila siku nimekuwa nikitoa kilio changu hapa kuhusiana na miundombinu hasa katika majengo na mojawapo ni jengo la uhamiaji hapa mkoani ambalo kama ulivyosema mashine zinapatikana katika Ofisi ya Mkoa Uhamiaji hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, jengo hilo lipo ghorofa ya nne na jengo hilo ngazi zake ni za zamani sana kwa mtu kama Mheshimiwa pacha wangu Mheshimiwa Ikupa, binafsi mimi, Mheshimiwa Lulida na wananchi wengine wenye ulemavu hivi wanafikaje katika jengo hili kuweza kupata hizo *passport?* Kwa sababu haki ya kupata passport kwa yeyote yule mwenye kutimiza vigezo ni wajibu wake lakini tunawasaidiaje wakati mazingira yenyewe...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mollel una maana ya hilo jengo la uhamiaji au?

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, uhamiaji pale. Kwa hiyo, naomba mwongozo wako na kwa sababu Waziri yupo hapa atueleze sasa sisi ambao wenye mahitaji tunapandaje kule juu? Hakuna lifti katika jengo la uhamiaji.

**SPIKA:** Nadhani ni *point* aichukue tu, ni *point noted* kabisa ataifanyia kazi, haina shida. Mimi nilifikiri unafanya ombi maalum kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa sababu wana *passport* basi wao wabadilishiwe *passport* kwa *passport* badala ya... *(Makofi)*

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, hata hilo pia, nilikuwa nakwenda huko huko lakini unajua kwa sababu masuala ya watu wenye ulemavu mara nyingi sana haki zao zimekuwa haziangaliwi kwa jicho la pili, kwa hiyo najikuta wakati mwingine nalemewa zaidi huko lakini...

**SPIKA:** Hapana hatukulaumu hata kidogo, tunasema ni *point* muhimu imeshachukuliwa na hapa Mheshimiwa Waziri ame...

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nilichokuwa nataka kuongezea pia ni kwamba Wabunge kwa sababu tayari wanazo *passport* zipelekwe tu ili kuona utaratibu ni jinsi gani ya kupatiwa hizo *passport* nyingine badala ya hizo *documents* nyingine zote zinazohitajika.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Sasa bahati mbaya hukutoa hoja ili uungwe mkono. (*Kicheko)*

Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pia naomba mwongozo kwa hiyo kanuni ya 68(7) ambayo inatokana na swali la Mheshimiwa Paschal Haonga na Waziri wa Elimu alijibu swali lake la nyongeza kuwa kuna wanafunzi wanarudishwa madarasa kwa sababu ya kuonewa.

Mheshimiwa Spika, naomba tu niipe taarifa Wizara kuwa tabia hii ya kurudisha madarasa wanafunzi kwa kuwaonea ipo vyuo vikuu na hasa wanafunzi wetu, dada zetu wa kike. Katika vyuo vikuu kuna Walimu wanajulikana kabisa kuwa huyu Mwalimu ni dume la mbegu kuwa mwanafunzi kama hatoi hawezi kufaulu na kuna Walimu kabisa wao wanajulikana wanataka pesa. Kwa hiyo naiomba Wizara baada hii nguvu kuelekezea shule za sekondari sasa waelekeze katika vyuo vikuu kwa wanawake ambao wanaonewa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Olenasha umepokea hiyo maneno eh!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, nimepokea, lakini maneno ambayo Mhemiwa Mlinga ameyatumia yalinifanya niwe nasikiliza ukakasi zaidi wa yale maneno kuliko hoja yake. Kwa hiyo nitakutana naye nijaribu kujua alikuwa anataka kusema nini.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nitamshauri tu vilevile mdogo wangu kwamba hili ni Bunge kwa hiyo siku nyingine aangalie lugha ambayo anatumia, kwa sababu kwa kweli ameongea maneno ambayo siyo ya Kibunge, lakini hoja yake hiyo nitaenda kuzungumza naye nielewe vizuri zaidi

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa Katibu tuendelee.

**PAMELA PALLANGYO-KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2018/2019 - Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Ahsante. Kabla majadiliano hayajaendelea tunaye mgeni kwenye *Gallery* ya Spika, ambaye naomba nimtambulishe, naye ni Balozi wa Morocco hapa nchini Tanzania, Mheshimiwa Abdallah Berian, karibu sana sana na baadaye tutaonana kidogo ili tuongelee habari ya ujenzi wa uwanja wa kisasa hapa Dodoma. *(Makofi)*

Ahsante sana, uchangiaji unaendelea, tuanze na Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la barabara, lakini kwanza nianze na fedha iliyotengwa kwa ajili ya Mfuko wa Barabara kwa Mkoa mzima wa Tabora. Kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri ukiangalia fedha iliyotengwa kwa Mkoa wa Tabora barabara za ndani ni milioni mia nane themanini na tano tu, lakini ukiangalia Mkoa wa Tabora kwa Tanzania ndio mkoa unaoongoza kuwa mkubwa kwa sasa hivi kuliko mikoa yote na ni mkoa ambao una mzunguko mkubwa sana wa barabara tofauti na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, fedha iliyotengwa na hali ya barabara za Mkoa wa Tabora ni hatari sana kwa mwaka huu mzima. Iko mikoa mingine wamepata mpaka bilioni mbili, tatu, moja *point*, kwa Mkoa wa Tabora kuwapa milioni mia nane themanini na tano ni fedha kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wizara iuangalie Mkoa wa Tabora kwa jicho la pekee. Hivi tunavyoongea kuna maeneo ambayo hayapitiki kabisa wananchi wanaogelea, hali ya uchumi ni mbaya, mazao hayasafirishwi kwenda mjini kwa sababu barabara zile ni mbovu sana.

Mheshimiwa Spika, *specifically* nizungumzie barabara ya kutoka Kaliua na hasa eneo ambalo linatoka pale Kazilambwa Kaliua kwenda Chagu ambako ni mpakani mwa Uvinza Mkoa wa Kigoma. Barabara hii ni mbaya sana na nimekuwa nikiomba ipatiwe fedha za kujengwa kwa kiwango cha lami. Hivi ninavyoongea na wiki nzima iliyopita sikuwepo hapa Bungeni kwa sababu nilikuwa jimboni. Hali ni mbaya kweli kweli; watoto, wagonjwa, wazee wamekaa pale zaidi ya siku nne kwa sababu ya barabara.

Mheshimiwa Spika, *TANROAD* Mkoa wamejitahidi kurekebisha eneo moja, hilo ni eneo moja tu. Barabara hii imekatika maeneo manne tofauti, hivi tunavyoendelea huku ni bahari, huku ni bahari. Kwa mvua zinazoendelea barabara ile yote inaenda kuteketea mwaka huu. Ukiangalia barabara ya Mpanda imekatika, magari yamekuwa yakitumia kutoka

Tabora kwenda Kaliua na kwenda Mpanda, leo haipitiki, Kaliua kwenda Tabora haipitiki, Watanzania watateseka sana.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali, nilikuwa naangalia pia kwenye kitabu, ukiangalia fedha iliyotengwa kwa fedha za ndani kwenye barabara kuu kwa Mkoa wa Tabora ni barabara mbili tu na mojawapo ni Kaliua kwenda Puge na fedha iliyotengwa ni milioni saba, inafanya nini kwa uharibifu ule?

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aangalie, kwa Kaliua kwa kweli inahitaji *special priority* mwaka huu, vinginevyo tutakuwa ni kisiwa. Barabara zote hazipitiki za ndani hazipitiki, barabara kuu hazipitiki, wananchi wale wako katika hali mbaya sana sana.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la kampuni hizi za ujenzi. Tumekuwa tunashuhudia kampuni za ujenzi zinapewa *tender* zinakwenda kuchukua *material* kwa ajili ya kujenga kwenye vijiji huko changarawe, mawe, mchanga lakini bahati mbaya sana wanapokabidhi kazi baada ya ujenzi hawatengenezi zile barabara wanaziacha zikiwa katika hali mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, mfano mkubwa ni wa Kaliua, Kampuni ya *Chico* ilipewa mradi kutengeneza barabara ya Kazilambwa kuja Kaliua Mjini, wamekwenda kuchukua kokoto kutoka Igwisi; kwanza wamemaliza, tumepiga kelele sana kwenye halmashauri na hata hapa Bungeni, kwamba watengeneze barabara ya Igwisi kuja Kaliua, lakini wamemaliza kazi, wamekabidhi kazi barabara ile sasa hivi ni mashimo ni mahandaki, hakuingiliki na wameshaondoka tayari.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali bado Chiko wamepewa kazi nyingine Mkoa wa Tabora, waelekezwe wakatengeneze barabara ya Igwisi kuja Kaliua, ni barabara ya uchumi lakini kwa hali ambayo imeachwa ni hali ambayo ni mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia *TARURA* wanapewa fedha ndogo, hazitoshi kutengeneza zile barabara ambazo zimeharibiwa na *Chico* lakini wameondoka wameachia madhara makubwa pale. Pia hata fedha ya wananchi wa Igwisi ambapo walichukua kokoto na mchanga pia hawakuwapa stahili zao kama walivyokubaliana kwenye mikataba yao.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itoe agizo, kampuni zote zinavyopewa *tender* kabla ya kukabidhi kazi na kupewa *certificate* ya mwisho wahakikishe kwamba wanatengeneza barabara na kufukia mashimo ili waweze kuacha mazingira yale yakiwa katika hali nzuri.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu uharibifu wa miundombinu barabani. Tumekuwa tunashuhudia barabara zetu zinatengenezwa kwa gharama kubwa sana lakini kiukweli zinaharibika sana sana na zipo taarifa za uhakika kwamba miundombinu yetu ya barabara inahujumiwa kwa namna ya kutumia kwamba ni screpa. Zipo taarifa kwamba vifaa vingi ambavyo vinaingia barabarani vinapelekwa kwenye *scraper*.

Mheshimiwa Spika, hebu Serikali tuangalie tunawezaje kuruhusu *scraper* mpaka zinapelekwa kwenye viwanda? Viwanda tunavijua, vinatengeneza chuma katika maeneo mbalimbali lakini vinatumika vifaa vya ujenzi barabarani, zinatumika alama za barabarani, ni miundombinu ya barabani. Leo haiwezekani kuendelea kutengeneza gharama kubwa hivi wakati inahujumiwa na tunajua.

Mheshimiwa Spika, ninazo taarifa kwamba nyingine zimefikia Serikalini lakini hazipatiwi taarifa, nitakuja kuongea na Waziri nimpatie takwimu ni namna gani ambavyo barabara zinahujumiwa na baadhi ya watu wanafahamika, lakini hatua hazichukuliwi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu reli. Niipongeze Serikali kwa hatua ambayo imefikia ya

kutengeneza reli kwa *standard gauge* kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro pia Morogoro mpaka Dodoma na nina imani kwamba itatoka Dodoma itakwenda Kaliua na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyoongea bado mabehewa ni machache sana. Pamoja na kuwa kweli reli hii ni reli ya uchumi, reli hii, kama tunavyosema hatuwezi kuacha barabara kuharibiwa kama hatutengenezi reli zikawa imara. Pia reli inaweza ikawa nzuri ikawa inapitika lakini bado ikawa na mabehewa machache, Kaliua mabehewa ni machache sana na nimeongea na Waziri na yeye amefika jimboni ameona, wananchi wengi wanashindwa kutumia reli kwa sababu ya uchache wa mabehewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikali, Waziri aliagiza kwamba ataongeza bajeti kwa ajili ya kununua mabehewa, nilikuwa nategemea niione huku bajeti tuongeze mabehewa ili usafiri huu wa reli uweze kunufaisha wananchi wa Kaliua, Mpanda na maeneo mengine. Kwa sababu sasa hivi wanahesabiwa watu 15 mpaka 20 wakati wengi wao wangependa kusafiri na reli lakini wanashindwa wanatumia barabara ambapo pia hazina uhakika sana.

Mheshimiwa Spika, lingine, ni pale wasafiri watakapotaka kusafiri reli imepata matatizo, wananchi wanashindwa kupewa taarifa kwa muda. Hivi wiki iliyopita wako wasafiri wamekaa Kaliua siku tatu mpaka wakaandamana kwenda kwa Mkuu wa Wilaya, kwenda kwa Mbunge kwa sababu wana njaa wameishiwa, hawaambiwi taarifa zozote ikawa ni matatizo.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali, kwa kuwa kuna *communication* nzuri pale inapotokea tatizo kwamba miundombinu ya barabara labda reli imekatika mahali waelezwe, tusisubiri waandamane waanze kulia na watu wanakuwa wameshateseka sana na wanaumwa na mbu. Tuwape taarifa kwamba reli itakuwa tayari siku fulani *prior*, kabla ya kuteseka na tuhakikishe kwamba wasafiri wetu wanaweza kusafiri kwa muda. Pia tuharakishe lile tatizo

ambalo limetokea ili wasiendelee kuteseka. Kwa kweli ukifika pale Kaliua wakati ambapo reli imeharibika utaona uchungu, watoto wamelala chini, wagonjwa wamelala chini ni mateso ya hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu mawasiliano ya simu. Kwanza nashukuru kwamba kiukweli, hata mimi mwenyewe na wananchi wengi hawajui kwamba kuna mpango wa fursa za mawasiliano kwa wote ambao unajenga minara nchini.

Mheshimiwa Spika, sisi tulifikiri kwamba minara mingi inajengwa na kampuni za simu, lakini kumbe tuna mpango mzuri wa mawasiliano kwa wote ambapo unajenga minara. Kwa hiyo, kwanza naomba, kwa kuwa sisi kama Taifa tuna mpango wa mawasiliano kwa wote, tunaomba wahakikishe kwamba maeneo ambayo kampuni hazifiki wanafika waweke mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyoongea Wilaya ya Kaliua kuna maeneo mengi sana hakuna mawasiliano ya simu mpaka upande juu ya mti, juu ya paa ndipo upate mawasiliano. Maeneo ya Igwisi, Mloka, Usenye, Usinge na maeneo mengine, nikihesabu hapa vijiji zaidi ya 20 hakuna mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Wizara hii ijue kwamba mawasiliano sasa hivi ni uchumi, kama hakuna mawasiliano hakuna uchumi; huwezi kufanya biashara kama hakuna mawasiliano. Kwa hiyo tunaiomba Serikali ihakikishe kwamba inapeleka mawasiliano maeneo yote ya Kaliua ambayo hayana mawasiliano ili wananchi waweze kupata mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mawasiliano ya redio; yapo maeneo ambapo hakuna radio kabisa. Tunaomba Serikali ihakikishe kwamba mawasiliano ya redio yanakuwepo, kwa sababu dunia ya leo kama hakuna mawasiliano ya simu wala redio ni kwamba unakuwa kisiwani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu magari kujaza kupita uwezo. Tumekuwa tunalalamika, ukiona barabara zetu zilivyokuwa na mabonde; ni hatari kubwa, lakini ninachoshangaa ni kwamba tunayo mizani, sasa inafanya nini? Kwa nini tunaruhusu magari kujaza kupita uwezo licha ya kwamba pia barabara zinaharibika kwa haraka pia zinasababisha ajali?

Mheshimiwa Spika,Leo ukiwa unaendesha kutoka Morogoro kuja Dodoma unakutana na milima ndani ya barabara ingawa tunayo mizani. Naiomba Serikali tuhakikishe magari yanatii sheria...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Sakaya tayari muda wako.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana sana kwa mchango wako. Tunahamia CHADEMA sasa, Mheshimiwa Halima Mdee dakika 10.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwanza nataka Mheshimiwa Waziri anisaidie kupata majibu kuhusiana na barabara za Jimbo la Kawe ambazo ni barabara za kupunguza foleni ya Makongo, Chuo Cha Ardhi, Makongo Juu kwenda Goba. Nimesoma kitabu cha hotuba hapa kinaonesha kwamba, kilometa nne zimekamilika. Sasa kilometa nne zilizokamilika ni kutoka Goba na kilometa moja imeingia Makongo.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka nifahamu, kwa sababu zoezi sasa hivi ni kama limesimama na haijulikani kama kuna fedha ya fidia kwa sababu hapa fidia sijaona; na *corridor* ya barabara ina changamoto kidogo. Sasa nataka nipate majibu kwa mustakabali wa barabara ya Makongo.

Mheshimiwa Spika, pili, nataka vile vile anisaidie majibu ya barabara ya Wazo-Tegeta Kibaoni-Wazo-Madale, kuungana na Goba; kuna ujenzi unaendelea sasa hivi, lakini nikiangalia hiki kitabu kinazungumzia kilometa tano zinazojengwa sasa hivi, hakizungumzii kilometa sita ambazo zitaunganisha Madale kwenda Wazo. Kwa hiyo, naomba anipe hayo majibu kwa sababu hii barabara ni *very strategic.*

Mheshimiwa Spika, la tatu lakini sio kwa umuhimu; tunafahamu kwamba kuna upanuzi wa barabara ambao unatakiwa ufanyike kati ya Tegeta kwenda Bagamoyo. Sasa pale ni kati ya maeneo ambayo yanakumbwa na mafuriko miaka yote. Tutakumbuka katika utawala wa Awamu ya Nne viongozi wote walikwenda pale, mpaka aliyekuwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Pinda na tukakubaliana kuna mfereji wa chini utakaojengwa, ili kuondoa yale mafuriko na kumwaga maji Mto Nyakasangu.

Mheshimiwa Spika, sasa mfereji ulichorwa na watu wa *TANROADS* Mkoa wa Dar-es-Salaam, lakini mpaka sasa hivi hakuna hatua zozote ambazo zinafanyika. Sasa nataka tu nifahamu kwa sababu wananchi wanaumia sana kipindi hiki cha mafuriko, kwamba ule mpango wa ujenzi wa mfereji upo? Ama kwa sababu kuna mpango wa kuipanua hii barabara kutoka Tegeta kwenda Bagamoyo basi ndio utajumuishwa katika huo mradi wa upanuzi wa barabara?

Mheshimiwa Spika, baada ya kumaliza hayo ya ufupi ya jimboni kwangu, naomba nije kwenye suala la kitaifa la *ATCL.* Nikiangalia randama ukurasa wa 11 tunaambiwa kwamba kwa mwaka huu wa fedha Serikali inatarajia kufanya ununuzi wa ndege mpya kwa ajili ya Kampuni ya Ndege ya Tanzania *(ATCL),* shilingi bilioni mia nne tisini na tano. Tunakumbuka vile vile mwaka jana Serikali kupitia Waziri wa Fedha ilitenga vile vile bilioni zisizopungua mia tano kwa ajili ya ununuzi wa ndege.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu ieleweka hapa na Wabunge waelewe, kwamba hoja hapa si kupinga ununuzi wa ndege. Hoja hapa ni hizi fedha ambazo tunaziwekeza

ambazo ni matrilioni ya shilingi zinaenda kuzalisha ama tunaenda kuzitupa chini na zinapotea kama fedha nyingine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina taarifa ya Msajili wa Hazina hapa. Msajili wa Hazina ndiye amepewa dhamana ya kusimamia mashirika yote ya Tanzania, anasema hivi, ukurasa wa nne wa taarifa yake:-

*"Imekuwa vigumu kwa ofisi yangu kuweza kufanya uchambuzi wa kina wa utendaji wa ATCL kutokana na kutokuwepo taarifa za kutosha za kampuni. Kwa mfano, mahesabu ya kampuni yaliyokamilika ni ya mwaka 2014/2015 tu yaliyofanywa na PWC. Hata hivyo mahesabu hayo hayajatizamwa wala kupitishwa na Bodi. Hali hii imesababisha Ofisi ya Msajili wa Hazina kutoweza kuchambua na kubainisha hali halisi ya uwekezaji ilivyo hadi sasa kuhusu madeni na mali za kampuni,"*

Mheshimiwa Spika, vile vile wanasema wanashindwa kujua hali ya ukwasi wa kampuni kwa sababu ya kampuni kutokuwa na mahesabu kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukija kwenye taarifa yenyewe ya *ATCL* wanasena kwamba, shirika halikuwa na mpango wa biashara. Yaani tunawekeza bilioni mia tano 2016/2017, 2017/2018 tukawekeza bilioni mia tano, 2018/2019 tunataka tuwekeze bilioni mia nne tisini na tano halafu hatuna mpango wa biashara. Hivi unaenda kuanzaje kufanya biashara wakati huna mpango? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna *business plan,* tunawekeza *trillion shillings.* Tunakuja hapa wanasema inabidi tuanze kuajiri *management* yenye uwezo kwa sababu sasa hivi shirika halina wataalam wenye uzoefu wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge lako mwezi Januari, walitoa taarifa za Kamati, kwa niaba ya Bunge wameita wataalam wa Serikali wanaosimamia mashirika yetu. Wamesema kwamba shirika letu mpaka sasa lina hali dhoofu na lina

madeni ya shilingi bilioni mia tano kumi na saba. Sasa shirika lina madeni, shirika halina mpango wa biashara, shirika halina wataalam, tunaweka trilioni mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliombe hili Bunge tutekeleze wajibu wetu. Hivi inaingia akili timamu, kwamba kwenye kilimo ambacho mkinaajiri asilimia zaidi ya 75 ya Watanzania tumeweza kuweka bilioni 11 tu, kwenye ndege ambayo tuna uhakika kwamba hii pesa tunaenda kuimwaga chini, tuna uhakika, tumeweka trilioni moja.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri akija hapa atujibu. Ni muhimu akajua wasije wakafikiria watakuwa salama, hizi pesa wanakumbuka akina Mramba, mnakumbuka akina Yona, hizi pesa tukigundua wameziwekeza kinyume na utaratibu, kama ambavyo nyaraka zinaonesha, tutawachukulia hatua.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu Mheshimiwa Rais akajua pia, hiyo kinga aliyonayo ya Kikatiba inaangalia kama kuna masuala yalifanywa kwa makusudi kwa kuona kwamba kuna hasara mbele tukajiingiza kichwa-kichwa, huo usalama ama hiyo kinga ya Katiba haipo, tutamshughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haiwezekani. Naongea kwa dhamira ya dhati na najua Wabunge wengi wanajua, wengi wakiwa huko nje wanalialia, tukija huku ndani...

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima, kuna taarifa, kuhusu utaratibu eeh? Mheshimiwa Stella Manyanya, tafadhali.

**KUHUSU UTARATIBU**

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe mzungumzaji utaratibu...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** ...tafadhalini, nazungumza na Spika. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa 64(1), sasa unaanza kuzungumza kabla sijazungumza?

Mheshimiwa Spika, nasema Kuhusu Utaratibu ni huu Mheshimiwa; Utaratibu ninaotaka kumpa Mheshimiwa mzungumzaji ni huu, ni kwamba, kwanza achukulie kwamba, Mheshimiwa Rais wa Nchi ni kiongozi anayeheshimika na watu wote, hasa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ni kwamba, mambo yote yanayofanywa kwa nia njema yanatakiwa kuungwa mkono na kusaidiwa. Ninachokiona kila wakati tangu mwanzo wa michango hii inavyoendelea, upande wa upinzani wenzetu badala ya kujielekeza kutoa mawazo mbadala wamekuwa ni wa kulalamika. Sasa kulalamika peke yake haitoshi.

Mheshimiwa Spika, nikuombe kwa sababu, *Hansard* zetu zinaonesha ni namna gani Waheshimiwa Wabunge wa Upinzani kwa siku za nyuma walikuwa wanachangia pia kuhusu suala la *ATC* na ukosefu wa ndege zetu, hebu tupate zile *Hansard* zote kabla ya mtu, maana inaonekana kwamba mtu anachangia leo kesho hakumbuki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya katka hii michango tunayoifanya kunakuwa hakuna mtu anayesahihisha leo umesema vizuri au umesema vibaya. Kwa sababu, tumeambiwa kazi ya Mbunge ni kusema, basi mtu anasema tu anasema tu hata kama jambo halina tija, hapana.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, tukienda kwenye ndege ninyi wenyewe mnakuwa wa kwanza kupanda, kwa nini mnakuwa hivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ninachosema ni kwamba taarifa ninayoisisitiza kumpa mzungumzaji ni kwamba, binafsi naunga mkono pale michango ambayo ni chanya inatolewa, lakini michango ambayo inalenga katika kukashifu na kusemasema ilimradi uonekane, basi wote sisi uwezo huo tunao.

**SPIKA:** Nilikuona Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Lukuvi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nataka nikuombe tu Kuhusu Utaratibu nimsaidie Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, kwamba, tunachokisema kuhusu Kanuni ya 64, inasema hivi, Mbunge yeyote akiwa anazungumza humu Bungeni:-

*"Hatatumia jina la Rais kwa dhihaka katika mjadala, au kwa madhumuni ya kutaka kulishawishi Bunge kuamua jambo lolote kwa namna fulani".*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge, jina la Rais kwanza halitakiwi kutumika namna hiyo, lakini pia, maneno aliyosema kwamba, watamshughulikia Rais kwa maoni yangu halina uhusiano na mjadala huu. Kwa hiyo, nataka kutoa tu Utaratibu huo ili angalau Mheshimiwa Mbunge aweze kuondoa maneno yake ili ajirekebishe kwenye mjadala, kwa sababu kwa kuendelea kutamka jina la Rais anavunja kanuni. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester anaelekezewa Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, Rais alichaguliwa na Watanzania. Hili Bunge ni la wawakilishi wa Watanzania. Rais lazima akosolewe na jina la Rais lazima litajwe kama anaenda kinyume na utaratibu. Lazima hii *perception* kwamba, Rais ni *untouchable,* lazima iishe. Bunge likiogopa kumtaja Rais wakati sisi tunapitisha bajeti, Rais ni

sehemu ya Bunge, tutakuwa tunalifanyia makosa makubwa sana aifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi sijatumia jina la Rais kwa kebehi, nimesema hivi, tuna taarifa mbili hapa; tuna taarifa ya Msajili wa Hazina, tuna Taarifa ya *ATCL.* Taarifa ya Msajili wa Hazina inasema, nataka...

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Aah, kaa chini bwana.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** We Dokta Shika vipi? *(Kicheko)*

**T A A R I F A**

**SPIKA:** Mheshimiwa Mollel, nimekuona, taarifa.

**MHE. DKT. GODWIN O. MLOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nilitaka kumpa taarifa mwenzangu hapa. Anachotaka kujielekeza ni kuonesha kwa namna gani inatakiwa kuwekezwa kwa namna nzuri ambayo italeta pato zuri katika Taifa, lakini yeye kama kiongozi wa chama kikuu cha upinzani kwenye chama chake asilimia 100 ya mapato hayaonekani, hiyo ni moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini leo kwenye chama hicho pasipokuwepo na ruzuku ya Serikali, pasipokuwepo na michango ya Wabunge, chama hakiendesheki, lakini kwa zaidi ya miaka mingi hawajaweka hata *investment* moja ya kumlipa *PS.* Kwa maana hiyo ni nini... *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tusikilizane.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: ...**kwa maana hiyo ni nini!...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Tulieni! Mnaniita Dokta Shika nimewashika vizuri na naendelea kushika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mollel, ngoja kwanza kidogo.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Na bado nitawashika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tusikilizane. Mheshimiwa Mollel hatujakusikia vizuri, hebu anza tena. *(Makofi/Vigelegele)*

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, kwanza nirekebishe tu, wananiita Dokta Shika, nitawashika na nitamshika Mheshimiwa Msigwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ninachosema, leo kwa miaka yote chama hiki hawana hata kibanda kimoja ambacho wanaweza hata wakapata kipato ili wamlipie *PS* na wamekuwa wakipata mabilioni. Kwa hiyo ninachosema hata kama una mawazo mazuri vizuri kiasi gani, niambie kwa uongozi wenu huu wote mmefanya nini kinachoweza kuletea uchumi CHADEMA ili muweze kupewa Serikali tuwaamini kwamba mnaweza mkaisaidia Serikali? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hilo jiwe sijui kama Mheshimiwa Halima ataweza kusimama; Mheshimiwa Halima nafasi yako. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, siwezi kumjibu Dokta Shika, bidhaa ya Kichina, hata mara moja. *(Makofi)*

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Nashukuru hujanipeleka kwa Makonda na bado nitarudi nyumbani naendelea na wewe nitakushika vizuri. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nimesema hivi, siwezi kumjibu Dokta Shika bidhaa ya Kichina, umenielewa; nikimjibu nitakuwa najidhalilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja yangu iko wazi kabisa. Nimesema hivi na naomba nirudie kwa sababu, najua kengele itagonga; nina nyaraka mbili za Serikali, nina nyaraka ya Msajili wa Hazina, nina nyaraka ya *ATCL* yenyewe; wanasema kwamba, mosi, tumewekeza...

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Aah' hii imekuwa hatari hii; Mheshimiwa Musukuma, sasa iwe Taarifa ya mwisho hii.

**T A A R I F A**

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mzungumzaji aliyekaa, Mheshimiwa Dkt. Mollel alikuwa anatoa taarifa sahihi kikanuni. Hata hivyo ninajaribu kusikiliza huku kuna lugha inatoka inasema Dkt. Shika; na Mheshimiwa Halima Mdee amesimama akasema hawezi kumjibu Dkt. Shika. Ukisoma Kanuni ya 64, tulitaka kupata uhakika, hili jina la Dkt. Shika linaingia kwenye dhihaka ya kumdhihaki Mbunge, kitu ambacho si sahihi kikanuni.

**MBUNGE FULANI:** Kwani ni wewe? Yeye mwenyewe kakubali.

**SPIKA:** Umebakiza dakika moja Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nasema hivi, mwaka jana tumewekeza bilioni...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Unasema usenge Bungeni? Kuhusu Utararibu, ametukana, afute kauli yake.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetukanwa, afute kauli yake Mheshimiwa.

**SPIKA:** Nani? Amefanya nini?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nimetukanwa tusi kubwa sana.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Lusinde katukana.

**SPIKA:** Tulieni, tulieni. Mheshimiwa Halima sijakuelewa, nini kimetokea?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetukanwa tusi zito na Mheshimiwa Lusinde. Sasa kama hatafuta na mimi nitafanya la kwangu. Kwa hiyo naomba...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, nimefuta. Nimefuta.

**SPIKA:** Mwenye *floor* ni Mheshimiwa Halima Mdee, muacheni aseme, bado ananieleza, sasa mnapiga kelele ya nini ikiwa anaeleza? Au hamtaki aseme basi?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema hivi...

**SPIKA:** *No,* lile ulilokuwa unalisema lile.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, ameshalifuta mwenyewe, nikilirudia nitaharibu *Hansard.* Yani ametukana halafu akafuta juu kwa juu.

**SPIKA:** Ameshafuta eeh?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, ameshafuta.

**SPIKA:** *Ok,* endelea basi. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasema hivi kwa dhamira njema...*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**SPIKA:** Ahsante sana, muda umekwisha Mheshimiwa Halima. Sasa Waheshimiwa Wabunge, mchangiaji atayefuatia hapa; tumemaliza *CUF*, CHADEMA tunaenda NCCR; atakuwa Mheshimiwa Mbatia na wengine watafuata. Baada ya muda mfupi nitamwachia Mheshimiwa Najma hapa kuendeleza gurudumu hili.

Niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba leo tunao ugeni mzito kwenye viwanja vyetu vya Bunge itakapofika saa saba, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli atatembelea hapa kwenye viwanja vya Bunge, atakuwa mgeni wa Bunge la Afrika Mashariki. Kwa hiyo kutakuwa na shughuli shughuli zitakazoendelea hapo nje na baadaye ataingia kwenye ukumbi wa Msekwa na kulihutubia Bunge hilo la Afrika Mashariki.

Sisi tutawakilishwa na Kamati ya Uongozi na Makamishna ambao wataingia kwenye ukumbi wa Msekwa, kuna mahali watakapokaa kutuwakilisha. Wabunge wengine wote tutaendelea na shughuli zetu kama kawaida, tusijae mle *unless* uwe umealikwa. Kwa hiyo napenda niwataarifu kuhusu jambo hilo, kwamba wale wanaopapasa papasa wale mwamba anaingia saa saba.

Basi baada ya hapo nimkaribishe Mheshimiwa Najma ili aendeleze gurudumu hili .

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu...

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo, sema mwongozo.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na uchangiaji, Mheshimiwa Mbatia.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wako tafadhali. Mwongozo wa kiti tafadhali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nassari naomba ukae chini. Mheshimiwa Mbatia tuendelee. *(Makofi)*

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa heshima kubwa kabisa hili ni Bunge na tukishatamka Bunge Tukufu linatakiwa lioneshe utukufu wake. Hii si sehemu ya matusi na ukisoma Zaburi 1:1 inasema

*"Heri watu wale wasiokwenda katika shauri la wasio haki, wala hawakusimama katika njia ya wakosaji, wala hawaketi barazani pa watu wenye mzaha."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi tukafanya Bunge hili ni sehemu ya mzaha wakati kuna *issues serious* za kitaifa za kuzungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ukishaitwa Mbunge halafu unaleta matusi ya nguoni ndani ya Bunge, si jambo la heri kabisa kwa yeyote yule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa heshima kubwa kabisa, sisi ni watu wazima, tuheshimiane, tusikilizane. Pia ukisoma Mithali 18:13 inasema:-

*"Kujibu kabla ya kusikiliza ni upumbavu na jambo la aibu"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujibu kabla ya kusikiliza ni upumbavu na jambo la aibu na hii ni Mithali 18:13. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite kwenye mchango wangu, baada ya kusema hayo, ni angalizo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wahandisi katika Taifa letu wanafanya kazi nzuri na niwapongeze sana na hasa Mhandisi au Meneja wa *TANROAD* wa Mkoa wa Kilimanjaro, tunashirikiana naye vizuri, anafanya kazi vizuri na tunamtia moyo na tutaendelea kufanya naye kazi vizuri. Hata hivyo, niwatahadharishe tu Wahandisi kwamba taaluma ya uhandisi duniani leo ni taaluma shirikishi. Huwezi ukajiita mimi ni *engineer* kwamba basi ile taaluma yako huwezi ukashirikisha wengine la hasha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na hilo kwa sababu ukiangalia adui mkubwa wa barabara leo hii ni maji; na mwaka jana nilisema tena namna gani Wizara hii inashirikiana na TAMISEMI na kutoa elimu ya kutosha namna ya uhifadhi mzuri wa barabara zetu na hasa kwenye suala la *drainage system.* Kwa sababu tunakubali Serikali haina fedha za kutosha kwa ajili ya *maintenance* ya barabara, sasa *Local Government* wanasafisha namna gani hii mitaro, kilimo cha matuta, mmomonyoko unavyotokea, maporomoko yanavyotokea barabara zetu zinaharibika kwa haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kilimanjaro uko kwenye mwinuko wa hali ya juu, hali ya barabara sio nzuri. Changamoto kwa wahandishi wetu, kwamba ni namna gani wanakuja na ubunifu mpya wa kupata *material* mpya ambayo inatumika kwenye hizi barabara badala ya kuweka kokoto zile zile au moram ya aina ile ile, lazima kuja na *material* nyingine labda moram mnachanganya na *lime* au *moram* mnachanganya na *material* mengine kwa ajili ya muda na uimara wa barabara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasahau kuna barabara moja tuliomba, barabara inayoenda Kilema Hospitali ambayo ni hospitali ya wilaya. Barabara hii inahudumia watu wengi, tunaomba ipewe nafasi. Milioni mia mbili ishirini iliyopewa barabara hii kusema ukweli na ina kilomita zaidi ya 13, hazitatosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni zungumze suala la ujumla la miradi hii hasa sekta ya ujenzi. Nikizungumzia miradi ya Mkoa wa Dar es Salaam kwa mfano na Dodoma nayo imeshaambukizwa na majiji mengine. Ukiangalia *Master Plan* ya Mkoa wa Dar es Salaam, ukizungumzia magari yaendayo mwendo kasi, *Dar es Salaam Rapid Transport* (BRT). Mradi ule wa Reli wa Dar es Salaam, *flyovers,* suala la usafiri wa majini kutoka Dar es Salaam kwenda Bagamoyo, boti ya Bagamoyo sijui imeishia wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la barabara za kutoka Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro ambapo watu wamevunjiwa nyumba zao. Benki ya Dunia imesitisha, hakuna fidia na maumivu ni makubwa. Mambo hayo ya kujenga mambo ya namna hii si mema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la upanuzi wa *Julius Kambarage Nyerere International Airport, ring roads* za kutawanya *traffic* katika Jiji la Dar es Salaam na miradi mingine mingi. Hainiingii akilini nikizungumza masuala ya majanga leo hii; mafuriko Dar es Salaam ni majanga makubwa lakini juzi tumeshuhudia pale Jangwani wanakoegesha au *depot* ya *Dar es Salaam Rapid Transport.* Serikali inawezaje ikasema watu watoke mabondeni na wao wakaenda wakawekeza pale? *Future Plan* iko wapi, UDA waliweza kujenga Ubungo walijenga Kurasini UDA wakati wa Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamata walijenga kule barabara ya Nyerere lakini leo hii *depot* ya Jangwani mafuriko yaliyotokea juzi mradi huu mkubwa uliowekezwa pale, nguvu iliyowekezwa pale, *investment* iliyowekezwa pale, nani

anawajibika kwa kushauri ujinga huo wa *depot* ya *Dar es Salaam Rapid Transport*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kwa pamoja kwa sababu zaidi ya asilimia 96 ya majanga ya dunia hii yanasababishwa na binadamu. Najua Wahandisi wengine wanafanya kazi vizuri tu; lakini wanasiasa wanaingilia Wahandisi, matamko ya kisiasa; huku wamenipa kura wasibomolewe na huku hawajanipa kura wabomolewe. Sasa mambo ya namna hii, Tanzania ni yetu sote, hatuwezi kuangamia kwa ajili ya kukosa maarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia miradi hii ukisema ni ipi ya *PPP*, ukiangalia ni miradi ipi ya *BOT* ni *investor* gani ambaye ni makini *serious investor* atawekeza Dar es Salaam, huku kuna reli inayojengwa kwa *standard gauge* sawa tunaunga mkono itoke Dar es Salaam na isafirishe abiria kwa kasi kuleta Morogoro. Dar es Salaam Chalinze mradi huo, magari yaendayo kwa kasi, je, wanakaa pamoja na kuratibu miradi hii yote kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Dodoma imeanza tena, ukifika St. Gasper *traffic* imeanza, asubuhi na jioni, mvua ikinyesha Dodoma mafuriko yameanza *area* D na maeneo mengine. Sasa *future plan* yetu tuna *design* namna gani? Hii miradi *return period* yake tunaifanya kwa kiasi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya ni majanga na ni majanga makubwa kweli kweli. Kwa mfano, ukisoma ile taarifa ya *CAG* na hili ni janga la kitaifa, ni janga pia la 1.5 *trillion.* Ukichukua majimbo yote ya uchaguzi Tanzania yako 264 ukigawanya kwa kila kilomita moja ya lami ya shilingi milioni mia saba kila jimbo la uchaguzi lingepata zaidi ya kilomita 8.12 za lami nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya ni vema tukayasimamia vizuri kwa sababu kashfa juu ya kashfa hakuna mwendelezo hakuna *sustainability*. Sasa *sustainability* haitakuwepo tukitoka kwenye ule mradi wa kutoka Dar es

Salaam Bagamoyo *Boat* kashfa, sasa hivi kashfa nyingine *ATCL,* nayo tumeona matatizo yakijitokeza sasa hivi, kashfa juu ya kashfa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niseme tu, maandiko matakatifu yanasema watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa. Haya tunayoyasema; *Isack Newton* anasema katika kila kani mkabala kuna kani mrejeo sawa na kinyume na anasema vile kwa sababu lazima kukubali mawazo mbadala tushirikiane vizuri, tufanye kazi vizuri, kwa kuwa Tanzania ni yetu sote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tusipokuwa makini tukafuta Katiba, tukafuata sheria, tukafuata taratibu, Bunge likajua nafasi yake, *a democratic principle* inayosema *no taxation without representation.* Ndiyo maana Wabunge tuko hapa kwa ajili ya kuisimamia na kuishauri Serikali, kuangalia kodi za Watanzania zinatumika vizuri la sivyo Bunge hili litakuja kuhukumiwa kwa nini haya yanatokea kwa kiasi hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri, ukiangalia ule Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere, *lift* pale tu ni tatizo *lift*. Wagonjwa wanatoka na ndege huko wananyanyuliwa na viti kana kwamba wananyanyuliwa kwenye machela wanawabeba mzoba mzoba. Watu wa nje wanatuonaje. Hilo lilinikumba mimi mwenyewe mwaka juzi tarehe 2 Disemba, mwaka juzi. Juzi tarehe 30 Ijumaa Kuu uwanja ule *lift* zilikuwa hazifanyi kazi. Yaani tunaonekana ni watu wa ajabu *lift* tu Uwanja wa Ndege wa Kimataifa hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lazima tu-*think* dunia wanatuonaje. Waziri *with due respect,* kazi yote mnayoifanya ni kazi kubwa, miaka miwili mmepewa zaidi ya trilioni tisa katika miundombinu ya nchi hii, lakini ni namna gani tunaipa kipaumbele miradi yetu ya sekta ya ujenzi, mawasiliano na uchukuzi. Kupanga ni kuchagua, sasa sisi tunapanga vipi? Kama tunasema sungura ni mdogo, basi twende kwenye *idea* ya *concept* mpaka *formalization*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana Serikali kwamba lazima tukubali taaluma za watu lazima ziheshimike. Pia naomba Wahandisi wasikate tamaa, waendelee kushauri vizuri na sisi wanasiasa tupate takwimu kutoka kwao ili tuweze tukazungumza na kuwasimamia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbatia. Tunaendelea na Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza dakika tano na Mheshimiwa Joseph Mkundi ajiandae.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kidogo tu katika hizi dakika tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nianze moja kwa moja na usafiri katika Ziwa Victoria. Meli yetu ya *MV* Victoria iliharibika miaka mitano iliyopita na Serikali imekuwa ikiahidi kutengeneza meli hiyo. Ukitazama hata katika makadirio ya mwaka jana Serikali ilisema katika makisio kwamba ingetoa bilioni hamsini ili kuweza kununua meli mpya lakini pia kufanya matengenezo kwa meli hiyo ya *MV* Victoria. Pia mwaka huu wametoa bilioni tisa kwenda kutengeneza meli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimuulize tu Mheshimiwa Waziri, hii meli ya *MV* Victoria ambayo inatengenezwa katika miaka mitano inatengenezwa kitu gani? Kwa sababu inashangaza kwamba meli ambayo inahitajika; kwa sababu sisi watu wa Mkoa wa Kagera ili uweze kusafiri kibiashara na hasa akinamama ambao wanasafirisha ndizi, *Avocado* na bidhaa nyingine za maharage, wanatumia njia ya barabara, kitu ambacho kwa kweli kinawa-*cost* na gharama za kuendesha biashara hiyo inakuwa kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba majibu, tunaomba Waziri atuambie, ni lini atatutengenezea hiyo meli wakati tunasubiri meli ile ambayo wamesema kwamba

itajengwa? Kujenga meli mpya kunachukua muda mrefu lakini matengenezo ya *MV* Victoria ni kwa nini yamechukua muda mrefu na kila mwaka wamekuwa wanatenga fedha kwa ajili ya meli hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia kitabu cha hotuba cha Mheshimiwa Waziri cha mwaka jana hiki, ukurasa wa 81, alichokisema na hata mwaka huu ameongea lakini hakuna kitu chochote. Hata Watanzania wa Mkoa wa Kagera hawapewi taarifa ni kitu gani kinaendelea kuhusu meli yao ambayo ilikuwa inarahisisha usafiri kutoka Bukoba kwenda Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongelea hiyo nije kwenye *TARURA.* Japokuwa hii *TARURA* ipo chini ya TAMISEMI, lakini fedha zake zinatolewa na Serikali Kuu kutoka kwenye Mfuko wa Barabara. Kwa muda mrefu tumekuwa tukiiomba Serikali, kwamba huu mgawanyo wa asilimia 30 ni mdogo na Halmashauri walikuwa wanashindwa kutengeneza barabara nzuri na zilizo imara. Sasa pesa hiyo hiyo asilimia 30 ndiyo inapelekwa kwa *TARURA* na huu ni Wakala ambao umeundwa au umeanzishwa ili kuweza kusaidia barabara za vijijini zilizo chini ya halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Wizara haifikirii namna ya kuongeza pesa kutoka angalau asilimia 30 kwenda asilimia 40 ili *TARURA* waweze kujenga na kutengeneza barabara; na tukijua kwamba wana mtandao mkubwa wa barabara zilizo halmashauri na kuna maeneo mapya ya utawala ambayo yamekuwepo; tunaomba Serikali ifikirie namna ya kuongeza pesa kwa *TARURA* au mtindo utakuwa ni ule ule na *TARURA* watashindwa kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije sasa kwenye Bodi ya Usajili wa Wahandisi. Wamesema katika kitabu na hata cha mwaka jana wamesema kwamba wanataka hii Bodi ya Usajili wa Wahandisi iweze kusimamia kazi zote zinazofanywa za kihandisi, wahandisi watokane na umoja huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingi zinazojengwa zinakuwa chini ya viwango; naomba nitoe mfano, barabara ya Biharamulo ambayo imetoka Rusaunga inakwenda mpaka Kasindaga. Ukienda kwenye barabara hiyo pale kwenye *keep left* ya Biharamulo barabara imebomoka kabisa. Kilomita mbili kabla hujafika Kasindaga barabara imekwisha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukiitazama baada ya lami kubanduka pale utaona kwamba ile barabara imetengenezwa chini ya kiwango. Kwa hiyo, naomba Wahandisi ambao tunawasifu kwamba wanafanya kazi wafanye kazi kulingana na taaluma zao. Kama Wahandisi hawawezi kusimamia miradi hii, basi hii miradi itajengwa chini ya kiwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kusisitiza kuhusu usafiri wa Ziwa Victoria, watuletee meli yetu. Nisiseme, labda niseme wana ajenda gani na watu wa Kagera pale ambapo wanatunyima meli, tunakosa usafiri. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Rwamlaza. Tunaendelea na Joseph Mkundi dakika tano halafu Mheshimiwa Dkt. Kikwembe ajiandae.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa dakika tano hizi nitajikita kwenye maeneo mawili. Kwanza kabisa nipende kupata kauli ya Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Waziri, ni suala ambalo tumekuwa tukilishughulikia mara kwa mara. Tuna kivuko kinachounganisha Kisiwa cha Ukerewe na Kisiwa cha Ukala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kivuko hiki kinahudumia zaidi ya wananchi 50,000, kimekuwa kinaleta shida mara kwa mara na nimekuwa nawasiliana na Wizara. Sipendi siku moja

tuje hapa kuomba rambirambi kwa sababu ya wananchi waliozama katika kivuko kile. Naomba nipate kauli ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mwaka jana tumeahidiwa kwamba mpaka mwezi Desemba mashine mbili zilizokuwa zimeagizwa zingefungwa kwenye kivuko kile lakini mpaka sasa hakuna kinachoendelea. Niombe kauli ya Serikali mashine kwa ajili ya kivuko cha *MV* Nyerere kinachofanya kazi kati ya Bugolola na Ukala zinafungwa lini na kivuko hiki kiweze kuwa katika utendaji kazi mzuri na ulio salama kwa wakazi wa eneo lile?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine katika maeneo hayo hayo ya vivuko tuna Kisiwa cha Ilugwa. Wananchi wanasafiri zaidi ya masaa manne kuja Ukerewe. Wana-*risk* sana, wanasafiri kwa kutumia mitumbwi. Serikali ina mkakati gani kutupatia kivuko kwa ajili ya eneo lile?

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka nichangie ni juu ya Kampuni ya Huduma za Meli. Kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 75, anaongelea juu ya kampuni hii. Mwaka 1999 kampuni hii ilibinafsishwa, lakini baada ya kubinafsishwa na kukosa watu wa kuichukua iliendelea kufanya kazi. Bahati mbaya sana kwamba vile vifaa na mashine kwa ajili ya matengenezo vilibinafsishwa lakini wale watumishi waliobaki kwenye kampuni hii walijikongoja wakaendelea kufanya kazi pamoja na kwamba kulikuwa na matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni nini, watumishi hawa waliobaki wakiwa wanafanya kazi kwenye kampuni hii wana miezi 23 sasa hawajalipwa mishahara. Hebu tuweze kutafakari kama ni sisi hawa watumishi wanaweza kuishi vipi? Inawezekana kweli kuna watu wamefanya vibaya kwenye kampuni ile, lakini basi Serikali iweze kufanya uchambuzi; ina vyombo vyake; ijue ni watu gani hawajafanya vizuri, watu gani wamehujumu kampuni ile na wasio na makosa waendelee na kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kukaa na watumishi miezi 23 hawajalipwa mishahara halafu tutegemee waendeshe kampuni hii wakiwa na tija na ufanisi, si kweli. Wakati wanasikia kwamba kuna trilioni moja sijui *point* tano imepotea halafu wao miezi 23 hawajalipwa mishahara hawawezi kuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni muhimu sana Serikali iangalie namna gani ya kufanya watumishi hawa wapate haki yao ili waweze kufanya kazi katika mazingira yaliyo salama. Ni jambo jema kwamba sasa tuna Mtendaji Mkuu, Mkurugenzi ambaye wamemteua mwaka jana, ni mtu makini, mchapakazi, mbunifu, basi Serikali impe *support*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya kumteua kumpa kampuni ile ambayo ilikuwa inaelekea kufa halafu wakam-*dump* wakamtelekeza pale hawatakuwa wamemsaidia, wampe nguvu, wamtie moyo, wampe msaada wa karibu ili aweze kusaidia kwenye kampuni hii ili iweze kufanya kazi kwa sababu ni kampuni muhimu sana kwa usafiri unaounganisha Ukerewe, Mwanza lakini na maeneo mengine; Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, basi Serikali ifanye kile ambacho inapaswa kufanya wafanyakazi hawa waweze kulipwa mshahara wao waweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunaendelea na Mheshimiwa Kikwembe, baadaye Dokta Kafumu ajiandae.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante ila hujaniambia dakika ila najua nitachangia dakika 10.

**MWENYEKITI:** Dakika tano, tano kila mmoja.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba dakika 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda niishukuru Serikali yangu pamoja na Wizara kwa ujumla kwa namna ya pekee ambavyo wamekuwa wakifanya kazi kwa bidii na kuhakikisha kwamba wanachanganua changamoto ambazo zinatupelekea kupata maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri na Serikali katika kutupatia pesa ya maendeleo ya barabara; milioni karibu mia tisa katika Mkoa wa Katavi, lakini bado ni chache. Naomba wafikirie namna ya kuongeza kutokana na namna ambavyo barabara zimeharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi katika jimbo langu; napenda kuongelea Daraja la Kavuu. Daraja la Kavuu lilikwisha, lakini pamoja na kwamba ni la muda naomba sasa barabara ya Majimoto-Inyonga ambayo wamenitengea karibu milioni mia moja sabini, sidhani kama zitatosha kutengeneza zile kilomita mia mbili na kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sasa ili daraja lile liweze kupitika niombe Mheshimiwa Waziri wanisimamie na waniongezee pesa katika barabara hii ya Majimoto-Inyonga ili tuweze kutumia lile daraja na tuweze kuwarahisishia wananchi kutoka katika Jimbo la Kavuu kufika Inyonga na hatimaye kuweza kufika Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwashukuru wameweza kunipatia hela ya matengenezo ya barabara ya Mamba-Kasansa ambayo ni karibu milioni tisini. Pia niwashukuru kwa kunipatia pesa kwa ajili Kibaoni-Majimoto-Kasansa ambayo ni milioni takriban mia moja hamsini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri asinichoke ninapokwenda kuendelea kuomba kuhusu maendeleo ya Jimbo langu la Kavuu kwa sababu mvua ni nyingi na hivi ninavyoongea bado zinaendelea kunyesha na barabara na madaraja mengi na makalavati mengi yameharibika. Kwa hiyo, naomba washirikiane na *TARURA* kwa karibu na najua pesa yao ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na Wabunge wengine, kama vile tunavyosema tuwaongezee pesa angalau sasa ifike asilimia 50 kwa sababu wamekuwa wakifanya kazi nyingi bila uwezo wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee daraja langu ya Mwamapuli-Chamalendi ambalo *TARURA* wameweza kunipa pesa ya dharura na sasa hivi linapitika na wananchi wangu wanaweza kupita kwenda kwenye matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sasa yale maombi yangu ya dharura niliyoleta *TANROAD* ambayo nataka kujenga daraja la kudumu basi wayafikirie ili tuweze kurahisisha wananchi wa Kata kuanzia ya Majimoto, Mbede, Chamalendi, Mwamapuli, Ikuba, wote waweze kufika katika hospitali ama Kituo cha Afya cha Usevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kuongelea suala la Mradi wa Kokoto wa Kongoro. Mradi huu kwa kweli kama tutausimamia vizuri tunaweza tukaingiza pesa za kutosha. Inawezekana tatizo ni makubaliano kati ya *TAZARA* upande wa Zambia na upande wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri aunde tume basi ambayo itaweza kusimamia na kuangalia mkataba huo ili huu mradi uweze kujiendesha kibiashara na Watanzania wengi waweze kufaidika katika mradi huo ili tuweze kuona ni namna gani wanaweza wakachangia maendeleo katika nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niongelee Gati la Karema. Gati la Karema limeshafanyiwa upembuzi yakinifu, lakini katika bajeti iliyopita walituambia kwamba Karema hakutajengwa tena gati patajengwa bandari. Sasa tulikuwa tunaomba tupate ufafanuzi ni gati litakalojengwa ama ni bandari ili wananchi waweze kuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba wameshafanya upembuzi yakinifu tunataka tujue maendeleo

ya Bandari hiyo ya Karema ikoje, kwa sababu ndio kiungo kinachotusaidia sisi kutoka Kavuu kuja Mpanda Mjini mpaka Karema kuvuka mpaka Congo ambako tunaweza kupeleka mazao kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niongelee kuhusu Kiwanja cha Ndege cha Mpanda. Kiwanja cha Ndege cha Mpanda ni kizuri na kimekwisha. Naomba ule upungufu uliobaki, Mheshimiwa Waziri mwaka jana nimemweleza na naomba tena na narudia, ili kiweze kufanya kazi tuweze kupata na sisi watalii wanaoweza kuja katika Mbuga ya Katavi ili tuweze kuongeza uchumi, kwa sababu Mbuga ile ya Katavi ina wanyama ambao ni *unique*. Tuna Twiga ambao ni machotara ambao hawapatikani kokote, ni warefu kuliko kama wengine, ni wanyama walioshiba. Tuki-*promote* na sisi mbuga yetu upande wa kule angalau tunaweza tukaongeza kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudi pia katika suala la mawasiliano, kwa ndugu yangu Mzee Kamwele Ilunde, bado mawasiliano ni shida katika Kata ya Inyonga-Ilunde. Niwaombe basi tuweze kuwasaidia ndugu zetu wa Ilunde ili waweze kupata mawasiliano hatimaye waweze kuongeza vipato vyao kwa sababu wako karibu na Tabora na wako karibu na Kavuu, kwa hiyo inaweza kuturahisishia sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watakapokuwa na mawasiliano mazuri wanaweza wakafika mpaka Mbeya na wakarudi wakaingia mpaka Tunduma, Zambia kuweza kufanya shughuli zao ambazo zinaweza kuwaletea vipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niongelee kuhusu *TBA*. *TBA* wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana; tatizo ni kwamba inawezekana hawana mtaji. Kwa hiyo naomba Serikali iangalie namna ya kuwatumia *TBA* katika miradi mbalimbali ya ujenzi inayoendelea nchini ili waweze na wao kuweza kwenda mbele katika kuongeza pato la Taifa. Kwa hiyo lengo ni kwamba wawaongezee hawa watu ili waweze kupata nanii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Waziri naomba niulize, katika maziwa makuu yanayotajwa sijasikia Ziwa Rukwa. Sasa nataka kujua Ziwa Rukwa wana mpango gani nalo, maana yake wavuvi wako kule; lakini nasikia Ziwa Tanganyika, Victoria na Ziwa Nyasa, lakini sijasikia Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa, kama walikuwa hawajaliweka katika mpango wa Maziwa Makuu, naomba wafahamu kwamba lile ziwa nalo lipo na naomba liingizwe katika mpango wa maendeleo namna ambavyo wataweza kulishughulikia tuone namna gani ambavyo wavuvi wa upande wa kule nao wanafaidika kutokana na miradi ambayo wanakuwa wameiweka kwenye Maziwa Makuu ambayo Ziwa Rukwa hawajaliweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo naomba nikumbushe barabara yangu ya Kibaoni kupita mpaka Muze mpaka Kilyamatundu ambayo waliahidi kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami, lakini ipo kwenye ilani ya Chama cha Mapinduzi tangu awamu iliyopita mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tupate majibu, je, barabara hii itajengwa lini na itaanza lini na itakwisha lini? Kwa sababu ni zaidi ya miaka 15 ipo kwenye maandishi ambayo haijaweza kufanyiwa lolote. Ni kutoka Kibaoni kupita Majimoto–Kasansa-Mfinga- Muze mpaka Kilyamatundu. Kwa hiyo tunaomba kabisa tutake kujua hatma ya barabara hiyo ikoje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo napenda tu niwapongeze Wizara kwa namna ambavyo wamekuwa wasikivu, hasa Mheshimiwa Waziri ni msikivu sana tunaposema shida zetu anatusikiliza na Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni sikivu, Rais wetu ni msikivu, napenda tu niwatie moyo, naomba wasikate tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua changamoto za hali ya hewa ni nyingi sana, tuangalie, tushirikiane na Ma-*engineer*

kama walivyosema na watu wa hali ya hewa tuone tunajenga barabara za aina gani ili tuweze kukabiliana na majanga yanayotokana na hali ya hewa hasa mafuriko yanayoendelea hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kikwembe, tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Kafumu na baadaye Mheshimiwa Joram Hongoli ajiandae.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niongee. Niliomba dakika 10 za kikanuni kwa sababu sijawahi kuchangia kwa mwaka mzima.

**MWENYEKITI:** Dakika 10 Mheshimiwa Kafumu.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mungu kwa kunipa nafasi hii tena kwa mwaka huu ili niweze kuchangia habari za wananchi wa Igunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti,, nataka niseme na jambo hili nimeendelea kulisema kila wakati, kijiolojia Jimbo la Igunga ni ziwa lililokauka miaka 60 elfu iliyopita. Narudia hili ili Mheshimiwa Waziri anielewe, kwamba kujenga barabara kwenye eneo hilo la Mbuga ni lazima ujenge tuta kubwa. Halmashauri imeshindwa kujenga barabara hizi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya zaidi Jimbo la Igunga halina barabara hata moja ya *TANROADS*. Tuna kata 13 ziko kwenye jimbo hili, sasa hivi ukienda hakuna hata kata moja ambayo unaweza kufika kwa sababu hapafikiki kabisa. Nimeomba mwaka jana na naomba tena kwa Mheshimiwa Waziri, Igunga hatuna barabara, tunaomba waje watutengenezee barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2014, 2015 na 2016 tuliomba barabara ya kutoka Igurubi kuja Igunga ipandishwe hadhi. Barabara hii inaunganisha wilaya yetu na mkoa wetu na Mkoa wa Shinyanga. Hata hivyo, kwa bahati mbaya sana wakatuambia kwamba wameirudisha *TARURA,* kwa kweli inatusikitisha sana, jimbo lisilo na barabara yoyote ya *TANROADS* inayohudumiwa na mkoa halafu wakairudisha *TARURA* tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni muhimu kuliko barabara zote kwenye Jimbo la Igunga kwa sababu sisi Jimbo la Igunga tunalima asilimia 90 ya pamba inayolimwa Mkoa wa Tabora. Sasa hivi ndiyo tunaozalisha mbegu kwa ajili ya wakulima wa pamba Tanzania. Hiyo mbegu au pamba inayozalisha hiyo mbegu inatoka kwenye barabara hii. Ziko kata kama 13 kwenye barabara hii ambazo zimelima pamba mwaka huu vizuri na tunategemea barabara hii ndiyo ibebe pamba hizo kutoka kwenye maeneo hayo, halafu wanatuambia kwamba imerudi *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli samahani sana nashindwa kuongea, naongea kwa uchungu na wananchi wa Igunga wananisikia. Barabara ya kutoka Igurubi kwenda Igunga tuliomba ipandishwe na tunaomba bado ipandishwe *TARURA* hawaiwezi. Sasa hivi ukitoka Igunga kwenda Igurubi hamna mtu anayeweza kwenda tena. Naomba sana Mheshimiwa Waziri anisikilize safari hii. Kwenye kitabu hiki cha bajeti mimi sina barabara yoyote humo ndani, nasema hapa kwa sababu ni kama vile wananchi wa jimbo lile wamesahauliwa wameachwa. Kuna Wabunge wamesema hapa hivi Jimbo la Igunga tuna matatizo gani au tumekosa nini hasa? Naomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingine ambayo tuliomba ipandishwa hadhi ni barabara ya kutoka Igunga kwenda Itumba mpaka Loya. Hii barabara inafungua tena Mkoa wa Tabora inaunganisha na ile barabara wanayoifungua inatoka Tura kwenda Iyumbu na ukiziunganisha hizo barabara unakwenda mpaka Mbeya.

Mheshimiwa Spika, tuliomba ipandishwe hadhi, makaratasi yote tulipeleka na ikakubalika, lakini leo tumeambiwa tena bado iko *TARURA* na *TARURA* hawana uwezo. Sasa hivi hiyo barabara ya kutoka Igunga kwenda Itumba kupitia Mwanzugi daraja limebomolewa kabisa na kuna Mkandarasi alikuwa anajaribu kujenga pale, lakini hana fedha ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi niliuliza swali watafanya fanyaje basi kutusaidia barabara hiyo haipitiki kabisa saa hizi na huko ndiyo nyumbani kwetu, mimi nikifika kule inabidi nitembee kwa mguu kwenda nyumbani kwetu. Naomba tena hii barabara kama wanaweza kuipandisha hadhi ili wafungue Mkoa wa Tabora, wafungue jimbo hili liunganike na Singida na Mbeya, litakuwa jambo zuri kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli naomba tena, Mheshimiwa Waziri kama anaweza kuja kututembelea Igunga aje; pamoja na kwamba kuna barabara moja tu kuu ya kwenda Mwanza kutoka Singida basi aje tumpitishe hata kidogo wakati wa masika aone mambo yalivyo, nadhani anaweza akaelewa hiki ninachokisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Igunga kwa sasa hivi hawawasiliani kabisa, hakuna mtu anayeweza kutoka Igurubi akaja Igunga, hakuna mtu anayeweza kutoka Itumba akaja mjini Igunga, hakuna mtu anayetoka hata Isugiro pale karibu karibu pale akaja mjini, hali ni mbaya kweli kweli na wananchi wanasema sasa Mheshimiwa Mbunge tunafanyaje? Nikawaambia nitalisemea hili jambo na saa hizi wanaweza kuwa wananisikia. Hamna Bunge *live* lakini nadhani nitapeleka kibwagizo kidogo wasikilize sikilize haya ninayoyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakinisaidia hizo barabara mbili wakafungua tukatoka tunaweza kutoka Kolandoto tukapita Ukenyenge, tukaja Igurubi, tukaja Mwamakona, Mbutu, Igunga tukaenda Itumba tukaenda Loya, Tura tukaenda mpaka Mbeya, watakuwa wamenisaidia sana. Kwanza wamefungua maeneo ya kiuchumi, pamba yote ipo

maeneo hayo kama nilivyosema. Upande wa huku chini kuna mifugo, *concentration* ya mifugo mingi iko kusini mwa Igunga mpaka Loya kwa ndugu yangu wa Igalula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakifungua hii barabara tutakuwa na ng'ombe wengi ambao watafikia minada. Sasa hivi tunapeleka ng'ombe kwenye minada ya Singida. Tunaomba sana Waheshimiwa Mawaziri hebu wanisikilize na mimi, naongea taratibu kwa uchungu ili wanisikilize jamani, tafadhali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nataka kusema kuna madaraja ambayo yanaunganisha kata kwa kata ambayo ni makubwa kiasi ambacho hayawezi kujengwa na halmashauri wala na *TARURA*. Naomba madaraja hayo nitakayoyataja wayafanye kama walivyofanya daraja la Mbutu. Daraja la Mbutu lilikuwa ni daraja lililokuwa chini ya halmashauri lakini kwa umuhimu wake lilijengwa na mradi maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madaraja hayo pamoja na daraja la kutoka Igunga kwenda Mwanzugi, mahali ambapo saa hizi pamebomolewa panahitaji madaraja zaidi ya matano, mkandarasi aliyepo hawezi kuyajenga. Tuna daraja la kutoka Bukoko kwenda Mtungulu Mto Ncheli, mto mkubwa sana, watu wa Ncheli kule pamoja na Mtungulu hawawezi kuwasiliana na wilaya, kwa sasa hivi wanakaa huko mpaka mvua ziishe. Ni daraja kubwa kweli kweli linahitaji bilioni kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna daraja la kutoka Itunduru kwenda Kagongwa, wananchi wale wakati wa mvua lazima watembee kwa mguu, wanajaribu kwenda Shinyanga kwa upande wa pili. Kuja huku hawawezi, ni daraja kubwa kweli, halmashauri haiwezi pamoja na *TARURA* haiwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, daraja la mwisho, ni kutoka Igunga kwenda Isugiro, ni hapo hapo karibu. Mto Igogo ambao unajaza maji kwenye bwawa la Igogo unapotoa

maji unakatisha barabara, haiwezekani kabisa kujenga daraja hilo na halipo hilo daraja. Naomba Mheshimiwa Waziri wanisaidie ili na mimi angalau niwe kama wengine kama kata zingine, kama wilaya zingine, kama majimbo mengine niwe na barabara hata za *TANROADS* mbili, tatu hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunisikiliza na Mungu awabariki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Dkt. Kafumu. Tunaendelea na Mheshimiwa Hongoli, baadaye Mheshimiwa Abbas Mwinyi na Mheshimiwa Andrew Chenge wajiandae.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua dakika 10?

**MWENYEKITI:** Dakika kumi, kumi.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nianze kwa kuwapongeza sana Mawaziri wanaosimamia Wizara, hii kwa maana ya Waziri Mheshimiwa Profesa Mbarawa, Mheshimiwa Nditiye na Mheshimiwa Kwandikwa na Makatibu Wakuu wote na watumishi wote wa Wizara hii ya Ujenzi kwa namna wanavyofanya kazi usiku na mchana kuhakikisha kwamba miundombinu mingi inatengenezwa hasa barabara na mambo mengine ya viwanja vya ndege na bandari. Niwapongeze sana, wanafanya kazi kubwa sana ambayo itasaidia kusukuma maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haipingiki ni kwamba tunavyoboresha barabara, tunavyoboresha viwanja vya ndege, tunavyoboresha bandari na miundombinu mingine tunachochea kwa kasi kubwa sana maendeleo. Kwa hiyo naipongeza sana Serikali, inafanya kazi kubwa sana. Tayari tumeshaona maeneo ambako barabara za lami zimefunguliwa, maeneo ambako kuna ujenzi wa reli na maeneo mengine ambapo miundombinu inatengenezwa, tayari kasi ya maendeleo imeanza kuonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe Serikali tuendelee bila kukata tamaa na kusikiliza maneno ya watu ambao wanabeza maendeleo haya. Tumwombe Mheshimiwa Rais aendelee kutusaidia kuhakikisha kwamba Watanzania tunatoka hapa tulipo tunaenda mbali zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuongelea kuhusu Jimbo langu hasa barabara ile ya Kibena – Lupembe – Madeke - Morogoro. Barabara hii inaunganisha Mkoa wa Njombe na Morogoro na ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu, lakini pia kwa uchumi wa Mkoa wa Njombe. Katika eneo ambako barabara hii inapita, eneo lote la Lupembe na Jimbo zima tunazalisha mbao kwa wingi sana. Mbao mnazoziona Dodoma asilimia 40 zinatoka kule Lupembe lakini eneo hili pia tunazalisha nguzo za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema hapa kwamba tunataka kila kijiji kiwe na umeme, nguzo zinatoka katika maeneo haya kwa asilimia kubwa sana. Eneo hili pia tunazalisha chai kwa wingi sana, kahawa, mahindi, maharage na aina zote za matunda kama vile parachichi, papai, nanasi, ndizi na matunda mengine mengi. Eneo hili lina mvua nyingi, takribani miezi nane katika kipindi cha mwaka mzima ni kipindi cha mvua. Kwa hiyo, unaweza ukaona kwa namna gani ni muhimu sana hizi barabara za maeneo haya ziweze kutengenezwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka 2016/2017, barabara hii ilipangiwa shilingi bilioni nane kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami na mwaka wa 2017/2018, tulipanga shilingi bilioni mbili na mwaka huu nashukuru sana Wizara na Serikali kwa ujumla tumepangiwa shilingi bilioni tano. Niombe sana bado barabara hii haijatangazwa kwa maana ya zabuni, haijatangazwa ili kuweza kumpata mkandarasi ili aanze kutengeneza barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba upembuzi yakinifu umeshakamilika, usanifu umeshafanyika

lakini bado ujenzi wake haujatangazwa. Niombe sana Wizara hii ya Ujenzi itusaidie ili barabara hii iweze kutengenezwa kwa kiwango cha lami na hatimaye tuweze kusafirisha mazao haya niliyoyataja kwa urahisi zaidi ili yaweze kufikia soko kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukipoteza fedha nyingi sana hasa kwenye mazao haya ya chai, mbao na mazao ya matunda kama nilivyoyataja. Kwa mfano, mwaka huu tu kuanzia Januari mpaka sasa hivi mwezi wa kwanza wananchi wa Madeke walipakia nanasi tani 40 kwenda kuuza sokoni lakini tani hizi zote 40 zimeozea njiani kwa sababu ya ubovu wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo katika barabara hii yameharibika, magari hayawezi kupita mfano maeneo ya Mtakuja, baadhi ya maeneo ya Kidegembye na maeneo mengine mengi tu. Kwa hiyo, unaweza ukaona jinsi tunavyopoteza uchumi katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki mbili zilizopita tumepakia maparachichi tani 30 katika vijiji viwili tu, unaweza ukaona ni shilingi ngapi hizo. Baada ya kuwaka jua kidogo tu siku mbili, tatu tukaweza kusafirisha tani 30 za parachichi kutoka kwenye vijiji viwili tu na parachichi kilo moja ni Sh.1,150. Kwa hiyo, unaweza ukaona ni namna gani hii barabara inavyochelewa kutengenezwa tunavyopoteza fedha nyingi na wananchi wanavyoingia hasara kutokana na ubovu wa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sana Serikali barabara hii tuipe kipaumbele ili angalau mwaka huu mara baada ya kupitisha bajeti hii, basi itangazwe, tupate mkandarasi aanze kutengeneza barabara hii. Kwa sababu tukiunganisha Mkoa wa Njombe na Morogoro na Mkoa wa Morogoro ni wazalishaji wakubwa sana naamini pato la Taifa litaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukiunganisha kwa mfano, Mkoa wa Njombe na Morogoro, tukaunganisha Mkoa

wa Njombe, Makete na Mbeya, tukaunganisha Mkoa wa Njombe kupitia Ludewa na mikoa mingine kimsingi tutapata maendeleo makubwa sana kwa sababu haya ndiyo maeneo yanayotegemewa kwa chakula na ndiyo maeneo yenye uchumi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri hii barabara wananchi wetu wa Jimbo la Lupembe hawanielewi ni kwa nini barabara hii kandarasi haitangazwi wakati imesanifiwa muda mrefu na tayari ilitakiwa iwe imeshaanza kutengenezwa muda mrefu. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri ashughulikie suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna barabara moja ya Ilunda – Igongolo – Kivitu - Ilengititu – Kifumbe. Barabara hii inasimamiwa na *TANROADS,* lakini imekuwa ikitengenezwa kilometa tisa tu, imeishia sehemu fulani njiani, kule mbele haiendelei kutengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana *TANROADS* waongeze kipande kile kingine kwa maana waende Kijiji cha Kivitu kutoka Idonda, Igongoro waende Kivitu baadaye iende Ilengititu na itokeze kule Kifumbe ambako ni Jimbo la Makambako ili angalau tuweze kutengeneza mtandao mzuri wa barabara na hatimaye mazao ya eneo lile yaweze kusafirishwa kirahisi zaidi hasa wakati wa mvua. Kama nilivyosema Jimbo langu mimi linapata kipindi kirefu sana cha mvua, miezi nane mvua inanyesha, kwa hiyo inapofikia wakati wa kuvuna mazao haya hayawezi kufikia soko kwa urahisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia kuhusu minara ya simu kwa maana ya mawasiliano. Kuna kata kama tano hivi simu hazishiki vizuri hasa Kata zile za Ninga, Ikondo, Mfiga lakini pia na maeneo mengine ya vijijini ambako simu hazishiki vizuri. Nilishapeleka taarifa na nashukuru kwamba Waziri aliniahidi kwamba mwaka huu wa fedha watapeleka minara katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana tujitahidi ili tuweze kufungua mawasiliano na hatimaye waweze kufanya biashara na shughuli zao za kiuchumi vizuri. Maana biashara za kilimo ni lazima uwe na mawasiliano ya karibu sana na soko. Kama hakuna mawasiliano ni vigumu sana kujua ni wapi bidhaa yako uweze kuipeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukiwafungulia mawasiliano na tukawa tumetengeneza barabara hizi kama nilivyosema hasa barabara kuu hii ya Kibena – Lupembe – Madeke – Mlimba - Morogoro, kasi ya uchumi itakua na hatimaye maisha ya Watanzania yataboreshwa kwa sababu uzalishaji utakuwa umeongezeka na bidhaa zao zitazalishwa kirahisi zaidi kwa sababu barabara ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nirudie kuipongeza Serikali, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa jitihada anazozifanya kuhakikisha kwamba anafungua mawasiliano katika nchi hii. Niwapongeze Mawaziri wote kwa maana ya Waziri Profesa Mbarawa na Naibu Mawaziri Mheshimiwa Nditiye na Mheshimiwa Kwandikwa. Pia nimpongeze Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa ambayo wanafanya. Niombe sana Mwenyezi Mungu awabariki ili waendelee kuwa na afya njema na hatimaye waweze kutuletea sisi Watanzania maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hongoli. Tunaendelea na Mheshimiwa Abbas Mwinyi baadaye Mheshimiwa Andrew Chenge na Mheshimiwa Mwamoto wajiandae.

**MHE. ABBAS ALI HASSAN MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na kutuwezesha kukutana asubuhi ya leo

kwa lengo la kujadili maendeleo ya sekta ya ujenzi, uchukuzi na mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii ya adhimu na adimu ya kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli na Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mheshimiwa Ali Mohamed Shein kwa kutekeleza kwa umahiri mkubwa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano imefanya kazi kubwa ndani ya kipindi cha muda mfupi sana na baadhi ya mambo waliyofanya yaliyoleta tija kubwa ni pamoja na kupata mafanikio katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya afya, bajeti imeongezeka kwa kiasi kikubwa sana na sasa hivi hata hospitali zetu za rufaa msongamano wa wagonjwa umepungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatokana na kuimarisha hospitali zetu za wilaya na vituo vyetu vya afya. Sio hayo tu bali hata wale wagonjwa waliokuwa na matatizo ya kuwekewa figo *(kidney transplant)* na wale ambao walikuwa na matatizo ya moyo hali kadhalika sasa huduma tunazo hapa hapa nchini na kwa hali hiyo basi Serikali imeweza ku-*save* pesa nyingi za kuwapeleka nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nichukue fursa hii ya kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano pamoja na Naibu Mawaziri wake wawili, Mheshimiwa Nditiye na Mheshimiwa Kwandikwa kwa kazi nzuri sana ambayo wanaifanya na kutekeleza wajibu wao ipasavyo, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi ya leo mchango wangu utajielekeza katika maeneo matatu: usafiri wa anga ambapo mimi ni mdau mkubwa; Mamlaka ya Viwanja vya Ndege - *TAA (Tanzania Airport Authority)* pamoja na Mamlaka ya Udhibiti - *TCAA (Tanzania Civil Aviation Authority).* Kama muda utabakia basi nitazungumzia ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa cha *standard gauge. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuanze na usafiri wa anga. Nichukue tu fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la *ATCL* na timu yake kwa kazi nzuri sana wanayoifanya na kuandaa mpango mkakati wa muda mrefu wa kujiendesha. Naamini ukitekelezwa vizuri basi kutakuwepo na matunda mazuri ambayo yatazaliwa kutokana na mpango huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina shauku kubwa sasa kuelewa, je, shirika hili lini hasa litaanza kujiendesha lenyewe? Narudia tena swali hilo kwa Mheshimiwa Waziri, lini shirika hili litapata uwezo wa kujiendesha lenyewe? Sio hilo tu, muda gani sasa itatuchukua kurudisha gharama za uwekezaji ambao umewekezwa na Serikali? Nalo hilo ni swali la pili ambalo napenda kujua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshawahi kufanya kazi katika shirika hilo kwa muda wa miaka nane. Kwa kweli kipindi ambacho nilikuwa nafanya kazi, shirika hilo lilikuwa limegubikwa na ukata mkali, hata fedha ambazo ilikuwa tunapaswa sisi wafanyakazi kupelekewa katika Mifuko ya Hifadhi kama *PPF* zilikuwa haziendi kutokana na ukata huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuarifu kwamba sasa ukata huo na mwaka mmoja tu baada ya uwekezaji mambo yamekuwa mazuri zaidi. Sasa fedha zinapelekwa katika mifuko hiyo kwa wakati, shirika linaendesha mipango yake vizuri kabisa kwa maana ya kwamba linalipa kodi za Serikali na baadhi ya madeni ya shirika yamelipwa, kwa hiyo, hilo ni jambo jema sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna faida nyingi sana za kuboresha shirika hili la ndege. Faida ambazo zimepatikana ni pamoja na gharama nafuu za usafirishaji kwa kutumia anga na safari hivi sasa ni za uhakika kuliko ilivyokuwepo siku za nyuma. Kubwa zaidi ni kutengeneza ajira, tunategemea baada ya mwaka huu kumalizika shirika litakuwa limeajiri wafanyakazi takribani 600 ambapo hii ni utekelezaji wa moja kwa moja wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2015. Kwa hiyo, hili ni jambo jema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kidogo pale la kulipwa marubani. Marubani sasa hivi katika shirika letu wanapokea mishahara ambayo ipo chini kidogo na soko la ajira la ndani lilivyo, hili linashusha kidogo morali yao. Kwa hiyo basi, ningemwomba Mheshimiwa Waziri angalau basi awaongezee mishahara marubani wetu angalau ikubaliane na soko la ajira ya ndani. Kwa hiyo, hilo litakuwa ni jambo zuri sana na wenzetu wale watapata motisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ilivyo sasa ni kwamba shirika au nchi kwa ujumla wake imepungukiwa na kada hii ya wafanyakazi (marubani) kwa sababu hakuna *succession plan* nzuri kati ya wale marubani ambao wanamaliza muda wao na wale ambao wanaajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina taarifa kwamba kila shirika la ndege kwa maana ya waajiri kuna tozo la asilimia nne ambalo linakwenda kwenye programu ya *SDL (Scheme Development Levy)* ambapo sijui fedha hizi zinatumikaje au zimenufaisha marubani na ma-*engineer* wangapi. Kwa hiyo, napenda kujua manufaa ya hii *SDL* ambayo inatolewa na waajiri wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la viwanja vya ndege, *Tanzania Airport Authority* inasimamia viwanja 58. Kati ya hivyo vitatu tu ndiyo ambavyo vina manufaa kwa maana vinaweza kujiendesha vyenyewe, vilivyobakia vyote 55 haviwezi kujiendesha vyenyewe vinategemea faida ambayo inazalishwa na hivi viwanja vitatu ambavyo ni cha Mwanza, Arusha na Kilimanjaro nafikiri. Kwa hiyo, hii inapelekea mamlaka hiyo kupata fedha chache sana ya kuweza kutekeleza majukumu yake. Kwa hiyo... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Abbas Mwinyi.

**MHE. ABBAS ALI HASSAN MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Andrew Chenge, Mheshimiwa Mwamoto na Mheshimiwa Zungu wajiandae.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Nianze kwa kumpongeza sana mtoa hoja Mheshimiwa Profesa Mbarawa kwa hoja yake nzuri ambayo inatoa matumaini kwa Watanzania katika sekta zote tatu muhimu ambazo anaziongoza. Niwapongeze pia Naibu Mawaziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya. Tanzania inafunguka na inaunganishwa, sote tunaona, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitasema kwa kifupi katika maeneo ambayo nadhani ni muhimu. Moja ambalo nadhani tusaidiane Waheshimiwa Wabunge ni hili la *TANROADS* na *TARURA* kwa upande wa *financing.* Nimesikia mawazo mazuri tu ya Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na kuongeza nguvu ya *financing* lakini kwa kupendekeza kwamba asilimia 70 ambayo ndiyo inakwenda *TANROADS* na 30 inakwenda *TARURA* tufanye uwiano mzuri, ni wazo zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema, ukiangalia mtandao wa barabara zetu hizi za lami ambazo tunajenga kwa gharama kubwa, barabara kuu na za mikoa, sehemu kubwa ni kama asilimia tunayoweza kugharamia kwa matengenezo/matunzo ya kila mwaka haifiki asilimia 60. Sehemu kubwa ya barabara hizi hazitunzwi, sasa ukipunguza tena ukasema upeleke *TARURA* ujue *network* kubwa ya nchi hii ambayo tumeijenga kwa gharama kubwa itaharibika haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuendelee kuishauri vizuri Serikali, tutafute vyanzo vipya vya mapato badala ya kwenda na *approach* hii. Najua zoezi hili limekuwa linafanyika, tufike mahali basi tuone hii *road users' fee or charges,* mapendekezo yaliyokuwa yanafanyiwa kazi tumefika nayo wapi? Mimi naliona hilo ni bora kuliko hii ya kusema tukagawane mbao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia mimi nachokoza tena, hii *source* ya shilingi ya mafuta nasema kwa sasa tujaribu kuiangalia tena. Maana yake nasema tuangalie kuongeza katika bajeti ya Serikali mwaka huu ili tukatunishe *TARURA* kwa kuanzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza juhudi za Serikali kwa kazi inayofanyika Simiyu sasa hivi. Barabara ya Lamadi – Bariadi imekamilika, Mwigumbi – Maswa imekamilika, sehemu ya Bariadi – Maswa mkandarasi yuko *site* na bajeti tunaiona, shilingi bilioni kumi hizo zimetengwa na Serikali kwa mwaka ujao wa fedha. Matarajio yangu ni kwamba hata hicho kidogo kitapatikana ili mkandarasi afanye kazi na tuone kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Mto Sibiti, daraja hilo linalotuunganisha sisi kwenye barabara ya kutoka Bariadi - Singida - Arusha linaendelea vizuri, tunaipongeza Serikali. Tunataka tuone barabara unganishi kwa pande zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe radhi sana Mheshimiwa Waziri, jana wakati na-*chair* Kikao nilisoma kwa harakaharaka nikamwandikia ki-*note* kwa sababu nilikuwa sijaisoma vizuri hotuba yake, ilikuwa ni barabara ya zaidi ya miaka 30. Tunaongelea barabara ya kutoka Kolandoto – Lalago – Mwanhuzi – Matala – Mang'ola – Oldeani *Junction,* kila Waziri aliyepita pale Wizarani barabara hii ipo. Najua pesa ndiyo hivyo, ombi langu kwa sababu imo kwenye mpangokazi wa *TANROADS,* tufike basi mahali vipande ambavyo vimekamilika tuanze kuvitengeneza kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ukurasa wa 32, baada ya kumwomba samahani Mheshimiwa Waziri kwa mkanganyiko wangu wa jana, barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom - Mto Sibiti - Lalago – Maswa, mimi sina *problem* kwa sababu nataka tufungue nchi hii lakini unapoiangalia pale sehemu kubwa ya barabara hiyo kuanzia Kolandoto – Munze – Lalago – Mwanhuzi - Sibiti - Mang'ola - Oldeani

*Junction* tumeshafanya upembuzi yakinifu na *detailed design,* sasa wanapoichanganya hivi wanatuchanganya, si kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama *KfW* wanatoa hizi pesa tunawapongeza na tunawashukuru, lakini sehemu kubwa imeshafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Waheshimiwa napenda waje wanisaidie kwa maelezo yanayotosheleza kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda tusaidiane kuelewa. Hii barabara inayopendekezwa ya kutoka Karatu – Endebash, ninavyoifahamu ni kansa, unashuka nayo unakuja mpaka Kilimapunda pale, unashuka nayo Mbulu unakwenda Dongobesh unakwenda Haydom. Sasa napenda tusaidiane, ikitoka Haydom inaelekea wapi, inaenda Matala au Kidarafa? Napenda tuelewane maana hatuwezi kuwa tunafichana njia hii inapita wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na wazo la Serikali kwamba ikitoka pale tunarudi sasa Sibiti tunapandisha kwenda Mwanhuzi anayetaka kwenda Shinyanga anakata mpaka Lalago lakini ukifika pale Lalago unapandisha kwenda Maswa. Ndiyo utamu wa mapendekezo haya. Nadhani ma-*engineer* wote hebu waliangalie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadaye tungependa tuone barabara inayounganisha upande wa Singida, barabara ya kutoka Sibiti maana chemchemi unaiona pale, unashuka kuja Mkalama, si ndiyo hivyo, halafu unakuja Gamanga, Ilemo huku au unaweza ukaja moja kwa moja mpaka Iguguno, tusaidiwe kuelewa barabara unganishi ni ipi? Nataka tu wanisaidie lakini nataka maendeleo ya haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hizi tunazijenga kwa gharama kubwa. Nisingependa tugombanie fito, lakini angalau kama hii ya Kolandoto nairudia sana, tuwe na muono wa pamoja hasa katika maeneo ambayo hayana *connectivity* nzuri kama Mkoa mpya wa Simiyu. Nadhani Mheshimiwa Profesa Mbarawa atanielewa kwa nini nalisema kwa uchungu namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napongeza sana upande wa reli, napongeza sana reli ya kisasa kiwango cha kimataifa. Ombi langu kwa Serikali na nalisema kwa kujivuna, twendeni tukakope tushambulie maeneo yote kwa pamoja tusiende kwa spidi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Chenge. Tunaendelea na Mheshimiwa Mwamoto, baadaye Mheshimiwa Zungu na Mheshimiwa Dunstan Kitandula ajiandae.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hotuba ya Wizara hii. Kwanza kabisa, nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Profesa Mbarawa, Mheshimiwa Injinia Nditiye pamoja na Mheshimiwa Kwandikwa pamoja na wataalam wa Wizara. Nimshukuru Mheshimiwa Profesa Mbarawa kwa kazi nzuri aliyoifanya alipokuja kule jimboni kwangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mustakabali wa nchi hii unategemea sana miundombinu ya barabara. Tunakwenda kwenye nchi ya viwanda, tusipozungumza habari ya barabara, hakuna mafanikio tena kuhusu viwanda. Kwa hiyo, niwaombe sana hizi kelele ambazo tunapiga siyo kwa manufaa yetu bali ni kwa manufaa ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitakuwa na maneno mengi sana, nitakuwa na maneno kidogo sana. Kwanza nianze na barabara ya mkoa ya Kilolo ambayo inaanzia Iringa – Kilolo - Idete. Barabara hii si ngeni kwa sababu Marais wote waliopita walitoa ahadi, ni barabara ambayo iko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Mheshimiwa Profesa Mbarawa alifika na alituahidi alichotuahidi, wananchi wanaendelea kusubiri. Mheshimiwa Makamu wa Rais amefika, ameahidi na wananchi wanaendelea kusubiri.

Barabara hii siyo inaunganisha Kilolo tu, barabara ya Kilolo yenyewe sasa, tuliomba lami kutoka wilayani ni kilometa nane lakini inaunganika na kilometa tatu za Iringa Mjini, kilometa kumi za Kalenga, zote zinapita kwenye barabara hiyo zinafikia takribani kilometa 21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi ambayo tunayo ni ya kujenga kilometa mojamoja. Nilishawahi kuuliza hapa Bungeni, barabara hii kwa ahadi hiyo itajengwa kwa miaka 21, Mheshimiwa Profesa Mbarawa hatakuwepo kwenye nafasi hiyo, mimi sitakuwepo tena, miaka 21 mingi, ndugu yangu Mheshimiwa Injinia Nditiye na yeye hatakuwepo na Mheshimiwa Kwandikwa hatakuwepo. Sasa tunaomba waitendee haki, unaposikia ujenzi wa Makao Makuu Dodoma mbao asilimia 60 zinatoka Kilolo. Kama kweli zinatoka Kilolo inakuwaje unamwacha mtu ambaye analeta maendeleo kwenye makao makuu ya nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali kubwa, nzuri ya halmashauri ya wilaya imejengwa Kilolo, ndiyo hospitali ya mfano, lakini hospitali ile itawasaidia hata watu wa kutoka Iringa Mjini, Mufindi na sehemu nyingine, unawasafirishaje? Sidhani kama kuna mgonjwa ambaye atapona akiwa anapelekwa kwenye ile hospitali. Ili waendelee kuwaombea vizuri, Mheshimiwa Profesa Mbarawa afanye lile Mungu atakalomjalia kuhakikisha kwamba hizo kilometa tunazipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Mfugale ambaye kwa kweli ametusaidia sana nchi hii pamoja na Mkoa wa Iringa kwa ujumla kwa kujua umuhimu wake. Mwenyezi Mungu aendelee kumpa afya njema, aendelee kumlinda ili aendelee kutusaidia pale atakapoweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ya mkoa inakwenda mpaka Idete, nimeshawahi kusema hapa Bungeni kwamba barabara pekee inayounganisha Mkoa wa Iringa na Mkoa wa Morogoro inapita kwenye Milima ya Kitonga. Siku milima ile mawe yakadondokea barabarani

au kukatokea tafrani yoyote, uwezekano wa magari ya kutoka South Africa, Zambia, Malawi kwenda Dar es Salaam au Morogoro itakuwa hakuna. Kwa hiyo, barabara pekee ni kuunganisha Idete – Itonya – Muhanga - Morogoro (Mbingu) kwa Mheshimiwa Susan Kiwanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ile siyo ndefu, ni kilometa takribani 25, wananchi wameshaifungua na ahadi ya mwanzo ilikuwa kwamba barabara ile mkoa iichukue kwa sababu ni barabara ambayo ilikuwa ya mkoa. Sasa baada ya *TARURA* kuanza bado *TANROADS* wanaweza kuweka mkono wao hata kwa wataalam ili barabara ile sasa ipitike. Leo tunazungumza hapa kama mzaha lakini kuna siku watakuja kukumbuka maneno yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sitaki sana kusema kwa sababu nimeshasema sana kuhusu suala hili niende kwenye mawasiliano. Ndugu yangu Mheshimiwa Injinia Nditiye anajua tumetoka wote Kibondo kule, sasa akija akinitupa leo kwa kukosa mawasiliano nikienda Kibondo nitazungumza kule kwamba ndugu yangu ameshindwa kunisaidia, itakuwa siyo kitu kizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sehemu, kwa mfano, Ifua, Udekwa, Irambo, Ibumu, Magana, Ilindi ambako ni Mahenge, Imalutwa, Lugalo, hivyo ni Vijiji, Mbawi, Masisiwe, Isere, Ukwega, Ikula, Ruaha, Mbuyuni na Isagwa hakuna kabisa mawasiliano. Bado narudi palepale, tunakwenda kwenye nchi ya viwanda, unaendaje kwenye nchi ya viwanda wakati mawasiliano hakuna, barabara hakuna. Kwa hiyo, mimi nimwombe ndugu yangu, aliniahidi kufanya ziara, hebu afanye ziara. Kama atakuwa hana mafuta niko tayari kumwekea ili tuweze kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kwandikwa na yeye kwa sababu Mheshimiwa Profesa Mbarawa alishafika, kazi sasa ni yeye, wao ndiyo wasaidizi wake, aje Kilolo sio mbali, kilometa zile sio nyingi, ziko kwenye ilani. Nikileta *Hansard* hapa toka mwaka 2000 nikiwa Mbunge nimekuwa

nikiambiwa habari zilezile. Sasa tusimuangushe Mheshimiwa Profesa Mbarawa, kama kweli wanampenda twende sote pale, sio mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Rais, Mheshimiwa Dkt. Magufuli katutengenezea barabara, kutoka Iringa mpaka Dodoma ni saa mbili na nusu, hata kama Bunge limeahirishwa, twende tunarudi tunakuja kutoa maoni hapa. Mnajua hasira za watu wa Iringa, kuna mambo mengi ambayo hayaendi vizuri, sasa hivi hatujinyongi tena, tunapanda juu ya mti unajitupa kwenye lami unakufa vizuri. Kwa hiyo, tutengenezeeni lami tu ili tuache kujitundika kwenye miti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndege, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, amefanya kazi kubwa, ametuletea ndege za uhakika na kelele hizi zilikuwa zinapigwa nchi gani haina hata ndege, lakini leo tuna ndege. Mheshimiwa aendelee kuongeza kwa sababu siku zote vita ya kiuchumi lazima akubali na kelele lazima zipigwe. Wako ambao watasema huyo, huyo, yeye asigeuke nyuma, aende, pale alipo na sisi tupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *standard gauge,* hata kama haipiti Kilolo, Iringa huko ni kwa ajili ya nchi hii. Barabara zetu zinakufa kwa sababu hatuna reli, kila mtu anajua hilo. Kwa hiyo, reli ile itakwenda mpaka Moshi kwa Mheshimiwa Mdee kule itafika na tunaomba waifungue ile. Mheshimiwa Injinia Nditiye wajitahidi waifungue ili Mheshimiwa Mdee naye aone manufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema pia suala la kuimarisha barabara nyingine hasa hapa Dodoma. Mji huu umeshakuwa mkubwa na tumeshaanza kupata shida kwenye hizi barabara. Leo hii kama wanafikiria mambo ya mabasi yaendayo kasi hiyo mipango ianze sasa, siyo ifikie wakati tuanze kubomoa nyumba za watu, itakuwa ni aibu. Tufanye sasa, kama kuna madaraja wa-*plan* sasa hivi ili baadaye isije ikatokea bomoabomoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sipendi kuzungumza maneno mengi kwa sababu siasa ya Kilolo ni barabara. Waheshimiwa Wabunge wanashindwa hata kufanya ziara sehemu nyingine kwa sababu barabara zimeharibika. Unapokwenda kule unaulizwa habari ya barabara na uliahidi kutengeneza barabara unajisikia aibu. Kwa hiyo, tutengenezeeni barabara twende majimboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwamoto. Tunaendelea na Mheshimiwa Zungu dakika tano na baadaye Mheshimiwa Kitandula na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka wajiandae.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa sababu muda wangu ni mdogo, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. Nawapongeza Serikali lakini tupongeze na jitihada za Mheshimiwa Rais kutaka ku-*excel* uchumi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna ndege nzuri, jana nilikuwa nasikia mtu anasema ndege hizi hazifai. Ndege hizi zina *store equipment system* ambazo zina-*show take off* na *landing,* zinafaa kwenye viwanja vyetu vidogo ambavyo haviwezi kubeba ndege ambazo zinachukua *runway* ndefu sana. Kwa hiyo, tupongeze jitihada hizi za ndege hizi kuweza kutumika katika viwanja vingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ndege hizi hazitumiki sawasawa kwa sababu viwanja vyetu havina ubora wa kupokea ndege husika. Hata viwanja vingine, kuna kipindi viwanja vyetu vinashindwa kuchukua ndege au ndege kutua kutokana na hali mbaya ya hewa, *simply* kwa sababu hatuna *transponder instrument landing system* ambazo katika mazingira ya hali yoyote ya hewa ndege hizi zinaweza kutua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze ku-*capitalize* matumizi ya ndege hizi, kitaalam ndege huwa haipumziki,

kinachopumzika ni rubani na *crew* ambao wako kwenye ndege. Kwa hiyo, tungekuwa na viwanja ambavyo vina taa, *instrument landing system, precision approach path indicators* na *vertical approach slope indicators,* itasaidia ndege hizi kuwa *capitalized* na kutumika kwa kipindi chote 24/7. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri alizingatie hili aboreshe viwanja ndege ziweze kuruka kwa usalama wa abiria, vifaa vyenyewe na viwanja vya ndege vyenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la reli hii ya *SGR,* ni hatua kubwa sana ambayo tumepiga na naipongeza Serikali. Reli hii kama haina mizigo itakuwa haiwezi kufanya kazi vizuri, haitaweza kulipa deni kwa muda unaotakiwa. *Solution* ya reli hii ni mizigo na bandari ya Dar es Salaam iko *congested.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kuwa kuna utaratibu wa mazungumzo lakini yasiwe taratibu. Mpaka leo ujenzi wa bandari ya Bagamoyo bado hakieleweki, bila bandari hii reli yetu itakosa mizigo na tutashindwa kurudisha pesa hizi mapema, tusiogope kukopa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali ijaribu na wataalam ambao wapo na wazuri wakae na mwekezaji wakubaliane *twenty equivalent units* za makontena yatakayoingia kwenye bandari ni mangapi, waweze kujua *wharfage* ya mwekezaji ni ngapi na *duty* ya Serikali ni ngapi. Tukienda hivi tutafanikiwa kujenga reli na bandari kubwa ya kisasa ya kuweza kubeba mizigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imekumbwa na mafuriko, mafuriko hayana nguvu mbele ya utaalam na *engineering* ya binadamu. Katika Bonde la Msimbazi ambalo linaanza kutoka Segerea linakwenda *Surrender Bridge.* Jambo ni dogo sana, Serikali wametuambia katika mpango wa *DMDP* wana mpango wa kuboresha mto huu, lakini wanakopa hizi pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako watu ambao wamejitokeza ambao watalipa fidia na kutengeneza

miundombinu ya mfereji huu, kwa nini hawa watu wasipewe kazi hii? Kwa nini Serikali mkope halafu katika kukopa kwenu hakuna *component ya* fidia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wananchi hawa hawatalipwa fidia sisi hatutakubali. Tunataka wananchi wetu walipwe fidia kwa sababu *they have been there for the last sixty years.* Kama kuna mtu kajitokeza ni bora afanye yeye na Serikali mkope kwa kufanya mambo mengine ili wananchi hawa waende katika sehemu bora zaidi na kuendeleza maisha yao. Hawa ndiyo watu walionipigia kura mimi lazima niwatete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Dodoma - Dar es Salaam imeshakwisha, iko *congested* na ni ndogo. Namwomba Waziri, tayari wako watu wamejitokeza wa Kuwait Fund kui-*finance* barabara hii, wazungumze nao ili waweze kujenga barabara hii kwa njia sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo, nikushukuru sana na naunga mkono hoja kwa kazi nzuri anayofanya Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zungu. Tunaendelea na Mheshimiwa Dunstan Kitandula baadaye Mheshimiwa Zuberi Kuchauka na Mheshimiwa Joyce Mukya ajiandae.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nami nichangie kwenye hoja iliyopo mbele yetu. Nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa wingi wa baraka zake ambazo amezidi kutukirimia siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumpongeza na kumshukuru sana Naibu Waziri, ndugu yangu Mheshimiwa Kwandikwa kwa ziara aliyoifanya kule Mkinga. Nashukuru sana kwa sababu ziara ile ilijenga matumaini kwa watu wa Maramba, Gombero, Mtonibombo, Daluni, wakijua

kilio chao cha muda mrefu sasa kimepata jibu, lakini nimepitia vitabu hivi, bahati mbaya sana kilio chao hakijasikika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Mabokweni – Maramba – Bombomtoni – Umba – Kisiwani – Same - Mkomazi ni barabara ya kuunganisha Mkoa wa Tanga na Kilimanjaro, ni barabara ya kimkakati, kiuchumi na ni barabara ya ulinzi. Ni barabara ambayo wagombea wetu wote wa urais kila wakati wa kuomba kura wamekuwa wakiipitia barabara hiyo, ni barabara ambayo imepewa ahadi mara nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawa wamekuwa na subira sana kwa barabara hii lakini barabara hii ni kero na imekuwa mateso kwao. Nilikuwa nasoma kitabu hiki nikadhani angalau safari hii tutaona neno *feasibility study* inafanyika kwa barabara ile lakini hakuna. Ni barabara ambayo nimeisemea sasa kwa miaka saba mfululizo, lakini Serikali haisikii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii mzee wangu Mheshimiwa Kikwete alipopita aliposikia kelele hizi akasema tuiweke kwenye utaratibu wa *Performance-Based Management and Maintenance* ili angalau iwe inapitika, tukafanya hivyo. Baadaye tukasema iingizwe kwenye mpango maalum kupitia *MCC*, namshukuru sana dada yangu aliyekuwa Mkuu wa Mkoa, dada Chiku Galawa akapambana tukaleta maombi barabara hii itengenezwe kupitia *MCC,* lakini haikuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano alipokuja kwenye kuomba kura ndugu zetu wa Maramba wakaomba, akasema amesikia. Alipofika Daluni Kibaoni pale wananchi wakamlilia, akatoa ahadi. Tumeisemea barabara hii lakini kwa masikitiko makubwa kilio chetu hakijasikika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli barabara inayounganisha Mbuga ya Saadani na Mbuga ya Mkomazi

hatuioni umuhimu wake? Hivi kweli barabara inayounganisha Mbuga ya Tsavo na Mbuga ya Mkomazi na Kilimanjaro hatuioni umuhimu wake? Hivi kweli tunashindwa kukamata kundi la watalii kutoka Mombasa ili waje kutembelea eneo la Mto Umba na Mbuga ya Saadani mpaka Kilimanjaro hatuoni umuhimu wake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi barabara inayotupa uhakika wa usalama wa nchi yetu kiulinzi hatuoni umuhimu wake? Hivi barabara inayopita kwenye maeneo ya uzalishaji wa kahawa, chai, mpunga, mkonge hatuoni umuhimu wake? Barabara hii haituweki vizuri kisiasa. Mheshimiwa Waziri alikuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya chama chetu, ninaposema barabara hii haituweki vizuri kisiasa, najua anaelewa. Naomba kilio hiki kisikike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni bandari. Pale Mkinga tuna wawekezaji wa *Hengya Cement* na kampuni ya Sinoma wameamua kuja kuwekeza pale watajenga viwanda kumi. Miongoni mwa viwanda hivyo kutakuwa na kiwanda kimoja cha *cement* chenye uwezo wa kuzalisha tani milioni saba kwa mwaka. Maana yake unazungumzia kiwanda ambacho *production* inayofanyika sasa nchini inakuja kufanywa na kiwanda kimoja. Tunazungumzia uwekezaji wa trilioni 7.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameomba pamoja na uwekezaji huo, wapewe ruhusa wajenge gati itakayowawezesha kusafirisha mizigo yao wenyewe. Wanataka kujenga gati ile kwa utaratibu *Build Operate and Transfer* watumie fedha zao wenyewe. Sasa huko bandarini kuna mtu nasikia ameweka ngumu hataki kutoa kibali. Uwekezaji wa trilioni saba kuna mtu mmoja anakwamisha, hatuwezi kukubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisipopata majibu ya kuridhisha nakusudia kushika shilingi. Waheshimiwa Wabunge, naomba kwenye hili mniunge mkono. Hatuwezi kuacha uwekezaji mkubwa wa trilioni saba uzuiwe na mtu mmoja. Hatuwezi kukubali ajira ya watu 4,000 izuiwe na mtu mmoja

eti ana ndoto ya kutujengea bandari ya Tanga iwe na uwezo wa kuwa *valid* kwa miaka 200 ijayo, lakini wakati akisema hayo sisi tunazo taarifa watu wa Tanga kwamba tangu mwaka 77 kwenye *business plan* ya Mamlaka ya Bandari imekuwa ikisema itajenga Bandari ya Mwambani haijatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna mtu ana hela zake anataka ajenge gati ili uwekezaji mkubwa wa namna hii utokee sisi tunaweka ngumu, haiwezekani. Wakati tunaweka ngumu hii ya kuruhusu kujenga gati pale Pangani Mamlaka hiihii ya Bandari imejenga gati, kwa nini Pangani tujenge gati lakini Mkinga iwe nongwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaunga mkono hoja nikipata majibu ya uhakika. Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kitandula. Tunaendelea na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka baadaye Mheshimiwa Joyce Mukya na Mheshimiwa Willy Qambalo wajiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili nichangie kwenye hoja iliyo mbele yetu. Naomba nianze mchango wangu kwa maneno mawili: Nangurukuru na Liwale, nitatoa ufafanuzi baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mchango wangu kwa leo kabla ya kusema chochote, kwanza nawashukuru Mawaziri wote wanaohudumu kwenye Wizara hii kwa utendaji wao. Nasikitika tu kwamba wataangushwa na Mheshimiwa Mpango kwa sababu ili waonekane kwamba kweli wanaweza Mheshimiwa Mpango lazima awape pesa. Naomba vilevile kuwashukuru siyo tu Mawaziri na watendaji wote wanaohudumu kwenye Wizara hii na taasisi mbalimbali kwa kazi zao nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu kwa kujielekeza kwanza kwenye mawasiliano. Sekta

hii ya mawasiliano kama sitakuwa nimesahau tunao mfuko unaoitwa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, ambao una pesa zake ambazo zimeandaliwa kisheria. Napata mashaka ninaposikia kwamba mfuko huu unashindwa kutekeleza baadhi ya miradi kwa kukosa fedha wakati hawa fedha zao zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Mpango awape fedha hawa *USCAF* ili waweze kufanya kazi. Watu wa *USCAF* wanafanya kazi nzuri sana kwa sababu kwanza kazi zao wanajikita zaidi vijijini ambako kunasemekana huko hakufikiki kibiashara. Sasa kama Serikali ya Awamu ya Tano inasema kwamba ni Serikali ya wananchi wa hali ya chini, basi ni vizuri sana kwenye sekta ya mawasiliano ikawapa fedha mfuko wa *USCAF* ili waweze kutimiza majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano katika Halmashauri yangu ya Wilaya ya Liwale haifikiki kwa barabara, redio au mitandao ya simu. Hivi navyoongea kwenye halmashauri ile kuna Kata za Mpigamiti, Ngongowele, Milui, Lilombe, Mkutano, Mtungunyu, Ndapata na Kimambi ili uweze kupata mawasiliano na ndugu zako ni lazima upande juu ya miti au juu ya vichuguu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linatupa shida sana hata wafanyakazi kama Walimu na watumishi mbalimbali wanashindwa kukaa kwenye maeneo haya kwa sababu ya kukosa mawasiliano. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali iwapatie fedha hawa jamaa wa *USCAF* waweze kutuhudumia ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie kwenye mtandao wa barabara ya Nangurukuru – Liwale. Nashukuru Mheshimiwa Waziri kwa mwaka huu nimeona kwenye vitabu barabara ya Nachingwea - Liwale iko kwenye upembuzi yakinifu na *detailed* design, nashukuru kwa hilo. Nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri barabara ya Nangurukuru - Liwale kwa maana ya Liwale na Mkoa wa Lindi kwa ujumla wake ni barabara ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyoongea pamoja na kwamba zao la korosho limefanya vizuri sana kwenye soko la kimataifa lakini sisi Liwale tunakwama sana, korosho zetu zinakaa ghalani muda mrefu, tunashindwa kufanya minada kwa wakati kwa sababu korosho zetu zinashindwa kutoka Liwale kufika Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri hii barabara siyo tu kwamba ina umuhimu vilevile imeongelewa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi na ni barabara ambayo inarudiwa mara kwa mara. Naomba Mheshimiwa Waziri aitazame barabara hii ya Nangurukuru - Liwale kwa jicho la huruma sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nataka niongelee barabara inayotoka Masasi - Nachingwea – Nanganga. Barabara hii tayari upembuzi yakinifu umekamilika miaka miwili, mitatu ya nyuma iliyopita. Barabara za Masasi - Nachingwea; Nachingwea – Rungwa; Ruangwa – Nanganga; Nanganga - Nachingwea msipoziwekea lami itakuwa ni miujiza kupata lami katika barabara ya Nachingwea - Liwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasisitiza Mheshimiwa Waziri waijenge hii barabara ya Masasi - Nachingwea – Nanganga; Ruangwa - Nachingwea ili nami niweze kupata hii barabara ya Liwale - Nanchingwea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijielekeze kwa upande wa madaraja. Mheshimiwa Waziri atakapokuja mara ya pili ku-*wind up* ajaribu kuniambia. Kuna miradi mingine utakuta daraja linapangwa moja moja lakini madaraja mengine yamewekwa kwenye makundi. Kwa mfano, sisi kwenye halmashauri yetu kuna daraja linalotuunganisha Nachingewa na Liwale la Mbwemkulu, ni daraja refu na kubwa sana na ndiyo kikwazo kikubwa cha kupeleka korosho Nachingwea mpaka Mtwara na sijaliona kwenye vitabu hapa likikumbukwa. Sijui Mheshimiwa Waziri wana mpango gani na hili daraja la Mbwemkulu linalounganisha Nachingwea na Liwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nataka nijielekeze kwenye hizi taasisi zilizoko chini ya Wizara hii, kwa mfano *TTCL.* Tumeamua tuwekeze kwamba *TTCL* ifanye biashara lakini ina madai makubwa sana kutoka kwenye taasisi zingine za Serikali. Naomba TTCL walipwe pesa zao ili tuweze kuwapima utendaji wao baada ya kupata mtaji. Leo hii hatuwezi kuwapima *TTCL* utendaji wao wakati hatujawapa pesa, wanadai pesa zao nyingi taasisi nyingine za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nataka niungane na Mtemi Chenge, anasema ni utaratibu mzuri kuamua kujenga reli ya *standard gauge* lakini ni lazima tutafute fedha au wahisani ili watusaidie *speed* iongezeke na vilevile Serikali iweze kupumua ili sehemu nyingine napo wapate pesa. Maana leo hii kila tukiamka reli, ndege, *as if* hatuna shughuli zingine za kufanya kama Serikali. Naomba Serikali mkope pesa kwa mkopo nafuu au kutafuta wahisani ili reli hii tuijenge kwa *speed* inayotakiwa na Serikali iweze kupumua na kutekeleza miradi mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee Kampuni ya Meli ya Maziwa Makuu. Kama kweli tumeamua kuifufua kampuni hii ni lazima tukubali tuchukue madeni yake Serikali wawalipe wafanyakazi ili tuwape mitaji hawa watu ndiyo tuweze kuwapima. Nashukuru taasisi nyingi kwenye Wizara hii zimepata viongozi wazuri sana ,tena wazalendo na wenye moyo lakini kama hatutawapa pesa za kutosha, hatutaweza kuwahukumu baada ya miaka miwili, mitatu ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze kwenye upande wa bandari. Kuna miradi mingi sana ya bandari imetajwa hapa, lakini nataka niwaambie kwamba sisi zamani Mkoa wa Lindi tulikuwa na Bandari ya Lindi, tulikuwa na meli ya *MV* Lindi. *MV* Lindi na Bandari ya Lindi imekufa na kwenye vitabu vya Mheshimiwa Waziri haipo. Naomba sana Bandari ya Lindi nayo waikumbuke kama ni kuifanyia ukarabati au kuijenga upya lakini sisi kama Lindi tunahitaji bandari...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kuchauka muda wako umemalizika.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Joyce Mukya atafuatiwa na Mheshimiwa Willy Qambalo na Mheshimiwa Hawa Ghasia ajiandae, wote dakika tano, tano.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi, Mawasiliano kwenye bajeti ya mwaka 2018/2019. Nitakuwa na hoja tatu kama muda utatosha, kwa sababu muda ni mchache, naomba nianze moja kwa moja kwenye hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuongelea karakana ya kuhifadhi na kutengeneza ndege ambayo iko katika Uwanja wa Ndege Kilimanjaro. Karakana hii ilinyang'anywa kwa mwekezaji wa *VIA Aviation* ambaye alikuwa anaitwa Susan Mashibe Februari, 2016 ambaye aliambiwa alikuwa anatoa ushuru kidogo. Alikuwa analipa dola 3,000 kwa mwezi na Serikali inasema alikuwa anapata hela nyingi sana lakini alikuwa anatoa ushuru kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niiulize Serikali, mpaka wanakubaliana awe analipa dola 3,000 alijipangia mwenyewe au waliandikishiana mikataba na yule mwekezaji ambaye ni *VIA Aviation* alipe dola hizo kwa mwezi. Kazi hii kaifanya kwa muda wa miaka 10 na yeye kwa sababu alikuwa anajua anatakiwa alipe dola 3,000 kwa mwezi ikabidi awe anatengeneza ndege nyingine ambazo siyo za *ATCL* lakini kwenye mkataba ilikuwa atengeneze ndege za *ATCL.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tunajua kwamba ndege za *ATCL* zimeanza kazi hivi karibuni. Ndege zilikuwa hazifanyi kazi lakini mwekezaji huyu alikuwa anatakiwa alipe dola 3,000 kwa mwezi, je, angefanyaje ili aweze kulipa dola hizo kwa mwezi kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwekezaji yule sasa hivi hana kazi lakini pia Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefungia vile vipuri na ndege za *ATCL* zinatengenezwa nje ya nchi kwa gharama kubwa sana. Vipuri vimefungiwa katika Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro na ndege hazitengenezwi tena katika uwanja huo bali zinapelekwa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, matengenezo madogo madogo ya ndege yafanyike pale katika karakana ya Kilimanjaro yaani Uwanja wa *KIA* kwa sababu kwa kupeleka ndege nje wanapoteza fedha nyingi sana za Tanzania na wakati pale *KIA* kuna karakana ya kutengeneza na kuhifadhi ndege za *ATCL. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelekea *TBA,* wazee wa *expansion joint. TBA* ambao wanahusika zaidi kutafuta viwanja kwa ajili ya Serikali, kujenga nyumba kwa ajili ya watumishi wa umma mbalimbali, wamekuwa wanajenga nyumba hizi lakini hawajui kuzigharamia. Mfano mzuri ni hapa Dodoma katika eneo la *Site One*, Sengia (*Area D),* wamejenga nyumba pale kuanzia mwaka 1994 mpaka leo ni miaka 24, hawajawahi kurudia hata kupaka rangi ya ukuta wa nje achilia mbali kukarabati nyumba moja moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pale unatafuta njia ya kuingilia kwenye *compound*, huoni njia kumejaa majani kila mahali. Mnakaa majumbani mwenu kwenye mikoa yenu lakini mkifika Dodoma kwa ajili ya Kamati na Bunge majani yamejaa kila mahali, eneo ni chafu, hakuna sehemu ya kupita, mkikaa baada ya siku mbili ndiyo hao *TBA* mnaona wanaanza kuja kufanya usafi na kufagia, walikuwa wapi wasifanye usafi wakati nyie hampo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hiyo, nyumba zile ambazo zina vyumba viwili wanalipa Sh.150,000 kwa mwezi, vyumba vitatu ni Sh.250,000 kwa mwezi, hela hizo zinakwenda wapi? Miaka 24 hata kama ni kurudisha gharama wamesharudisha gharama, kwa nini wanajenga majengo lakini hawayafanyii *maintenance? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine, hawa hawa *TBA* wanakwambia wanafanyia marekebisho nyumba za viongozi tu lakini pale Sengia*, Site One* wanakaa viongozi ambao ni Wabunge lakini nyumba zao hazifanyiwi matengenezo, zinafanyiwa matengenezo nyumba za Makatibu Wakuu ambao wanakuja kuhamia Dodoma kwa ajili ya Wizara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaambiwa wewe ambaye unataka kufanya matengenezo kwenye nyumba yako, baada ya kufanya matengenezo aidha uweke *tiles* au ubadilishe choo mkae na *TBA* tena chini mkubaliane gharama mpya ya kodi ya nyumba wakati mpangaji ametengeneza nyumba peke yake na kwa gharama zake. Kama *TBA* wanataka kweli hela kwa nini wasifanye matengenezo wao wenyewe na baada ya hapo wakaongeza hizo gharama za kodi za kila mwezi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo siyo sawa kabisa naomba sana hawa *TBA* wachukue jukumu lao la kujenga nyumba zao, wazifanyie ukarabati, zile nyumba zimechoka na kwao viongozi siyo Wabunge ni Makatibu Wakuu wa Wizara mbalimbali. Naomba sana hawa *TBA* wazifanyie ukarabati zile nyumba kwani zimechoka.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joyce. Tunaendelea na Mheshimiwa Willy Qambalo dakika tano.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nianze kuchangia Wizara hii muhimu kwa ajili

ya maendeleo ya nchi yetu na wananchi wetu na eneo la kuunganisha mikoa yetu kwa barabara za lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni sera ya makusudi iliyokuwa imefikiwa ili makao makuu ya mikoa yote yaweze kuunganishwa kwa barabara za lami. Kamati kwenye hotuba yake imesema vizuri sana iko zaidi ya mikoa 15 ambayo bado haijaunganishwa. Niunganishe kwenye orodha ile Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Manyara haujaunganishwa na Mkoa wa Arusha na Mkoa Mara haujaunganishwa. Malengo ya sera hii ilikuwa ni mwisho iwe 2017/2018, leo tunaingia 2018/2019 karibu robo ya mikoa haijaunganishwa, nadhani tunapaswa kuongeza kasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni ukweli kwamba bado kuna barabara nyingine ndogo ndogo labda ndani ya wilaya, barabara za kwenda hata kwenye vitongoji, hata njia za ng'ombe zinawekwa lami lakini mikoa bado haijaunganishwa. Kama kweli tumedhamiria kuunganisha mikoa hebu tuanze kufanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kuunganisha Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Simiyu ni barabara ya Oldeani *Junction* - Mang'ola - Matala - Mwanhuzi. Barabara inayosemekana ya Karatu - Mbulu – Haydom - Mto Sibiti - Mwanhuzi hiyo ni barabara nyingine na barabara hizi zote mbili zina umuhimu wake tusichanganye. Pale Mang'ola ambako barabara hii inapita kuna gesi muhimu sana ya *helium* ambayo imegundulika, utaisafirisha kwa barabara hii ya Oldeani J*unction* - Mang'ola - Matala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kama ni kweli hiyo reli wanayoisema ya Tanga – Arusha - Musoma itajengwa hiyo ndiyo barabara ya kupitishia vifaa vya ujenzi. Kwa hiyo, barabara ya Oldeani J*unction* - Mang'ola ni barabara muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, pale Mang'ola kila siku inayotoka kwa Mungu kuna tani 150 za vitunguu maji vinasafirishwa kuja Arusha. Kwa hiyo, ni barabara ambayo

naomba isiachwe kwa sababu tu tunasema barabara ni hii ya Karatu – Mbulu – Haydom, hiyo ni barabara nyingine na ni muhimu na kila barabara ina umuhimu wa aina yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye eneo la uwanja wa ndege, nashukuru Benki ya Dunia imeweka hela na naamini itakuja kwa ajili ya upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Lake Manyara. Wananchi wako tayari, miaka miwili imepita Wizara wameshaweka alama za uwanja lakini mpaka sasa hivi wananchi hawajui kinachoendelea. Kwa kuwa fedha zile zimetengwa na nina uhakika ni fedha za uhakika basi waende wakawaambie wananchi juu ya kile ambacho kinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo pia kuhusu Uwanja wa Ndege wa Songwe ni muhimu sana kwa maendeleo ya Nyanda za Juu Kusini. Hata hivyo, uwanja huu haukamiliki zaidi ya miaka 10, kuna tatizo gani? Tumetoka juzi pale Kamati ya Uwekezaji ya Mitaji ya Umma, mambo yanayoendelea kwenye Uwanja wa Ndege wa Songwe ni aibu. Mkandarasi ameshabadilishwa zaidi ya mara tatu, hivi taratibu za manunuzi ya hawa wakandarasi zikoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkandarasi wa kwanza hovyo, wa pili hovyo, wa tatu naye ameshamaliza pesa kazi imesimama, tunawateuaje hawa makandarasi? Mkandarasi wa mwisho huyu Shapriya ameshindwa kumaliza kazi lakini ameshalipwa fedha zaidi ya shilingi bilioni 1.4. Wanawezaje kumpa mkandarasi fedha ambazo siyo za kwake na leo ameshindwa kufanya kazi? Kwenye kitabu wametenga shilingi bilioni tatu ya kwenda Songwe, huyu mtu aliyechukua hii shilingi bilioni 1.4 wana mpango gani naye? Pana shida kubwa sana pale Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo kuhusu reli. Tunashukuru sana, ni mkakati mzuri lakini tusiishie kwenye reli ya kati. Hii reli inayosemwa ya Tanga – Arusha - Musoma imekuwepo tangu mimi niko mtoto wa shule. Kila siku upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na mabilioni yanakwenda. Kuna hiyo reli ya Kusini, yuko mwenzangu amesema kama

inawezekana na kama tuna sifa hebu twendeni tukakope ili hizi reli zote zikajengwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Waziri atusaidie, alikuja mbele ya Bunge hili akasema deni la Taifa limekuwa kubwa kwa sababu pia tunakopa fedha za ujenzi wa reli ya *standard gauge* lakini pia kuna kauli inasema...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Willy.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Tunajenga kwa fedha za ndani, hebu atuambie kauli ya Serikali ni nini juu ya ujenzi wa reli hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Hawa Ghasia dakika 10.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema nami kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili kuweza kuichangia bajeti hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kwa kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano na kumpongeza Waziri pamoja na Manaibu wake na watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kwa kuishukuru Serikali kwa upanuzi wa Bandari ya Mtwara ambao unaendelea vizuri. Ni imani yangu kwamba upanuzi ule utakamilika kwa wakati na hivyo kuwezesha huduma za usafirishaji katika mkoa wetu hasa za zao la korosho kwenda kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niishukuru Wizara hii kwa kuanza upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa

Mtwara. Juzi nimetoka Mtwara nimeona magari pale yapo, nina imani kabisa kwamba kazi ile itaanza kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia katika kitabu cha hotuba na nimeona kazi zitakazofanyika. Napenda kupendekeza kwamba pamoja na kazi walizojiwekea ikiwa ni pamoja na kuweka taa katika uwanja ule, naomba pia suala la kujenga jengo la abiria na lenyewe liwekwe kwa sababu jengo lililopo lipo ndani ya uwanja. Kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Waziri, yeye mwenyewe ameenda na ameona na pia lile jengo lililopo ni dogo na halitoshi kutokana na upanuzi ambao unataka kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda niipongeze Serikali kwa kununua ndege, sasa hivi tuna ndege ya tatu. Nina uhakika kabisa kwamba ufanisi wa Shirika la Ndege la Tanzania utakuwa ni wa kiwango cha juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa masikitiko yangu kwamba Bombadier zilikuwa zinakuja Mtwara lakini sasa hivi huu ni mwezi safari za Mtwara zimefutwa eti kwa sababu Kiwanja cha Ndege cha Songea ni kibovu. Sasa Kiwanja cha Ndege cha Songea kimeanza juzi, Kiwanja cha Ndege cha Mtwara kilikuwepo enzi na enzi na kilikuwa kinafanya kazi bila Kiwanja cha Ndege cha Songea. Sasa kama Kiwanja cha Ndege cha Songea kina matatizo, hakuna sababu yoyote ya kufungia ndege za *ATCL* kwenda Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnasema abiria ni wachache ni kutokana na ratiba zenu ambazo kwa kweli haziwavutii abiria. Mnaunganisha abiria wa Mtwara na Songea. Unaruka Dar es Salaam saa 6.30 unafika Mtwara saa 9.15, zaidi ya saa 2.45 wakati kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam ni dakika 50 kwa Bombadier. Hivi unafikiri kweli utaweza kushindana na *Precision*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida sisi kama ni kuunganishwa, tunaunganishwa na abiria wa Hahaya kule

Comoro kwa sababu kutoka Comoro mpaka Mtwara ni dakika 25 mpaka dakika 30. Kwa hiyo, niwaombe warejeshe ndege Mtwara lakini watuunganishe na Comoro na nawahakikishia watajaza ndege kwa abiria kutoka Mtwara kama watakuwa na ratiba zilizo...

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Mhagama.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mtani wangu Mheshimiwa Hawa Ghasia kwamba Kiwanja cha Ndege cha Songea kimekuwepo kwa kipindi sawa na Kiwanja cha Mtwara na tangu Kampuni ya *ATCL* ilivyoundwa ilikuwa inatua Songea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Ghasia, taarifa hiyo.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huyo ni mtani wangu, kwa hiyo sipendi kubishana na mtani wangu lakini ukweli anaujua na ninaozungumza nao nadhani wananielewa. Isipokuwa tu labda nimsaidie niseme uboreshaji wa Kiwanja cha Songea ufanyike kwa kasi ya hali ya juu ili mtani wangu naye aendelee ku-*enjoy* kwenda na ndege kwa sababu kwa sasa hivi hata wakiturudishia sisi hawezi kupata. Kwa hiyo, uboreshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara uende sambamba na Songea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka nilizungumzie ni suala la uunganishaji wa barabara zetu. Sera ya nchi ni kuunganisha barabara za nchi na nchi, lakini sasa hivi katika Mkoa wa Mtwara tunayo barabara ya kutoka Mtwara - Mozambique kupitia Kilambo ambayo ndiyo barabara inatumiwa na wananchi wengi wanaokwenda Mozambique.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Wizara hii imetuwekea kivuko pale cha kisasa na watu wanatumia sana lakini barabara hii bado haijajengwa kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, niiombe Serikali iijenge barabara ya kutoka Kilambo kwenda Mtwara kwa kiwango cha lami kwa sababu inatuunganisha na majirani zetu wa Mozambique na ni sera ya nchi kuunganisha nchi kwa nchi kwa barabara za lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuiomba Serikali kuharakisha mchakato wa kujenga reli ya kutoka Mtwara kwenda Mbamba Bay na matawi yake yanayokwenda Liganga na Mchuchuma. Upanuzi wa Bandari ya Mtwara kama hakutakuwa na reli itakuwa ni kazi bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mtwara tuna kiwanda kikubwa sana cha Dangote, magari ya kiwanda kile hakuna lililo chini ya tani 30. Sasa hivi zile barabara zetu za udongo ni mahandaki. Ndiyo kusema bila kuwa na reli tunategemea Dangote achukue makaa ya mawe kutoka Ngaka na saruji isafirishwe kupelekwa Songea na mikoa mingine na tuchukue chuma na makaa ya mawe ya Liganga na Mchuchuma kwenda Mtwara bila kuwa na reli barabara zile kwa kweli zitaharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza sana Serikali kwa kuikamilisha barabara ya kutoka Dar es Salaam – Songea. Sasa hivi watani zetu wale wanaoogopa milima wanaitumia sana, mabasi karibu yote ya Songea yanapita barabara ya kutoka Mtwara ya Kilwa Road – Masasi - Tunduru - Ruvuma lakini bila kuwa na reli nina uhakika barabara ile itadumu kwa muda mfupi tu. Sasa hivi kwa ushahidi barabara ya Masasi – Mangaka - Tunduru imeshaanza kuharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe mchakato uharakishwe kuhakikisha kwamba ujenzi wa reli ile unakamilika. Upembuzi yakinifu ulishakamilika, tathmini ya mimea ya maeneo inapopita ilishakamilika na tunachoomba

siyo lazima tutumie pesa za Serikali, tunaweza kujenga barabara ile kwa njia ya *PPP* na njia hii ndiyo itakayotusaidia pia kupunguza deni la Serikali kwa sababu hatutakopa. Tunaweza tukaingia ubia, sisi tukaweka mchango wetu na mwekezaji akaweka mchango wake na bado tukanufaika na matunda ya reli ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimalizie kwa kuipongeza Serikali kwa kuanza ujenzi wa barabara ya kutoka Mtwara – Nanyamba - Tandahimba-Newala - Masasi. Sasa hivi tuko katika kilomita 50, nimeangalia katika kitabu cha bajeti sijaona ile barabara kuongezewa pesa. Mheshimiwa Rais alituahidi kwamba akishinda vipande vilivyobaki atatafuta wakandarasi wengi zaidi ili barabara ile ikamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Profesa Mbarawa asimuangushe Rais wetu, nia yake ni njema kwa wananchi wa Mkoa wa Mtwara na Lindi kwa sababu barabara ile itakwenda mpaka Nachingwea na kutuunganisha pia na mikoa ya jirani zetu, watani zetu Songea, naomba aitekeleze kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Ghasia. Muda wetu kwa mchana huu wa leo umefikia mwisho.

Kabla sijasitisha shughuli za Bunge, naomba niwataje wachangiaji ambao wataanza jioni, ataanza Mheshimiwa Bobali, Mheshimiwa Heche, Mheshimiwa Salome Makamba, Mheshimiwa Hadji Mponda, Mheshimiwa Hassan Masala na Mheshimiwa Josephine Genzabuke.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 Jioni

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge tunaanza na wachangiaji wetu Mheshimiwa Bobali baadaye Mheshimiwa Heche ajiandae.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa mwanzo katika kipindi hiki cha jioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajadili bajeti ya Wizara ambayo inachukua takribani theluthi moja ya bajeti yetu ya nchi. Kwa hiyo, tunavyojadili bajeti ya Wizara hii kwanza ni vizuri ingependeza tukaondoa ushabiki tulionao badala yake tukachukua dhima na kazi yetu kama Bunge ya kuishauri na kuisimamia Serikali kwa sababu ni Wizara ambayo inatengewa fedha nyingi za kodi za walipa kodi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la barabara zetu kujengwa na kuharibika mara kwa mara. Ni jambo la aibu sana kwamba barabara za nchi hii zinapojengwa kila ukifika wakati wa masika zinaharibika, kana kwamba wakandarasi wanaojenga barabara za Tanzania hawajui kama Tanzania inapata mvua kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatia hasira wakati mwingine ukiona kwamba barabara za Tanzania zilizojengwa kwa kiwango cha lami, ukifika wakati wa masika mvua zikinyesha basi zinabadilika na balaa lake katikati ya barabara utakuta madimbwi ya maji, kitu kinachopelekea kuchangia ajali mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi juzi nilikuwa nasafiri natoka Lindi nakuja Dar es Salaam, barabara ambayo imejengwa si zaidi ya miaka sita, miaka mitano iliyopita sasa hivi karibu barabara nzima inahitaji *repair.* Ni barabara ambayo nadhani imejengwa mwishoni kabisa mwa kipindi

cha Rais Kikwete, lakini ukipita sasa hivi ukitembea bila kuwa na tahadhali ni jambo la hatari sana. Sasa nashangaa kwamba tunapojenga barabara zetu hivi hakuna chombo kinachodhibiti ubora wa ujenzi wa barabara hasa hizi barabara za lami?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hakuna chombo nashauri, kwa kuwa tunatumia *bilions of money* kwenye suala la ujenzi wa barabara za lami, nashauri Bunge kama kuna nafasi ya kuunda Kamati Bunge lingeweza kuunda Kamati ya kuchunguza mikataba ya barabara hasa hizi *trunk road* ambazo zimejengwa ni barabara kubwa na zina umuhimu mkubwa katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiingii akilini kuona barabara ya Lindi - Dar es Salam imejengwa juzi, leo hii barabara nzima ina viraka na kwa kweli ni barabara ambayo inatia kichefuchefu kabisa ukiwa unatembea kwenye ile barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni suala la ufufuaji wa shirika la ndege. Tunapaswa tuelewane humu kwamba hakuna mtu ambaye anakataa au anapinga shirika la ndege lisifufuliwe hakuna. Tunachopenda kushauri ni namna na njia inayotumika kulifufua shirika la ndege. Mathalani nyie wote mashahidi na Naibu Mawaziri wapo hapa wanasoma ripoti za *IATA (*Shirika la Ndege la Duniani) mnaona nini kinachoendelea kwenye mashirika ya ndege mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa takwimu zilizopo kwa mwaka mmoja mashirika ya ndege duniani yanapata hasara ya dola za Kimarekani bilioni nane kwa mwaka. Kwa Afrika pekee mwaka uliopita mashirika ya ndege yalipata hasara ya dola milioni 600, kwa Afrika pekee. Sasa ikiwa hali ndio hii tunapokwenda kulifufua shirika letu la ndege lazima tuwe na tahadhari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tahadhari mojawapo wako Wabunge wamechangia hapa walikuwa wanahoji kwamba

hivi inakuwaje tuna ndege ambazo zinasafiri ndani ya nchi tu lakini wateja wetu wako mikoani tuna viwanja vya ndege havina taa, ndege hazitui usiku. Ni kana kwamba wakati tunanunua ndege tulijua labda tutasafiri kwenye viwanja vya kimataifa vya nje ya nchi, lakini najua kusudio la kununua bombadia zitumike ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tumenunua ili zitumike ndani, kwa nini zaidi ya viwanja vya ndege zaidi ya asilimia 70 viwanja vya ndege nchi hii havina taa za usiku. Ndege zinapumzika, Mzee Zungu alikuwa anasema hapa ndege sio chombo kinachohitaji kupumzika, kwamba kimefanya kazi mchana usiku kipumzike hapana ndege zinasafiri wakati wote mchana, asubuhi, jioni, usiku, alfajiri wakati wote na nyie wote mnasafiri ni mashahidi mnajua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inakuwaje ndege za Tanzania zinafanya kazi asubuhi, zinafanya kazi mchana ikifika usiku zinapumzika ni kama mabasi ya abiria vile, kwamba ikifika saa sita usiku basi yaache kusafirisha abiria labda wanaogopa kutekwa mimi sijui. Kama kweli tumekusudia kufufua shirika la ndege, jambo la kwanza lilipaswa kujenga miundombinu, tulitakiwa tujenge miundombinu ambayo itaendana na ufufuaji wa Shirika la Ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitawapeni mfano, wote mnasafiri, ukifika Ethiopia pale Addis Ababa pale *Bole International Airport* jambo la kwanza utakaloliona ule uwanja wa ndege umezungukwa na hoteli kubwa za kifahari. Hii maana yake ni nini? Ni kwamba wanatoa picha kwamba Ethiopia *Airlines* inachangia kwa kiasi kikubwa sana biashara ya utalii na biashara ya hoteli ndio jibu wanalotoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi shirika letu la ndege hatuna hoteli ambazo ni nzuri tumezijenga ama zipo tumezi-*attract,* pia ndege zenyewe zinasafiri kuanzia saa 12 asubuhi mwisho saa 12 jioni maana yake ni kwamba tunatoa huduma kama huduma ya zahanati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukianza kufanya upembuzi yakinifu na tukaondoa ushabiki tukapima tunachokiingiza kwenye shirika letu la ndege tutakuwa tunapata hasara kubwa sana mimi sijawahi kuona shirika la ndege ambalo hili leo tunataka tulifufue, liwe linafanya kazi wakati wa mchana tu, tutapata hasara kubwa sana. Kwa hiyo, lazima tuchukue *precaution* kubwa kwamba kwa kuwa tunetenga pesa nyingi za walipa kodi wa Tanzania, basi haya mengine yaendane ili tuweze kupata faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida ya mashirika ya ndege siku hizi watu hawaangalii tiketi , hawaangalii *collection* ya*transport,*ukiangalia huko hakuna Shirika la Ndege linazalisha pote, hata hiyo unayosikia *Emirate* unasikia Dubai *Air*, unayosikia *Quatar Airlines,* hawaangalii fedha ya tiketi wanaangalia *income* inayopatikana kutokana na sekta zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa kuwa Shirika la Ndege ni *catalyst* ya maendeleo, iwe inachangia maendeleo kwenye sekta ya utalii, iwe inachangia maendeleo kwenye sekta zingine, ndio kinachoangaliwa, huangalii tiketi za ndege, hakuna shirika la ndege linapata faida kwa kuangalia tiketi, hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nizungumzie ni suala la upandishaji wa barabara zetu, mimi nina barabara pale jimboni kwangu, ina miaka kadhaa tunaiombea ipande lakini sijaona hapa inapandishwa. Naomba sana barabara yetu ya Chikonji - Nangalu kwenda Milola ina urefu wa zaidi ya kilometa 100, waipandishe, watu wa *TARURA* hawaiwezi na *nature* ya ile barabara angekuwepo Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa yeye ni shuhuda mkubwa sana kwa sababu wakati mwingine anaitumia kwenda kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *nature* ya ile barabara ni lazima iingie *TANROAD* ndio inawezekana ikafanyiwa marekebisho lakini hivi sasa inafika wakati kwamba tumeitumia *season,* kuna wakati hatuwezi kuitumia

kabisa kwa sababu kuna madaraja makubwa yamekatika na inahitaji ukarabati mkubwa fedha za *TARURA* haiwezi kabisa kujenga ile barabara, kwa hiyo naomba hilo jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nimepitia bajeti ya ukarabati wa hizi barabara za *TANROAD* ukiangalia hii bajeti na nimepitia vizuri sana kwa mikoa, mkoa ambao umepunjwa sana kuliko yoye ni Mkoa wa Tabora na bahati nimewasikia Wabunge wa Tabora wakisemea jambo hili, lakini mkoa uliofuatia ni Mkoa wa Lindi, yaani sisi Lindi tuna kilometa za barabara *TANROAD* kilometa 629 lakini kwa bahati mbaya tumepewa shilingi milioni 800.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo linasikitisha sana kwamba ukiangalia mikoa mingine ambayo wana kilometa 400, wana kilometa 300, wanapewa fedha nyingi, sisi wenye kilometa 600 tunapewa shilingi milioni 800. Jamani mtuangalie na sisi Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo inayosemwa korosho, ufuta inahitaji ipite kwenye barabara, inahitaji isafirishwe. Kwa mazingira haya tuliyonayo hivi sasa maana yake ni kwamba utafika wakati tutashindwa kusafirisha mazao yetu ya biashara na huo uchumi unaosemwa hautaweza kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, ni suala la mitandao, tunao Mfuko wa Mawasiliano, hebu na sisi tuleteeni, nimeona kwenye ripoti yao nimepata angalau vijiji viwili pale jimboni kwangu, lakini uhalisia ni kwamba zaidi ya vijiji 15 vinahitaji kupata minara ambayo itawezesha wananchi kupata mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana waingize kwenye *record* zao Vijiji kama vya Mputwa, Kiwawa, Namkongo, Nyamnyangala, Kijiweni, Mvuleni na Ruvu; hivi vijiji waviingize kwenye orodha ili viweze kupata fedha ya Mfuko huu na sisi tuweze kujengewa minara ili na sisi tuwe tunaishi katika Tanzania hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa Bobali. Tunaendelea na Mheshimiwa Heche na baadaye Mheshimiwa Salome Makamba, dakika tano, tano.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nianze kwa kusema hivi, mwaka jana, mwaka juzi na miaka mingine yote iliyopita tumezungumza hapa kuhusu uwanja wa ndege wa Mkoa wa Mara. Tumesema, tumesema, tumeonesha umuhimu wa huu uwanja ukilinganisha na viwanja vingine ambavyo vimetengewa mabilioni ya pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu uwanja ni muhimu kwa Taifa hili kwa sababu Mbuga ya Serengeti yote unayoijua iko Mkoa wa Mara, ambayo ndio inayoingiza watalii wengi kuliko sehemu nyingine yoyote ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisikia mtu ametoka Ulaya anasema anakwenda Serengeti, mambo ya Ngorongoro na mambo mengine huwa yanafuata baadaye, lakini kichwani kwa watu wanaotoka nje mara nyingi wanasema wanakwenda Serengeti, tumeimba hatusikilizwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ndio mkoa ambao anatoka Mwalimu Nyerere, niliwaambaia hapa wakati fulani, lakini hatusikilizwi. Pesa zinachukuliwa, tena zingine haziko hata kwenye utaratibu wa kibajeti, hazijapitishwa na Bunge hili zinapelekwa kwenye maeneo ambayo hayana muunganiko wa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Mkoa wa Mara ni watu wa misimamo na wanaona mnayoyafanya. Ukichukua barabara za Mkoa wa Mara kwa mfano ukaangalia barabara ya lami tuliyonayo mkoa mzima wa Mara ni barabara inayotoka Mwanza kwenda Sirari, iliyojengwa miaka ya 90 na kitu, hakuna barabara nyingine yoyote ya lami ambayo tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukiwaeleza ni kama wametutupa, lakini mali inayotoka Mkoa wa Mara inachangia pesa nyingi sana kwenye pato la Taifa. Nafikiri ni lazima Mawaziri waangalie haya mambo ya msingi yanayohusu maisha ya watu wa Mkoa wa Mara. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nizungumze kuhusu ufufaji wa *ATCL* na kila mara tunapozungumza hapa watu wanafikiri sisi tunapinga nchi hii kununua ndege. Hakuna mtu miongoni mwetu anayepinga tusinunue ndege, hakuna mtu miongoni mwetu anayekata tusifufue shirika letu la ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosema, kama tulivyosema wakati wa makinikia, kama tulivyozungumza wakati ule walikuja hapa wakatuambia kwamba tunaletewa trilioni 450, tunazisubiri hapa. Tuliwashauri humu, wakatuzomea, tuliwaambia wao ndio walioliingiza Taifa hili kwenye matatizo makubwa ya mikataba mibovu wakasababisha nchi hii inaibiwa na wazungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadaye wakaja hapa wanatunga sheria, tunawashauri njia ya kwenda nayo hawakusikia, wakatubandika majina ooh vibaraka wa wazungu, sijui vibaraka wa mabeberu. Sasa wao wenyewe aibu yao, hakuna pesa hata Sh.100 hata ile ya bia kishika uchumba haijaja ile ya balimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndivyo tunavyowashauri kwenye shirika hili la ndege tunawaeleza kwamba tusiende kununua ndege za nchi hii, mali ya Watanzania wote kama mtu unakwenda kununua machungwa ya nyumbani, kwako bila kushirikisha Bunge, bila kushirikisha bajeti ya Taifa hili, bila kufuata mipango na mikakati ya maendeleo ya nchi hii, hawataki kusikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawaaambia hasara ambazo watasababisha kwa kununua ndege kwenye mashirika tofauti tofauti na utengenezaji wake na *service*

yake itakavyokuwa ngumu, hawataki kusikia. Sasa leo na hapo Waziri atakuja ajibu, hatujui kama ni kwa *mistake* au ni kwa makusudi *ATCL,* ukaguzi wa *CAG* umefanyika lakini *performance* yake haijakaguliwa, *performance audit* haijakaguliwa, tunataka tujue kwamba pesa zilizochukuliwa ni kiasi gani na...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Heche.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Shukrani sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Salome Makamba baadaye Mheshimiwa Haji Mponda ajiandae.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi niweze kuchangia. Mwaka jana tulipitisha bajeti na tukakubaliana kwamba ili tuelekee Serikali ya viwanda, Tanzania ya viwanda, kuna baadhi ya maeneo ni lazima tuyaboreshe. Tukasema tutaboresha reli, tukasema tutaboresha barabara, bandari na maeneo mengi yenye vichocheo vya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Kamati inaonesha kwenye ukurasa wa nne, Serikali haijapeleka bilioni 14 ambazo zilipitishwa kwa ajili ya sekta ya mawasiliano, haijapeleka bilioni sita ambazo tulipitisha kwa ajili ya kuboresha bandari ya Mwanza, hawajapeleka hata senti tano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haijalipa Wakandarasi jambo ambalo limetuingiza kwenye deni la riba ya 3.9 bilioni, pesa hii tulipitisha lakini hazijapelekwa. Leo ni 2018 Watanzania wanaaminishwa tunakwenda kwenye Serikali ya Viwanda ilhali vichocheo ambavyo vinaweza kwenda kuhudumia viwanda kwa kusafirisha malighafi, kwa kuongeza utaalam mpaka leo havijapelekewa senti tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipitisha hapa bilioni mbili ikiwa ni pesa kwa ajili ya *feasibility study* ya uwanja wa ndege wa Chato, *feasibility study,* lakini leo tunaongea Bunge hili halikukaa halikupitisha popote uwanja wa ndege wa Chato umepelekewa bilioni 42 na *completion stage* ya *project* ya uwanja wa ndege wa chato ni zaidi ya asilimia 62, ilipitishwa wapi Bunge halikukaa, hatukuridhia, hakuna utaratibu wowote wa Serikali wa kimanunuzi ambao ulifanyika kupitisha ujenzi wa kiwanja hiki, leo tunacheka tu hapa na Serikali. Serikali inadharau Bunge, hakuna heshima kwa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *CAG* anasema asilimia 35 ya maoni yake aliyoyatoa katika ripoti yake mwaka jana haijafanyiwa kazi, Serikali imepuuza na wala hawaoni umuhimu wa kufanya hivyo, iko kwenye ripoti ya *CAG.* Bunge linalalamika asilimia kubwa ya bajeti yake iliyopitishwa humu Bungeni haijatekelezwa leo tunakaa hapa tunasema tunakaa kuishauri Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulizungumza hapa habari ya *TARURA,* tukasema tatizo la barabara za Wilaya sio chombo cha kutengeneza barabara, changamoto ni pesa katika maeneo haya. *TARURA* leo inatengewa asilimia 30, *TANROAD* inapewa asilimia 70, matokeo yake ni nini? Matokeo yake imeshindwa ku-*perform* kufanya kazi kwa sababu hawajapelekewa pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kahama ninakotoka mimi hakuna barabara inayopitika sasa hivi, ni mafuriko kila mahali, kwa sababu barabara zimeshashindwa kufanyiwa *maintenance,* pesa Serikali inapelekea inapotaka, halafu wanakuja hapa wanajifanya kichwa chini mikono nyuma, eti tuwape bajeti tuwapitishie, hakuna wanachokwenda kufanya ambacho tunashauri hapa Bungeni, wanatekeleza mambo yao wanayoyajua wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawaziri hawa ni Mawaziri welevu sana, yaani mimi leo ningekuwa ni hawa Mawaziri

ningeomba nipumzike, kwa sababu hakuna wanachofanya pale ofisini zaidi ya kutekeleza miradi ya kuletewa na sio miradi ambayo inatokana na michango ya wananchi kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwa sababu tu, sio kwamba hakuna makusanyo, kwa sababu pesa haziendi kwenye miradi. Wanawalazimisha wataalam wetu watafute njia mbadala ya kupata pesa...

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unitunzie muda. Eeh muda wangu umeisha. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hilo la utaratibu, Mheshimiwa Salome ameshamaliza muda wake, hata hivyo tu naomba kuiweka kwenye rekodi kwamba, kwa kweli sio sahihi Mheshimiwa Salome anaposema Mawaziri hao wamekaa hapa wanajitekelezea mambo ambayo wanaletewa tu na kuambiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifuatilia vitabu vyetu vya bajeti na taarifa za miradi ambazo tumeshaziwasilisha mpaka kwenye Kamati hata kama ni fedha kidogo ambayo imekwenda, ni fedha imekwenda katika ile miradi ambayo iko kwenye vitabu vyetu na imeandikwa kwenye vitabu vyetu vya bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala hili la utaratibu, Mheshimiwa Salome ameshamaliza kuzungumza, sina jinsi, lakini naomba tu niseme kwamba...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Ni lazima Mheshimiwa Salome ajue kwamba, asifanye hiyo *generalization* na asitake kutumia tu maneno kwa ajili ya kuchangia Bungeni...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Sisi Mawaziri hapa tunajifanyia tu kazi tu, eti bila kufuata utaratibu wowote ule. Hapana, sio sahihi.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tufuate utaratibu ili twende sawa. Tunaendelea na Mheshimiwa Josephine Genza...

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natakiwa kujibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome muda wako umekwisha? Mheshimiwa Hadji Mponda endelea.

**MHE. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu katika Bajeti hii ya Wizara lakini naomba nianze kutoa shukrani kwa Mwenyezi Mungu aliyenipa afya ya kuniwezesha kutoa mchango katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uungwana hata ukipewa kidogo inabidi ushukuru. Nianze kwa kupongeza Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe

Magufuli kwa kazi nzuri ambayo wanaianza ndani ya miaka miwili na nusu tunaona matokeo na tuna imani dhamira ya Serikali na mwelekeo wa Tanzania ya Viwanda mwaka 2025 tutakuwa tumeifikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Morogoro ni mojawapo ya mikoa miwili ambayo ina eneo kubwa. Mkoa huu wa Morogoro umepakana na Lindi, Pwani, Ruvuma, Iringa, Dodoma, Njombe, Tanga kwa maana tuna kilometa za barabara zipatazo 2,017. Katika kilometa hizo kilometa 538 za lami na kilometa 1497 ni za changarawe na vumbi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia bajeti iliyowekwa ambayo tunaizungumzia naomba kidogo Serikali, Wizara Mheshimiwa Mbarawa na Naibu Waziri wako na watendaji wengine hebu muiangalie kwa kina sana. Mkoa tumeomba ili tuhudumuie barabara hii yenye urefu wa kilometa 2,017 yenye madaraja 938, tumeomba bilioni 61, lakini tulizopewa ni bilioni 21 maana yake ni asilimia 43 tu ya tulichoomba. Nini Tafsiri yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa huu wa Morogoro una mikakati na miradi inayofahamika kuiokoa nchi hii kwenye janga la njaa. Kuna mkakati wa Fanya Mkoa wa Morogoro Kuwa Ghala la Taifa (FAMOGATA). Kuna miradi ambayo inafadhiliwa na marafiki zetu Wamarekani na wadau wengine wa maendeleo mradi wa *SAGCOT* na kuna mradi mwingine *Feed the Future. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii ili iwezeshe nchi hii ijitegemee kwa chakula ni kwamba lazima kuwe na kilimo cha biashara. Sifa ya kilimo cha biashara kuwe na mambo matatu; mosi, kuwa na miundombinu ya uhakika; pili, kuwa na nishati na nishati tayari tunayo na maji, maji tunayo Mkoa wa Morogoro. Tulichopungukiwa ni barabara za uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira yetu ya Mkoa wa Morogoro, hizi kilometa 1,497 zinapita katika maeneo ya

bonde na mvua inanyesha karibu miezi saba. Hali yake ni kwamba itakapokarabatiwa tu baada ya miezi mitatu imeharibika. Sasa nauliza hizi bilioni 21 sijui kama zitatuwezesha na hiyo dhamira ambayo tunakwenda ndani ya Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili nifafanue zaidi nirudi kwenye barabara ambayo tutaizungumzia muda mrefu, barabara ya Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha mpaka Songea. Barabara hii ina kilometa 396, barabara hii inapita katika ardhi kama nilivyosema ni bonde lakini ardhi yenyewe ni tifu tifu, kwa hiyo inahitaji hela ya kutosha. Nimekwenda kwa Mheshimiwa Profesa Mbarawa mara mbili, nimeandika na barua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Engineer* Mfugale, wanamuumiza bure huyu dada *TANROADS Manager* wa Morogoro, *Engineer* Dorothy Ntenga, anajitahidi lakini kwa hicho wanachompelekea wanamuumiza. Nami nimpongeze yeye na kundi lake zima pale *TANROADS* Morogoro wanajitahidi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekwenda ofisi kwa Mhandisi Mfugale zaidi ya mara mbili...

**MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO:** Taarifa.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Nimeandika, nini maana yangu sasa nataka kuelezea hapa?

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Mponda Taarifa. Dkt. Ndumbaro.

**T A A R I F A**

**MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe Taarifa Dkt. Mponda shemeji yangu kwamba barabara hiyo ni muhimu sana ambayo inaunganisha Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Ruvuma na kutokamilika kwake ni madhara kwa mikoa hiyo yote miwili.

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante. Mheshimiwa Dkt. Mponda, Taarifa hiyo?

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea Taarifa yake na ndiyo maana nilikuwa nataka kuishinikiza huko huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ina mambo mawili ambayo inabidi Waziri ayaelewe. Tarehe 5 Septemba, 2015, wakati tunatafuta kutengeneza Serikali, tulimnadi Dkt. John Pombe Magufuli na tulimwambia moja ya shida ya wakazi wa Wilaya ya Malinyi ni miundombinu ya hii barabara. Pale pale alisema nimefanya kwenye hii Wizara, sasa nipeni nafasi kwa nchi nitaweza niikamilishe, maana yake ni kwamba hii ni ahadi ya Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni sera. Sera zinazungumza wazi kuunganisha barabara zinazounganisha mikoa ziwe za lami. Hii barabara ninayozungumzia hawa *TANROADS* wanaijua, inaitwa T16 na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umeshakamilika miaka miwili iliyopita. Sasa inabaki kuanza kujenga hiyo barabara. Habari njema tayari wadau wameshajitokeza, *ADB Bank,* wao wako tayari kufadhili hii barabara. Sasa niwaulize namna gani wataweza kusogeza *speed* maana hii barabara sasa hivi imebaki miaka miwili na Rais hapa ameshaahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mawasiliano. Wilaya ya Malinyi kuna Kata mbili ndani ya Tarafa moja ya Ngoilanga Kata ya Kilosa Mpepo na Kata ya Biro. Kata hizi hazina kabisa mawasiliano. Nimeomba sana, habari njema ni kwamba wameniletea kupitia *UCSAF* ule Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, tumepata minara miwili mmoja Ngoilanga na mwingine Kiswago pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Serikali wamewekeza kila mnara dola la Marekani 30,000, minara hii haifanyi kazi, hii minara ya *Tigo,* tumeeleza mara nyingi hebu tuone hii *value for money,* kwa nini hawa wanatuchezea kiasi hicho mbona

minara yao ambayo haina ufadhili wa Serikali inafanya kazi? Kwa nini hii minara ambayo wanatengeneza *sub-standard? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na minara hiyo lakini bado Kata yangu ya Ngoilanga iko kwenye giza, haina mawasiliano na vilevile Kata ya Biro bado hawana mawasiliano kabisa. Nimwomba Mheshimiwa Waziri, wakati anajumuisha awahakikishie maana ilikuwa ni mojawapo ya ahadi ambayo wameahidi. Mheshimiwa Profesa Mbarawa wewe ni rafiki yangu toka 2015 ulikuwa unasema mimi nitamaliza hii lakini mpaka leo hii hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Wizara wameelezea ujenzi wa vivuko, kuna kivuko pale cha Kikove kinaunganisha Jimbo la Mlimba na Jimbo la Malinyi. Kivuko kile wameweka milioni 400 kwa ajili ya kumalizia ujenzi. Niwaombe, hata wakimalizia ujenzi, kile kivuko bado kuna changamoto, hakuna barabara ya kufika pale kutoka Ngoilanga. Niwaombe, kwenye hii bajeti watafute na mifumo mingine au vyanzo vingine wakimaliza kile kivuko cha Kikove basi ili kitumie barabara ile sasa kutoka kwenye Kijiji cha Ngoilanga iweze kufika pale kwenye kivuko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda, tunaendelea na Mheshimiwa Hassan Masala, baadaye Mheshimiwa Josephine Genzabuke ajiandae.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Ujenzi. Kazi inafanyika na naomba niungane na wenzangu waliotangulia kutoa neno la kushukuru kwa kazi ambazo zinaendelea kufanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo kimsingi ambayo niliomba nichangie ili kuweza kuona namna ambavyo watu wa Wizara ya Ujenzi wanavyoweza

kuendelea kusukuma baadhi ya kazi ambazo tayari zimeshaanza na zimeshaanzishiwa utaratibu wa kukamilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo nataka nilizungumze ni kuhusu suala la barabara ya Masasi kwenda Nachingwea. Barabara hii nikisoma katika ukurasa wa 148 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, wameeleza na wameonesha kiasi cha fedha ambacho wamekitenga jumla ya bilioni tano na hii ni nyongeza ya fedha shilingi bilioni moja na milioni 500 kutoka ile bajeti ambayo wamei-*carry forward* kutoka bajeti ambayo tumeimaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Nachingwea, Masasi na maeneo yote ambayo wananufaika na barabara hii, naomba nitoe neno kwa sababu ni hatua kubwa ambayo kimsingi tumeipigania kwa muda mrefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia iko barabara ambayo inatoka Nanganga kwenda Ruangwa na inaenda kuunganisha na Wilaya ya Nachingwea. Nayo pia nimeona katika ukurasa huo huo wa 148 na ukurasa wa 208 imetengewa shilingi bilioni tano pia kwa maana fedha hii ikipatikana utaratibu wa kuanza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami utafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimeona milioni 800 katika kuanza utaratibu wa kufanya *feasibility study* kutoka Nachingwea kwenda Liwale. Haya yote ni mambo ambayo kimsingi mwanzo hatukuwa nayo, lakini Wizara wameonesha kwamba sasa wanayo nia ya kuanza kufanyia kazi barabara hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kusema hayo, nimwombe sana Mheshimiwa Profesa Mbarawa, nimekuwa na yeye, nimekuwa nafuatilia kwake kwa karibu sana juu ya umuhimu wa kuanza kujengwa kwa hizi barabara. Ni muda mrefu sasa tumeahidiwa kwamba anatafutwa mkandarasi ambaye ataanza kufanya kazi, lakini mpaka sasa

hivi kazi bado haijaanzwa na nimeendelea kufuatilia kupitia Wizarani kuona ni lini kazi hii na fedha hii ambayo tumetengewa itaenda kufanya kazi ili tuweze kutatua changamoto ya barabara ambayo kimsingi tumeipigia kelele kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii pamoja na kwamba ni ya muda mrefu ya kutoka Masasi kwenda Nachingwea barabara hii bado taratibu na *speed* yake kidogo inatutia mashaka sisi ambayo tayari tumeshawaelekeza wananchi wetu kwa majibu ambayo tumepewa kwamba itaanza kujengwa. Kwa hiyo, kupitia hotuba ambayo utakwenda kuhitimisha Mheshimiwa Profesa Mbarawa tunaomba atupe maelezo na haya ni maelezo ambayo wananchi wa Jimbo wanapenda kuyafahamu. Ni lini hii barabara hasa itaanza kwenda kujengwa kwa kiwango cha lami kwa sababu ni ahadi ambayo kimsingi sasa ni kama tayari watu imeshaanza kuwachosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kidogo nipate ufafanuzi kuhusu barabara hii ya Nachingwea kwenda Masasi, ilikuwa inasomeka ni barabara ya Nachingwea - Masasi - Nanganga, lakini nikisoma kwenye hii hotuba barabara hii sasa naona kama kuna kitu kinaondolewa. Jumla ya barabara hii kwa bajeti ya mwaka jana ambayo walitupitishia ilikuwa inasomeka kilometa 91, lakini sasa hivi kuna kilometa 41 ya kutoka Masasi kwenda Nachingwea tu, Nanganga haizungumzwi na sasa hivi tunaizungumza barabara ya kutoka Ruangwa - Nanganga - Nachingwea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii ya katikati sijajua nini kimetokea hapo kwa sababu hii yote ni barabara moja. Ningependa kuwakumbusha watu wa Wizara, kama wamesahau basi ni vizuri tukarekebisha hili jambo kwa sababu tayari linatupa shida kutoa tafsiri sahihi ya barabara hii kama ambavyo tulianza ule mchakato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naomba pia nichukue nafasi hii kuwakumbusha watu wa

Wizara ya Ujenzi, pamoja na kuunganisha hizi barabara ambazo nimezitaja, bado tunaona umuhimu wa kutengenezewa barabara ya kutoka Nachingwea kupitia Ruangwa Mjini kwenda Namichiga kwenda kutokea Kiranjeranje. Barabara hii ina urefu wa takriban kilometa 107.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni muhimu sana, barabara hii ndiyo itakayounganisha watu wanaotoka Tunduru, watapita Masasi, wanakwenda Nachingwea, wanatokea Ruangwa wanaenda kutokea Kiranjeranje, tayari kwa kwenda Dar es Salaam, hakutakuwa na sababu ya kupita Lindi Mjini na maeneo yale ambayo kimsingi tutakuwa tumepunguza umbali mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii sisi katika ngazi ya mkoa tayari tumeshaizungumza na tumeshaipitisha. Kwa hiyo, tunaomba watu wa Wizara katika bajeti yao wakumbuke kwamba kuna hii barabara na bado ni barabara muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingine ambayo ningependa pia kuwaomba watu wa Wizara na Mheshimiwa Kwandikwa tulishazungumza juu ya hii barabara na mwenyewe ameshafika, amefanya ziara katika wilaya yetu ya Nachingwea. Tunayo barabara ya kutoka Nachingwea kwenda Kilimarondo kutokea Lumesule. Kwa ngazi ya Mkoa kupitia *TANROADS* tayari tumeshafanya taratibu zote za kuipandisha hadhi. Tulichokuwa tunaomba katika mipango ya Wizara, barabara hii iingizwe katika utaratibu wa kufanyiwa kazi ili tuweze kufungua mawasiliano kati ya Mkoa wa Lindi na Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo nataka nizungumzie ni eneo la mawasiliano. Mheshimiwa Nditiye nimekwenda sana kwake, lakini pia naomba nimwombe, kazi niliyomfanyia nikiwa Kibondo nami pia naomba alipe fadhila awafanyie kazi watu wa Nachingwea. Tarafa ya Kilimarondo ambayo inajumuisha Kata za Kiegei, Matekwe, Mbondo, hizi kata kwa muda mrefu hazina mawasiliano ya mtandao wa simu, nimeshapeleka haya majina kwako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana ndugu yangu, kaka yangu, watu hawa wameteseka kwa muda mrefu sana wanahitaji mawasiliano. Sasa hivi wanatumia *TTCL* tu na *TTCL* hii toka mwezi wa 12 mpaka sasa hivi mawasiliano bado wananchi wale kule wanatumia *message* tu simu hazitoki. Tunaomba atusaidie katika Mfuko huu wa Fursa sawa wa Mawasiliano, aweze kututengea utaratibu wa kuweza kupata mawasiliano na kampuni nyingine ili tuweze kuwaunganisha hawa watu wa tarafa pamoja na wilaya nzima ya Nachingwea ili tuweze kuboresha uchumi wa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho ambalo ningependa kulizungumzia ni eneo la hawa wenzetu wa *TARURA. TARURA* wamefanya upembuzi yakinifu juu ya ukarabati wa barabara zinazozunguka Jimbo la Nachingwea. Kwa Mwaka wa Fedha uliopita waliomba bajeti ya bilioni moja karibu na milioni 300, lakini fedha ambayo ilitoka ni *almost* bilioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bilioni moja hii, milioni 750 imetumika tu kwa ajili ya kulipa madeni ya Mwaka wa Fedha uliopita. Fedha iliyobaki milioni 300 ndiyo ambayo imetumika kutengeneza barabara na itakayotumika, kitu ambacho bado kwa mtandao wa barabara wa Wilaya ya Nachingwea, fedha hii ni ndogo sana na umuhimu wa Wilaya ya Nachingwea unafahamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nachingwea sasa hivi tunazalisha korosho, ndani ya Mkoa wa Lindi ndiyo tunaongoza, lakini mtandao wa barabara ni mbovu na hauwezi kuhimili taratibu zozote za kuweza kusafirisha mazao kutoka eneo moja kwenda eneo lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo namwomba sana Mheshimiwa Waziri katika utaratibu wa fedha ambao wanaenda kuugawa, katika bajeti ya fedha ambayo wameitoa pamoja na kutoa *ceiling* ya mwaka uliopita, tumeomba jumla ya bilioni tatu, lakini mpaka sasa hivi kiasi

ambacho wame-*approve* bado Wilaya ya Nachingwea hawajatoa hata shilingi moja. Tunashindwa kujua dhamira yao hasa ni nini katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio lazima Wabunge wote tukisimama hapa tuongee kwa kutokwa mapovu, tunaona umuhimu wa kuzungumza kwa lugha laini ili tuweze kuelewana kwamba keki ya Taifa hili tugawane katika misingi ambayo inalingana. Haipendezi kuona maeneo mengine wanapata fedha, barabara zao hazina umuhimu mkubwa sana, lakini maeneo mengine barabara zao hazipati fedha kama ambavyo sisi tumekuwa tunalilia. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atueleze anatupatia shilingi ngapi kwa ajili ya kukarabati barabara ndani ya Jimbo la Nachingwea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hassan Masala. Tunaendelea na Mheshimiwa Josephine Genzabuke, baadaye Mheshimiwa Edwin Sannda na Mheshimiwa Stanslaus Mabula wajiandae.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia rehema za kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naunga mkono hoja. Napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Profesa Mbarawa kwa hotuba yake nzuri. Niwapongeze Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Kwandikwa na kaka yangu Mheshimiwa Nditiye na watendaji wote wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa juhudi zake anazoendelea kuwatumikia Watanzania bila kuchoka. Nafurahi kila ninapomwona anapofanya ziara anapotatua

matatizo ya wanawake wanaokuwa wamemtolea matatizo pale kwenye ziara, anapoyatolea majibu pale pale, kwa kweli huwa nafarajika sana kama mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie Barabara ya Kidawe –Kasulu - Nyakanazi-Kabingo. Sisi watu wa Kigoma ukisimama usizungumzie barabara hiyo unakuwa hujajitendea haki wewe mwenyewe, lakini unakuwa hujawatendea haki wananchi wa Mkoa wa Kigoma. Kwa muda mrefu sana wananchi wa Mkoa wa Kigoma wanapata shida sana, barabara hiyo haipitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kipindi hiki cha mvua mwezi wa Tatu na wa Nne, mvua ilikuwa inanyesha kila siku iendayo kwa Mungu na magari yalikuwa hayapiti, likipita gari moja kubwa likikatisha barabara msururu wa magari kama 20 unafata nyuma akinamama na watoto wanapata shida sana. Ndio maana ninaposimama hapa jioni hii ya leo naomba Serikali iendelee kuweka juhudi za kuhakikisha barabara hiyo inakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nyakanazi- Kabingo mkandarasi alishapewa pesa, lakini hajaweza kumaliza kukamilisha barabara hiyo. Nakumbuka mwaka jana Rais alipokuja Kigoma mkandarasi alileta vifaa vyake vingi vya maonyesho kuonyesha kama yupo kazini, lakini alipoondoka Mheshimiwa Rais zile juhudi zikaishia palepale. Naomba basi kwa vile ameshapewa pesa na pesa yake amekamilishiwa tunaomba barabara hiyo iweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mweyekiti, barabara ya Kidahwe - Kasulu mkandarasi alikuwa hajakamilishiwa malipo yake akawa amesimama kuweza kujenga barabara hiyo, lakini kwa sasa ameanza, naomba naye aendelee kuhimizwa ili aweze kumaliza kazi hiyo na apelekewe pesa kusudi barabara hiyo iweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa mazungumzo ambayo tayari wameshaanza na Benki ya ADB,

naomba juhudi zifanyike. Barabara hiyo inapita katika misitu minene ukizingatia kwamba Mkoa wetu wa Kigoma umekumbwa na wimbi kubwa la wakimbizi. Wakimbizi wanapelekwa katika Mkoa wetu wa Kigoma, sasa usalama ni wa mashaka kwa sababu watu wote ambao sio waadilifu wanaenda kujificha katika misitu hiyo wanafanya ujambazi na ni kwa nini? Kwa sababu barabara ile haipitiki kiurahisi, ndio maana wanapata nafasi ya kwenda kujificha pale kufanya uhalifu. Kwa hiyo, naomba juhudi zifanyike barabara hiyo iweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishukuru kwa pesa ambazo zimetolewa na Falme za Kiarabu. Naomba zile kilometa 51 za kutoka Uvinza mpaka Malagarasi ziweze kufanya kazi zitakapopatikana ili kipande kile kiweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kipo kile kipande cha Chagu mpaka Kazilambwa, nacho naungana na Mheshimiwa Sakaya kipande kile ni kibaya sana. Wananchi wa Mkoa wa Kigoma hawana namna nyingine barabara zinapokuwa zimeharibika napengine inapotokea pengine usafiri wa treni umesitishwa, hakuna barabara nyingine wanayoitumia tofauti na barabara ya kupitia Uvinza - Tabora - Manyoni - Dar es Salaam. Kwa hiyo tunaomba barabara ile na yenyewe ikamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Kigoma - Nyakanazi ndio barabara inayounganisha Mkoa wa Kigoma na mikoa ya jirani, kwa hiyo ni barabara muhimu sana, tunaomba barabara hiyo ikamilishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza juhudi za Serikali kwa kazi kubwa iliyokwishaanza ya *standard gauge.* Naomba isiishie Dodoma tu naomba ifike Tabora hadi Kigoma. Usafiri wa reli ni muhimu sana kwa wananchi wa Mkoa wa Kigoma na maeneo ya Kanda ya Ziwa. Kwa hiyo, tunaomba *standard gauge* napo Kigoma iweze kufika kwa sababu nyie wenyewe humu ndani huwa mnatutania Kigoma mwisho wa reli. Kwa hiyo, tunaomba ianzie kule kule ambako

ndio kuna historia. Reli ikikamilika wananchi watapata nafasi ya kusafiri kwa gharama nafuu na itakuwa ni rahisi kusafirisha mizigo yao kuipeleka sokoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijielekeze kwenye mawasiliano ya mitandao ya simu. Mkoa wa Kigoma umepakana kabisa na nchi jirani za Burundi, DRC na Rwanda na wakati mwingine ukipiga simu kwa watu ambao wapo mipakani wanaitika watu wa nchi jirani. Tunaomba maeneo yale ambayo minara haipo Serikali iweze kufanya mazungumzo na watu wa mashirika wanaopeleka minara ili tuweze kupelekewa minara katika maeneo mbalimbali ili tuweze kupata mawasiliano bila shida yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo kwangu ni hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Josephine, Tunaendelea na Mheshimiwa Mariam Kisangi baadaye Mheshimiwa Stanslaus Mabula na Mheshimiwa Halima Bulembo ajiandaye.

Mheshimiwa Kisangi hayupo, Mheshimiwa Stanslaus Mabula dakika tano na Mheshimiwa Halima Bulembo dakika tano.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kupata muda angalau wa kuchangia nami niseme mambo machache ambayo nadhani yanaweza kutusaidia hasa tunapozungumza juu ya habari ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kwamba Wizara hii haihusiki sana na *TARURA,* lakini fedha zinazotoka katika Mfuko wa Barabara ni sehemu ya fedha zinazokwenda kuimarisha *TARURA* ili iweze kutengeneza miradi mingi zaidi kadri inavyowezekana. Imani yangu ni kwamba fedha hizi ni pamoja na kuhakikisha kwamba tunajenga miradi mingi ya barabara ambayo inapunguza msongamano kwenye miji mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko barabara mbili muhimu sana kwenye Jimbo la Nyamagana, barabara ya kutoka Buhongwa kwenda Igoma na barabara ya kutoka Mkuyuni kupita Nyangerengere kwenda kutokea Mahina na Nyakato Buzuruga. Barabara hizi zikijengwa naamini kwamba *TANROAD* wangeweza sana kufanya kazi hii na *TARURA* sio eneo lake sana kwa sababu ukifikiria Nyamagana tunao mtandao wa barabara kilomita 738, lakini ni kilomita 47 peke yake ndio zimejengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama hatutazingatia msingi huu wa kuona maeneo muhimu tukaimarisha ujenzi wa barabara hizi, hatuwezi kusaidia chochote na badala yake tutakuwa tunaipa *TARURA* mzigo ambao haiwezi kuumudu kwa miaka yote inayokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii sambamba na kwenye Jimbo la Ilemela ipo barabara ya kutoka Nyakato- Buseri - Monze yenye jumla ya kilometa 18. Leo tunakwenda mwaka wa tatu kilometa hizi toka zitengewe fedha imeshajengwa kilometa moja na *point* peke yake, sioni kama tuna dhamira njema ya kusaidia miji hii mikubwa ili iweze kupunguza msongamano na kuifanya ipumue kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda kuzungumza ni juu ya uwanja wa ndege. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, toka tumeanza kuzungumza habari ya uwanja wa ndege wa Mwanza leo ni takribani miaka sita. Hivi malengo na mipango yetu ni ipi? Mimi nafahamu Serikali yenye dhamira ya kukusanya kodi nyingi kama Serikali ya Awamu ya Tano ina kila sababu ya kuimarisha maeneo ambayo ilikwishaanza. Ukiimarisha uwanja wa ndege wa Mwanza kabla hujakimbilia maeneo mengine mengi kwenda kushika huku na kule utakuwa umesaidia zaidi kuhakikisha eneo hili linaimarika kwa nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tuko asilimia 65 tunasema ya ujenzi wa jengo la abiria, ya ujenzi wa jengo la kuongezea ndege, uwanja wa kukimbilia kwa maana uwanja

wa kurukia kwa maana ya *runway,* lakini tunajenga jengo kwa ajili ya mizigo. Hapa tunachokifanya ni sawa na kuvaa suti halafu unavaa kandambili; bila kujenga jengo la abiria hakuna tunachokifanya. Ni agizo la Mheshimiwa Rais viwanja vyote vinavyozunguka maeneo ya ziwa vijengewe *cold room* kubwa ambazo zitasaidia sana viwanja hivi kuwa kwenye maeneo ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko hata suala la ndege, unapozungumza kuimarisha Kiwanja cha Ndege cha Mwanza ndivyo unavyozungumza kuimarisha utalii wa ndani. Hata ndege hizi zinazozungumzwa hapa sana leo kwa hii robo peke yake nilikuwa najaribu kuona zaidi ya abiria 21,000 wamesafiri na ndege hizi ikiwemo Mwanza yenyewe kwa kiwanja chetu hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tafsiri yetu ni nini kukuza na kuendelea kuboresha uwanja wa ndege wa Mwanza itasaidia sana hata pato kubwa zaidi kuongezeka kwenye Serikali. Hata hivyo, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii atakuwa ni shahidi, kwa hii tu robo peke yake abiria hawa waliokuja Mwanza, wameenda Kigoma, wameenda Zanzibar, wameenda Bukoba, wameenda Comoro, wameenda Arusha, ni idadi kubwa sana ambayo inaingizia pato Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mpango wa Serikali ni nini? Niwaombe sana tuboreshe Kiwanja cha Ndege cha Mwanza, kazi tuliyoifanya sasa Mheshimiwa Waziri itabaki kuwa haina maana kama hatutajenga jengo la abiria. Kinachozungumzwa hapa ni mkataba wa mkandarasi kuelekea mwisho, lakini ni bilioni 61 peke yake zimebaki, hebu tutoe hizi fedha tujenge jengo hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Stanslaus.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini tukifanya hivyo tutafanya kazi kubwa, naomba nishukuru na tuone matokeo ya kazi ya Serikali ya Awamu ya Tano. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Halima Bulembo dakika tano.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nijielekeze moja kwa moja kwenye mchango wangu. Leo nilivyokuwa nikijiandaa kuchangia niliona ni vyema kupitia Ilani za Uchaguzi za vyama vitatu vilivyoweka wagombea wa Urais mwaka 2015 ili kuona sintofahamu ambayo imekuwa ikitokea mara kadhaa hasa hasa humu Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho nimekiona ni jambo moja kubwa tu kwamba hatupaswi kushambuliana kwa sababu Mheshimiwa Rais anafanya mambo ambayo hata wapinzani walipaswa kumpongeza. Leo nitatoa mifano kadhaa kudhibitisha hili, naomba mnisikilize kwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa kwanza Shirika la Ndege la Kitaifa; katika Ilani ya Uchaguzi wa CCM aya ya 41 tuliahidi naomba kunukuu

"Katika kipindi cha miaka mitano ijayo Chama cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali kufanya mambo yafuatayo; kuimarisha huduma za Shirika la Ndege la Taifa." mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ilani ya Chama cha UKAWA, ukurasa wa 40 eneo la miundombinu walisema naomba kunukuu:

"Kujenga Shirika la Ndege la Taifa linalojiendesha kwa misingi ya faida." mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ilani ya Uchaguzi ya *ACT* Wazalendo, aya ya 5.23, ukurasa wa 20 waliahidi naomba kunukuu:

"Kuunda upya Shirika la Ndege la Taifa ili iwe chachu ya kuongeza mapato ya fedha za kigeni nchini". Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais amehakikisha anafufua Shirika la *ATCL* kwa kununua ndege sita ili kuongeza njia, kukuza biashara, kupata faida na mapato ya fedha za kigeni. Rais ametekeleza Ilani ya CCM, UKAWA na *ACT* Wazalendo kwa mpigo, haunganishi nchi huyu? Anaunganisha jamani. *(Makofi)*

## TAARIFA

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimwa Mwenyekiti, mfano wa pili, reli...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima subiri kidogo, Mheshimiwa Silinde taarifa.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge anayechangia hapa amezungumza vizuri kabisa kwamba Ilani ya CHADEMA ambao ndio ilikuwa Ilani ya UKAWA imezungumza kuendesha Shirika la Ndege kwa faida, *ni very good note.* Faida ambayo sisi tunaizungumza ni ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaponunua ndege zinapaki, hazifanyi ile kazi yake ambayo inatakiwa kwenda kwenye viwanja mbalimbali yaani kazi ya kusafirisha maana yake ndege inapata hasara. Faida ya ndege inatokana na kusafiri na kukaa angani, sasa nchi yetu ukiangalia tu viwanja vyenye taa tu peke ambayo ndege inaweza kutua masaa 24 viko kama viwanja vitatu tu peke yake. Sasa ndege zetu nyingi tunazozinunua zinabaki eneo moja, kwa hiyo...

**WABUNGE FULANI:** Anachangia huyo.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Nampa taarifa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimwa Mwenyekiti, mfano wa pili ni reli, Ilani ya Uchaguzi wa CCM ukurasa wa 56 tuliahidi naomba kunukuu:

"Kuanza ujenzi wa reli zifuatazo kwa kiwango cha Kimataifa *(standard gauge)* kama ifuatavyo:- Dar es Salaam, Tabora, Kigoma, Mwanza, Uvinza, Msogati, Burundi na Isaka mpaka Kigali Rwanda, Mtwara, Songea, Mbambabay na matawi ya kwenda Mchuchuma na Liganga, Tanga, Arusha, Musoma, Kaliuwa, Mpanda, Kalema".

Ilani ya uchaguzi ya CHADEMA, ukurasa wa 40 waliahidi, nanukuu:

"Kujenga reli mpya kukarabati zilizopo kwa viwango vya kisasa." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais amehakikisha ujenzi wa reli ya kisasa ya kimataifa umeanza. Rais ametekeleza matakwa ya CCM na ya UKAWA, Rais anaunganisha nchi, huu sio muda muafaka wa kumpinga Rais, huu ni muda muafaka wa kumuunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ushauri kwa ndugu zangu wapinzani waibue masuala mapya yale waliyokuwa wakisema kila mwaka tumepata Rais ambaye anayatekeleza. Haitakuwa mbaya wao wakiona wameishiwa hoja wafunge milango, wahamie kwetu, haitakuwa mara ya kwanza wala hakuna atakayewacheka. *(Makofi)*

**TAARIFA**

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1960 waliokuwepo kuna chama kiliitwa *United Tanganyika Party,* kilifunga...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chacha Marwa taarifa, Mheshimiwa Halima Bulembo subiri kidogo nakulindia muda wako.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa msemaji kwamba kwenye Ilani pia ya CCM imeahidi kutoa milioni 50, 50 kila kijiji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima naomba uendelee.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema miaka ya 1960 kuna chama kinaitwa *United* Tanganyika *Party,* waliokuwa enzi hizo watakijua, kilifunga ofisi kikahamia *TANU* kwa kuonekana hawana hoja za msingi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1963 kulikuwa kuna Chama kinaitwa *ANC* cha Zuberi Mtemvu mtakuwa mnakijua miaka hiyo kilifunga ofisi na kuhamia *TANU* kwa kuwa hakikuwa na hoja. Kwa hiyo na wao kama hawana hoja mpya, tunawakaribisha CCM, tujenge nchi na tutawapokea vizuri kwenye Ukumbi wa JK, barabara.

**MBUNGE FULANI:** CCM wenyewe wamekunyagusha.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu anafanya kazi kwa bidii, anajitahidi huu sio muda muafaka wa wao kumbeza, kumdharau, kumdhoofisha badala yake ni kumuunga mkono kwa bidii na Rais anatekeleza matakwa ya Watanzania wote inapokuja suala zima la maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Halima.

**MBUNGE FULANI:** Huna hoja.

**MBUNGE FULANI:** Shemeji umepiga.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Halima kwa mchango wako tunaendelea na...

**MBUNGE FULANI:** Alikuwa hana hela ya maziwa ya mtoto, tunashukuru kwa kumchangia.

**MBUNGE FULANI:** Amewapiga!

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Desderius Mipata, baadaye Mheshimiwa Oran Njeza ajiandae.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, nadhani ninazo dakika kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi pia namshukuru Mwenyezi Mungu kutulindia afya zetu. Natambua sana kazi za Mheshimiwa Rais anazozifanya katika nchi yetu lakini pia natambua kazi nzuri inayofanywa na Wizara. Mheshimiwa Waziri anafanya kazi vizuri Manaibu wake wawili pamoja na watendaji wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mchango kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina shida kubwa sana ya mtandao katika Kata ya Kala na jambo hili nimekuwa nikizungumza zaidi na Mheshimiwa Waziri, vile vile na watendaji. Kata ya Kala ina Vijiji vya King'ombe, Kilambo, Mlambo, Kapumbuli, Mpasa, Lolesha, Tundu pamoja na Kala, vijiji vyote hivi havina mtandao na vijiji viko mpakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiacha tena hiyo kuna vijiji viko Kata ya Sintali, Kijiji cha Kasapa, Kata ya Ninde, Kijiji cha Kisambala na Msamba, lakini vilevile Vijiji vya Nundwe, Mlalambo, havina mtandao, naomba Serikali itupelekee mtandao mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mheshimiwa Waziri atusaidie vilevile barabara. Barabara sasa hivi sisi baada ya *TARURA* kuanza tulikuwa na mategemeo

makubwa sana, lakini bajeti ya mwaka huu ya *TARURA* haipendezi hata kuiona kwa wale ambao wameziona. Unaweza ukaona hata halmashauri wakati fulani waliweza kuchukua hata *own sources* wakafungua barabara zinazojifunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyozungumza hivi barabara zangu kadhaa zimejifunga. Naomba fedha za dharura zipelekwe, ili ziweze kupitika. Kuna Barabara ya Kisura – *Junction* – Malongwe, kuna Barabara ya Nkana – Kala kilometa 68 mabasi hayaendi, Barabara ya Kilambo – Mpasa – *Junction* haipitiki sasa, kuna barabara ya Kitosi – Wampembe, Barabara ya Katongoro - Namasi, barabara zote hizi hazipitiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niishukuru Serikali imetupatia hela kidogo kujenga barabara ya Katali – Miyula ambapo Vijiji vya Katani, Chonga, Makupa, Chelatila na Miyula vitaweza kuunganishwa vizuri na ni eneo la uzalishaji mzuri sana. Naomba Serikali ujenzi uanze mara moja ili kazi iweze kukamilika na wananchi wafaidi matunda ya Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Nkasi Kusini vilevile lina miji midogo iliyoko mwambao wa Ziwa Tanganyika; kuna Mji wa Kala, kuna Mji wa Wampembe. Mji wa Wampembe umeshakuwa mkubwa kiasi kwamba kuna shughuli nyingi za kibiashara na tunaomba tupate bandari, sio gati, tupate bandari Wampembe. Ni muda muafaka sasa, kuna biashara nyingi na ni makutano ya watu wa kutoka nje. Vilevile Kala kuna shughuli nyingi tunaweza tukapata bandari, kama sio bandari, basi tupate gati, itaweza kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona juhudi za Serikali katika kuimarisha usafiri wa majini. Nimeona nia njema ya Serikali ya kuimarisha usafiri wa majini kwani, katika kitabu chake Mheshimiwa Waziri tumeona kwamba, tarehe 18 mwezi huu kuna zabuni ya ununuzi wa meli mpya ya Ziwa Tanganyika imefunguliwa. Kwa hiyo,

naomba mchakato huu uendelee, lakini vilevile nimeona kuna mchakato unaoendelea wa kutengeneza meli ya zamani ya Lihemba, jambo hili ni jema tunalifurahia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, nifurahi kusema kwamba, tumeona juhudi ya kututengenezea uwanja wa ndege wa Sumbawanga ambapo tumetengewa zaidi ya bilioni 12. Hii sio kazi ndogo, kazi inayoenda kufanyika hapa ni fidia, kujenga uwanja pamoja na maeneo ya *parking,* ambapo ukikamilika tutaanza kuona *Bombadier* zinatua sasa. Ambazo sasa ni matunda ya Mheshimiwa Rais na Wanarukwa ambao hatujawahi kufaidi kwa kule, sasa tukitengenezewa huu uwanja wataweza kupata nafasi ya kufaidi na kuziona *Bombadier. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kusema kwamba, pamoja na ujenzi wa barabara ya lami kutoka Sumbawanga kwenda Mpanda kuna vijiji vilirukwa kwa barabara ya zamani iliyokuwa inaenda Mpanda. Kuna Vijiji vya Londokazi mpaka pale Palamayo kuna vijiji vingi hapa katikati, Vijiji kama vitatu vinne vya Mtenga, Mwai, Mashete, ni vijiji vya uzalishaji mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona pia kwenye bajeti hii kuna pesa nyingi inatengwa kwa ajili ya ukarabati wa eneo lile, Serikali ingefikiria eneo hili nalo iwekee lami. Kuna wananchi wa Londokazi waliniambia wanafurahi, tuwaombee kwamba, kwa vile lami imefika Chala ipite tu pale iunganishe, ili wananchi wote wa pale wanaolima mazao ya chakula katika maeneo hayo waweze kupata usafiri wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie kupongeza utekelezaji wa ilani unaofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Rais wetu ni Rais wa Kimataifa kwa msingi kwamba, anazungumzwa ndani ya nchi na nje ya nchi na mikakati yake ni ya kipekee. Yale mambo ambayo yalionekana kushindikana wakati ule ndio hayo yameweza kushamiri na kufanya kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hatushangai wanapompinga kupindukia kwa sababu, hoja zinaendelea kwisha, hawana namna nyingine ya kufanya lazima kupinga. Kwa sababu, kama wewe kazi yako ni kupinga hata jambo zuri utaendelea kupinga tu. Unaweza ukapinga kununua ndege, unaweza kupinga kujenga reli katika *standard gauge,* unaweza ukapinga mambo mazuri yanayofanywa katika nchi hii, jambo ambalo sio zuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja, naomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba, ananipelekea mawasiliano Kata ya Kala na *TARURA* ipewe hela za dharura. Barabara hizo zimejifunga na ni wakulima, hawana namna nyingine ya kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nichangie hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi. Awali ya yote nianze kumpongeza Rais wangu kwa kazi nzuri anayofanya, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Profesa Mbarawa, Mheshimiwa *Engineer* Nditiye, Mheshimiwa Kwandikwa na wataalam wote kwa kazi nzuri wanayofanya kwa sababu, mwenye macho haambiwi tazama. Mheshimiwa Profesa kazi ameiweza pamoja na timu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia, kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wa Wizara zote kwa sababu, sitapata nafasi ya kuwashukuru kwa kazi nzuri wanayofanya na Manaibu wao. Kazi wanayofanya kwa nchi hii wanaitendea haki Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia hoja hii ambayo iko mbele yetu kwa kusema haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote niiombe Wizara ichukue ushauri wa barabara wanazotoa Wabunge kwa sababu, Wabunge ndio wanaotembea kwenye maeneo hayo na ndio wanaoyafanyia kazi. kwa hiyo, la kwangu naomba nichangie kuhusu barabara inayotoka Puge – Ndala – Simbo – Nkinga – Ndembezi – Ziba – Manonga na Shinyanga, sijaona kama imewekewa fedha yoyote kwa ajili ya usanifu, lakini naomba nijenge hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii kuna hospitali kubwa mbili. Kuna Hospitali ya *Ndala Mission,* kuna Hospitali ya Nkinga, lakini azma yetu ni kufungua barabara ya Mkoa na Mkoa, barabara hii inaenda mpaka Shinyanga. Kwa hiyo, ikipatikana nafasi, kwa mwaka huu najua haitawezekana kwa sababu, haimo kwenye vitabu, lakini niombe tu kwamba, kama kutakuwa na uwezekano 2018/2019, namwomba Mheshimiwa Waziri iingie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingine nishukuru kwa ajili ya kuweka upembuzi yakinifu barabara ya Tabora – Mambali – Bukene – Itobo na Kahama. Hii barabara nayo ni kubwa sana, kwa hiyo, nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwamba, ameitengea fedha. Hata hivyo, barabara ya kutoka Tabora – Mambali – Bukumbi – Shitage – Kahama, hii haijaonekana, nimwombe Mheshimiwa Waziri hii barabara nayo aiangalie kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu sana kuongea na Mheshimiwa Kwandikwa, lakini majibu aliyokuwa ananipa naona kama Wizara yake haiitambui barabara hii. Kwa hiyo, niombe nayo pia iangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingine ni barabara ya Sikonge – Ipole – Mpembampazi – Kitunda – Rungwa. Hii barabara ni muhimu sana. Barabara hii akiifungua ikatoka Sikonge, ikapita Ipole, ikaenda Rungwa maana yake inaenda kukutana na barabara ya Itigi

inayokwenda Singida. Kwa utaalam huo pia, barabara hii akiifungua kwa kupitia Sikonge maana yake itaunganisha wageni kutoka Afrika Kusini, itaunganisha usafiri kutoka Malawi ambao wote wanaotaka kwenda Mwanza na kwenda Uganda, hii njia ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingine ambayo naomba niichangie ni ujenzi wa Ipole – Koga. Njia hii inasuasua, ina mkandarasi na mpaka sasa hakuna mawasiliano ya aina yoyote, imekatika kwa ajili ya mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna Barabara nyingine ya Kaliua – Uvinza – Kigoma, sasa hivi hamna kitu kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri anapoiacha hii ya Kaliua maana yake anatenganisha Kigoma na Tabora ambayo ndio njia rahisi ambayo inaweza kuunganisha Watanzania wote kwa kwenda Dar-es-Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo pia, Mheshimiwa Waziri bajeti ya mwaka huu kwa *TANROADS* pamoja na *TARURA* imevurugika. Mwaka huu mvua imenyesha sana, sijui Serikali imejipangaje kwa sababu, fedha iliyomo kwenye vitabu haitoshi na haitatosha. Kwa hiyo, niiombe Serikali itenge fedha ya dharura kwa ajili ya matengenezo ya barabara kwa sababu, mvua hii hatukuitegemea kunyesha kiasi hicho, lakini imenyesha Tanzania nzima na Tanzania nzima kuna mafuriko ya kila aina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe waiangalie *TARURA* na *TANROADS* kwa sababu, *TARURA* pia ingawaje iko chini ya TAMISEMI, lakini haina fedha na kama haina fedha ina maana kwamba, hata *TANROADS* haina fedha. Kwa hiyo, niiombe Serikali iangalie kwa jicho la huruma kwa sababu, tutakuwa tunawalaumu kumbe fedha hazipo kwa hiyo, wapewe fedha ya uhakika, ili waweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uharibifu mkubwa wa barabara, kuna mashimo makubwa ambayo hayazibiki

kwenye barabara kuu. Haya nayo ni matatizo kwa sababu, hata juzi juzi ajali iliyotokea Singida ni madereva walikuwa wanakwepa mashimo. Kwa hiyo, niiombe Serikali iangalie jinsi gani ya kuziba mashimo ambayo ni marefu mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka kuzungumzia kidogo kuhusu ununuzi wa ndege. Ununuzi wa ndege ni jambo zuri, naipongeza sana Serikali yangu na ikiwezekana iongeze tena na tena ili Watanzania tuwe kwenye neema tusiwe tunaziona tu ndege nyingine za *Emirates* zinaleta watalii, basi na za kwetu ziwe na wimbo mmoja, lakini niipongeze Serikali pia kwa *standard gauge* ambayo nina imani itafungua mambo mengi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongelee ukarabati wa majengo ya *TBA* hasa *Site II,* yako katika hali mbaya. Tunakaa kwa kusema hatuna mahali pa kukaa kwa sababu, sisi ni Wabunge, ni wageni, lakini tuko katika hali mbaya. Lingine uchafu uliokithiri. Kuna majumba yale yaliyowekwa sijui ni majumba, sijui manini ya taka, yamejaa mpaka yanatapika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe ushauri. Mitaani tunachangia usafi wa mazingira, kwa nini *TBA* wasijipange wakaleta waraka wa kuchangia angalau Sh.10,000/= kwa kuondoa uchafu wa taka mle? Kwa sababu, tukisema kila kitu bure ndio hayo; nimwombe Mheshimiwa Waziri, atume *delegation* yako ikakague usafi na uchafu uliopo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe tu kwamba, kama atapata muda mzuri ni vizuri watuandikie waraka wapangaji, tuna uwezo ndio maana tukapanga. Kwa hiyo, lazima kuwe na utaratibu wa kuchangia tusifanye bure au kuogopana bure, itatoka wapi hela? Kwa sababu, usafi ni wa kwetu, kodi tunayolipa ni ndogo kiasi ambacho kuchangia Sh.10,000/= hatutashindwa. Kwa hiyo, niombe tuweke utaratibu, tutafute jinsi ya kukusanya angalau Sh.10,000/= kwa kila nyumba tutoe ule uchafu ambao upo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni miundombinu rafiki na maji. Barabara nyingi zinakatwa wakati wa kuingiza maji, hivi hakuna ramani? Inajengwa barabara ya lami kwa gharama kubwa sana, lakini ndani ya mwezi mmoja au miezi miwili miundombinu ya maji inapita pale inakata barabara, hivi sheria hatuna? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanne Mchemba.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka nichangie hayo tu, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono kwa asilimia mia moja bajeti hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea na Mheshimiwa Shekilindi na Mheshimiwa Zacharia Issaay ajiandae.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kunipa uwezo nami niweze kuchangia katika hotuba hii ya Waziri wa Ujenzi na Mawasiliano. Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia uhai na kunipa nguvu niweze kuchangia katika hotuba yako hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Rais wangu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya ambayo imetukuka ambayo haina mfano. Hata hivyo, nataka nimwambie kaza buti, watasema sana na watochonga sana, lakini kaza buti mwendo uwe uleule. Kuna hadithi ya Mtume inasema*:* basi wapendelee wenzako vile vitu ambavyo unavyovipendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija Mathayo 22:34–39 inataja upendo, wapende au mpende jirani yako kama vile unavyoipenda nafsi yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika kwamba, Rais anawapendelea Watanzania kuliko hata familia yake. Huu ni ukweli ambao haujafichika na watu ambao wanabeza basi, ujue hawa wana lao jambo, lakini kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu atamjalia Rais wetu, atamjalia miaka mingi na atatimiza kazi hii na wao watasema baada ya Mheshimiwa Rais kustaafu ndio watajua kwamba, Rais wetu anafanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimshukuru Waziri Mheshimiwa Profesa Mbarawa na timu yake, Naibu Waziri Mheshimiwa Nditiye na Naibu Waziri Mheshimiwa Kwandikwa kwa kazi kubwa wanayoifanya, Mungu atawalipa, sisi hatuna cha kuwalipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika kuchangia sasa. Nimshukuru Rais wangu na niishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inaongozwa na Rais wangu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kunipatia barabara ya lami kilometa moja kila mwaka. Kwa hiyo, nimwombe sasa Waziri Mheshimiwa Profesa Mbarawa, kilometa hii ni chache sana, kwani naamini kabisa inaenda kwa kusuasua, niombe iongezwe hata iwe kilometa mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila ninapopata nafasi naongelea barabara kupandishwa hadhi, barabara ya kutoka Mlalo – Ngwelo – Mlola – Bakanya – Bilingano hadi Mashewa na ikitoka Mashewa inaenda kwa Mheshimiwa Kitandula mpaka Chongoleani Tanga, kule Mabokweni. Barabara hii Waziri Mheshimiwa Profesa Mbarawa aliniahidi kwamba, itapandishwa hadhi mwaka huu na niliongea nae na akajiridhisha kwa Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Tanga akaambiwa kila kitu kiko vizuri. Nashangaa kwenye bajeti hii siioni barabara ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa Mbarawa hebu aniambie, nitumie *style* gani, ili barabara yangu aweze kuipandisha? Watoto wa mjini wanasema nitoke vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana, unaposema barabara ya Lushoto ina maana umesema uchumi wa Lushoto. Barabara hiyo ambayo nimeitaja sasa hivi hata ng'ombe anapita kwa tabu. Nimwombe Mheshimiwa Profesa Mbarawa, niko chini ya miguu yake, naomba barabara hii wakati wa ku-*wind up* basi aipandishe hadhi kwani naamini kabisa hata wananchi wangu wanashindwa kwenda hospitali, akinamama wanajifungulia njiani maana hata gari halipiti wanawabeba kwenye machela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mbogamboga, viazi, matunda, ina maana hayafiki kwa wakati, wakati barabara ile ni barabara ya mkakati, barabara ya kiuchumi. Nilishaongea siku nyingi sana, namwomba Mheshimiwa Profesa Mbarawa asije aukawa masuula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuna barabara ambayo inaanza Dochi kwenda Nguli mpaka Mombo, kilometa 16... *(Makofi)*

**MHE. PASCHAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa subiri kidogo. Mheshimiwa Haonga Taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa Mchangiaji kwamba, aache kumdhalilisha Rais kwa sababu, ametoka kusema kwamba, kuna barabara ambayo hata ng'ombe hapiti, watu hawapiti, lakini mwanzoni alisema kwamba, Rais ni mzalendo anawapenda Watanzania kuliko familia yake, kwa hiyo, aache kumdhalilisha Rais kwenye hotuba yake. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa endelea.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yake siipokei, kwani hajui analolifanya na tabia zake zinajulikana kabisa hapa Bungeni na Tanzania nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Dochi kupitia Ngulwi hadi Mombo, kilometa 16.1 barabara hii Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja, Mheshimiwa Kwandikwa, akashuhudia barabara ile na akaongea na wananchi. Barabara ile ni barabara ya kihistoria, barabara ile ilitumika tangu mkoloni mpaka sasa hivi kuna sehemu inaitwa Kalimasumni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kalimasumni ina maana mababu zetu walikuwa wanabebeshwa mizigo na wazungu kutoka Bondeni Mombo mpaka hapo Kalimasumni sehemu wanaita Ngulwi kwa hiyo, analipwa senti 50 ndio maana panaitwa Kalimasumni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sasa Serikali yangu Tukufu, Mheshimiwa Profesa Mbarawa na timu yake, naomba barabara ile itengenezwe kwa sababu barabara ile ni barabara mbadala. Nimeshaiongelea sana barabara ile kila wakati nachangia. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Profesa Mbarawa sasa, barabara hii naomba kabisa aiweke kwenye mkakati wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitengenezewa barabara mwaka 1984 na *JBG. JBG* baada ya kutengeneza barabara kutoka Mombo mpaka Lushoto kilometa 32, walikabidhi majengo yale kwa halmashauri ya Lushoto, lakini *RRM* wakayachukua majengo yale mpaka sasa hivi majengo yale ni ya *TBA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimwombe Waziri Mheshimiwa Profesa Mbarawa, nimwombe Waziri wangu, chonde-chonde, naomba majengo yale sasa yarudishwe halmashauri, ili tuweze kufungua Chuo cha *VETA* pale kwa sababu, majengo yale tayari yana karakana, yana *garage* na chuo cha seremala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe Waziri wangu Mheshimiwa Profesa Mbarawa atakapohitimisha hoja yake basi, nimwombe karakana ile iweze kurudi halmashauri yetu tuweze kufungua Chuo cha *VETA*, Lushoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara za *TARURA.* Inasikitisha sana, inasikitisha mno unapozungumzia barabara za vijijini ni nyingi mno kiasi kwamba, *TARURA* hata haiwezi. Hebu angalia barabara ambayo nimemwambia, hiyo barabara ya kutoka Dochi – Ngulwi mpaka Mombo, barabara ile tangu mafuriko ya mwezi wa Nne mwaka 1917 haijawahi kupitika, matokeo yake *TARURA* naona wamepanga eti ukarabati sehemu korofi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Profesa Mbarawa, barabara haipitiki halafu inapangiwa pesa eti sehemu korofi, hivi inakuwaje? Basi nimwombe barabara hizi nazo ziweze kupatiwa fedha ziweze kutengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kitandula alisimama akasema kwamba, kuna Kampuni ya Kichina inawekeza kiwanda kikubwa sana ambacho kinatumia trilioni saba, lakini kuna baadhi ya watu au mtu ambaye amekwamisha Wachina wale wasijenge gati maeneo yale ya Mkinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Mheshimiwa Profesa Mbarawa mtu huyu anamfahamu, kama sio mmoja basi ni wengi anawafahamu. Nimwombe atakapo-*wind up* basi mtu huyo ampigie simu awaachie, atoe kibali, ili wananchi wa Mkinga au Mchina yule aweze kujenga gati pale. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Shekilindi. Mheshimiwa Zacharia...

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Zacharia Issaay, baadaye Mheshimiwa Augustino Masele, Mheshimiwa James Millya na Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka, wajiandae.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Basi, naomba nitumie dakika kumi pia. Kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujalia nafasi hii ya uwepo wetu hapa na jinsi ambavyo ametulinda hadi leo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, natoa shukrani za dhati kwa Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kutoka kwake Rais, Makamu wake, Waziri Mkuu na Mawaziri wote kwanza kwa kazi kubwa wanayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitachangia kwa staha sana. Kwanza nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri zaidi ya 14 waliofika Mbulu, lakini walipita katika barabara ya Magara na leo daraja la Magara linajengwa kwa fedha nyingi za Tanzania. Pia barabara zote za *TANROADs;* nawapongeza Watendaji wote wa *TANROADs* kwa jinsi ambavyo wanahangaika katika barabara zetu za Wilaya ya Mbulu, wakati wote kunapitika na wanajitahidi kufanya kazi hii mara mbili kwa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nina maombi Serikalini. La kwanza, naishukuru pia kwa mnara kule Nambisi umefunguliwa, Tarafa ambayo haikuwa na mawasiliano toka zamani na sasa wananchi wa Tarafa hiyo wamepata mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mambo machache. La kwanza, naungana na Waheshimiwa Wabunge wote ambao walikuwa wanatetea fedha za Mfuko wa Barabara, *TARURA* wapewe asilimia 50 na Serikali Kuu 50, vinginevyo basi hata tutafute namna ya vyanzo vingine vya kusaidia *TARURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu barabara zilizopokelewa na *TARURA* zimekuwa na jiografia

ya maeneo magumu sana. Maeneo mengine ni yale yenye makorongo katika maeneo ya vijijini. Kwa mfano, kwenye Jimbo langu la Mbulu Mjini, kuna makorongo ambayo yanahitaji madaraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, korongo moja linaweza kuwa bajeti ya *TARURA* kwa Halmashauri yangu au kwa Jimbo langu la Mbulu Mjini. Sasa hawezi kufanya daraja au kivuko na maeneo hayo yamekuwa kikwazo katika huduma za jamii za afya, elimu na huduma nyingine za kijamii. Kwa hiyo, tunaomba sana, pengine ikiwezekana hata madaraja ya chuma kusaidia kwa namna gani kwa sasa maeneo haya kwa nchi nzima yanapata muunganiko wa kupata mtandao wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua nyingine pia, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kila mwaka ametupa kilomita moja ama mita 500 katika mlima Magara. Waheshimiwa Mawaziri, ni mashahidi waliofika Mbulu, waliopita barabara ya Magara. Barabara ile kwa jiografia haipo Tanzania nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri zile kilomita moja au moja na nusu unayotoa kwa kilomita kama 40 inaweza kuwa takriban miaka kadhaa, wananchi wale wasihudumiwe kwenye hilo eneo. Kwa hiyo, tunaomba kwa bajeti ya mwaka huu kwa fedha walizotenga japo ni kidogo lakini watupe; na mwaka unaofuata watupe hata angalau kilomita tano za mlima ili mlima ule uweze kupitika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom mpaka Sibiti. Majimbo yanayopitiwa na barabara hii ni zaidi ya sita. Tunaomba sana Serikali itusaidie ni kwa namna gani barabara hii inapewa fedha mara moja kwa ajili ya usanifu ulioandikwa kwenye kitabu hiki, lakini na baadaye mpango wake wa kufanyiwa kazi kwa kiwango cha lami. Barabara hii inatoa huduma kwa Majimbo yasiyopungua sita au saba. Pia ina miji midogo takribani kama arobaini na kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Wakurugenzi wa Benki ya Ujerumani walikuwa wanasema barabara hii ni barabara muhimu, inapita kwenye miji mingi na jamii nyingi. Kwa hiyo, tunaomba sana kwa jinsi ambavyo Mheshimiwa Waziri ameandika kwenye kitabu hiki, lakini hakuna fedha zilizowekwa zaidi ya kuwategemea wahisani wa *KfW*. Kwa hiyo, tunaomba ili mtandao wa barabara katika eneo hili la bonde na juu ya Bonde la Ufa kwa maana ya Karatu, Mbulu na Haydom uweze kupatikana kuunganisha mikoa kama mitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naomba sana kama ambavyo nimezungumza, ni ahadi za Mheshimiwa Rais. Tuna miaka mitatu sasa, katika ahadi zile za Mheshimiwa Rais, kwa mtandao wa barabara za *TANROAD* na Serikali Kuu, watusaidie kutekeleza zile ahadi ili ziweze kupungua kwa maeneo yote ya nchi nzima na tunajua ni maeneo makubwa sana ambayo tayari yana matatizo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni eneo la minara. Sasa hivi kuna haja ya Mheshimiwa Waziri kufanya ziara kwa maeneo ambayo hajaenda, lakini pia kuchukua taarifa ya wataalam ambayo inaonesha ni maeneo gani hayana mawasiliano. Juzi Mheshimiwa Waziri alikuwa anatuhoji na kutuambia kila Mbunge yale maeneo ambayo yeye anaona ili alinganishe na yale ya Wizara kama yanafanana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawapongeza sana kwa mpango huu wa kushirikishana mawazo na kupokea mawazo ya Waheshimiwa Wabunge. Hata hivyo, niseme tu kwamba kumekuwa na desturi ya taasisi hizi zinazoweka minara kuweka minara mahali pamoja katika ushindani ule wa kukimbilia eneo moja. Basi Serikali isiwe inaruhusu uwekaji wa hiyo minara kwa maeneo yale. Tunaomba sana katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia barabara za miji Mikuu kama Dodoma. Sisi tunaoishi katika eneo hili la

Mji wa Dodoma kuja Bungeni imekuwa tabu sana na kwenda kwenye maeneo tunayoishi. Tunaomba hata uchongaji wa kawaida wa barabara za changarawe, maeneo yote ambayo hayajafikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hili kwa sababu siku moja nilikuwa nasafiri asubuhi lakini gari lilifunga njia nikawa nimechelewa usafiri ule wa kwenda na Waheshimiwa Wabunge wenzangu. Kwa hiyo, inaonekana kwamba barabara hizi za Dodoma zinahitaji upanuzi wa kina na namna ambavyo uchongaji utawekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili la Dodoma linahitaji sasa ongezeko la alama za wapita kwa miguu. Magari yamekuwa mengi, wapita njia wamekuwa wengi, tumehamia kwenye huu mji kwa wingi wetu. Kwa hiyo, kuna haja ya wataalam kupitia upya mfumo mzima wa barabara za Dodoma ili ziweze kuwekewa alama kwa jinsi itakavyowezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nimwombe sana Mheshimiwa Mbarawa, kama Waziri mwenye dhamana, naomba anisikilize; yeye na Naibu Mawaziri wote, Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii, aje Mbulu apite barabara ya Magara aone jinsi ambavyo barabara hii inahitaji sana jitihada za haraka za Serikali ili iweze kutafutiwa ufumbuzi hasa eneo la Mlima kwa kiwango cha zege kwa sababu ni hatari sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale Mawaziri waliopita kwenye vikao vya Baraza la Mawaziri, wawe Mabalozi wetu wazuri kuizungumzia barabara hii ya Mbulu - Magara hadi Mbuyuni, kwa maana ya barabara ya Magara kwa sababu jiografia yake ni hatarishi na wananchi hawataacha kwa sababu ina ufupi wa kwenda Mkoani Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, eneo hili Mheshimiwa Waziri aji-*commit* wakati anatoa mrejesho wake, atueleze anakuja lini Mbulu ili aone jinsi ambavyo tuna mahitaji makubwa na jiografia yake haipo katika Tanzania

nzima kwa sasa? Japokuwa eneo hili ni eneo fupi, lakini ni tete na hatarishi. Viongozi wote, Mawaziri wote wale 14 waliopita pale walikuwa wanasema Mheshimiwa Mbunge pole sana, kwa kweli hatukujua wakati wote ulikuwa unapiga kelele na kulalamika Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru kwa ujenzi wa daraja na hata kwa hizo kilomita chache wanazoweka Mlimani, ila watuongezee kwenye bajeti, ninyi Mawaziri na Naibu Mawaziri wake wote wawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tunaishukuru sana Serikali na tunawatakia kazi njema. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zacharia Issaay. Tunaendelea na Mheshimiwa Augustino Masele, baadaye Mheshimiwa James Millya, Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka na Mheshimiwa Rukia Kassim, wajiandae.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri ambazo imeendelea kuzifanya. Serikali yetu kupitia Wizara hii imekuwa ikitenda haki. Niseme kabisa kwamba hata katika Wilaya yetu ya Mbogwe *TANROAD* kwa maana ya Mkoa wa Geita chini ya uongozi wa Meneja wa Mkoa, Bwana Haruna Senkuku na Wasaidizi wake wamefanya kazi nzuri sana katika kuhakikisha kwamba Wilaya yetu mpya ya Mbogwe inapata barabara za Mkoa na kuifungua katika upya wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo hiyo barabara kutoka Butengoromasa kupita Iparamasa - Mbogwe mpaka Masumbwe. Barabara hii tumeomba ikapandishwa hadhi na zaidi sana tunaomba Wizara iendelee na mchakato wa

kuweza kuifanyia usanifu wa kina na upembuzi yakinifu ili kusudi ikiwezekana iweze kujengwa kwa kiwango cha lami ili kuweza kufungua mawasiliano ya muda wote wakati wa masika na wakati wa kiangazi, barabara hii iweze kupitika kwa urahisi na kuweza kuleta maendeleo kwa wananchi wa Wilaya ya Mbogwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisemee pia kuhusu barabara iliyopandishwa hadhi ya kutokea Ushirombo kwenda Makao Makuu ya Wilaya ya Mbogwe kuelekea Mkoani Geita. Hapa namwomba Mheshimiwa Waziri atusikilize vizuri kwa maana ya kwamba barabara hii tulikuwa tumeomba ichukuliwe na *TANROAD* kutoka Ushirombo kupita Bwera kwenda mpaka Wigo ambapo barabara hii inakutana na barabara ya kutoka Kahama kwenda Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, *TANROAD* wamechukua sehemu ya barabara hii. Sasa nikaiomba Wizara, kwa nini isitusaidie kuchukua tena hiki kipande cha kutokea Iboya kwenda Wigo ili kusudi barabara hii iwawezeshe Wanambogwe kwenda Mkoani Geita Makao Makuu ya Mkoa wetu wa Geita?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tu Mheshimiwa Waziri atumie wataalam wake waende kukagua hii barabara, ikiwezekana basi ikamilishwe kwa sababu imechukuliwa kipande kwa kupitia Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Geita. Tulikuwa tumeomba hii barabara ipandishwe lakini Wizara kwa busara zao wamechukua nusu. Tunaomba tu Wizara ichukue hatua za ziada ili kuweza kuikamilisha hii barabara, itakuwa imefanya jambo la msingi sana.

Mheshimwi Mwenyekiti, naomba pia Wizara itutazame tena kwa upya ili Mkoa wetu wa Geita uweze kuunganishwa na Mkoa wa Tabora kupitia Wilaya ya jirani kwetu kwa ndugu yangu, Mheshimiwa Elias Kwandikwa. Huyu ni jirani yangu na naomba sasa kwa kweli waangalie uwezekano wa kutupandishia hii barabara kutoka

Masumbwe kupitia Ushetu kwenda Kaliua mpaka Urambo. Hii barabara itatusaidia sana Wana-Geita kuweza kuunganishwa na Mkoa wa Tabora na Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naamini kabisa kwamba kwa uangalizi mzuri wa Mheshimiwa Profesa Mbarawa, barabara hii itapandishwa na itatusaidia sana katika kuhakikisha kwamba Mkoa wetu Mpya wa Geita na wenyewe unaenda kwa kasi katika nchi yetu hii ambayo tunaitarajia kuwa nchi ya viwanda katika muda mchache ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tena kuhusiana wa ukurasa wa 33 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Kuna utaratibu wa kujenga daraja la Busisi Kigongo. Daraja hili liko katika barabara ya Geita Usagara. Daraja hili kwa kweli endapo Serikali itafanikiwa kulikamilisha, naamini kwamba barabara hii ya kutoka Geita - Kagera mpaka Musoma Mkoani Mara, itakuwa ni ufumbuzi mkubwa sana katika suala zima katika ukuzaji wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwamba daraja hili endapo Mungu akitujalia likakamilika litakuwa ni sehemu ya Utalii, maana ni sehemu ambayo kwa kweli kimsingi ujenzi ukikamilika litakuwa ni la aina yake, kama ambavyo sasa hivi kuna daraja hilo la Kigamboni, hata hili la Kilombero pamoja na daraja la Mkapa, yamekuwa ni madaraja ambayo ni ya mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu wazi kwamba habari ya Wizara hii siyo ya kubahatisha. Kikwetu huwa tunasema hii ni Wizara ya *mashikolomageni*. Hii Wizara ni ya vitu vipya. Wizara hii imekuwa ikituletea *flyovers,* madaraja ambayo hayajawahi kuonekana katika Afrika Mashariki na Kati. Kwa hiyo, nawaombea Mungu aendelee kuwapa ujasiri, waendelee mbele, watutendee haki kwa kututoa kimasomaso.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za nyuma tulikuwa tunaonekana kama watoto yatima, nchi kubwa kama

Tanzania inakosa ndege. Kwa maana hiyo, kwa kweli tulikuwa tunadhalilika, wakati mwingine tunapita nchi jirani ya Kenya kwenda Dar es Salaam. Unatoka Mwanza unakwenda Nairobi, halafu ndiyo unakwenda kuzunguka kwenda Dar es Salaam. Ilikuwa ni aibu kubwa. Kutokana na ujasiri wa Wizara hii pamoja na wakala mbalimbali akiwemo Bwana Mfugale, Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema jambo hili kwa nia njema kabisa na ninaamini kila Mtanzania mwenye nia njema atawaombeeni kwa Mungu ili kusudi kwa kweli wapate thawabu hata siku ya mwisho, maana wanatuletea mambo mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala zima la ujenzi wa reli ya *standard gauge*. Hatua iliyofikiwa na Serikali ni nzuri na niseme tu kwamba hata ile reli ya kutokea Isaka kwenda Kigali Rwanda mpaka Msongati, naomba Mheshimiwa Waziri wetu aiangalie reli hiyo na yenyewe iweze kuchukuliwa hatua tuone mwelekeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunayo reli ya kutokea Dar es Salaam mpaka Arusha pamoja na Mkoani Mara, Serikali ilione hilo ili nchi yetu iweze kupiga hatua kwa hatua, kwa maana kwamba kuwe na *balance* ya maendeleo sehemu katika mbalimbali za nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI.** Ahsante sana Mheshimiwa Masele. Tunaendelea na Mheshimiwa James Millya, baadaye Mheshimiwa James Millya, Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka na Mheshimiwa Mussa Mbarouk ajiandae.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ukurasa wa 34 wa kitabu hiki utaona kuna barabara ya Arusha – Orkesumet - Kibaya mpaka Kongwa. Wakati upembuzi yakinifu na usanifu wa kina unafanyika kwenye barabara ile, inapita Wilaya ya Simanjiro, lakini walipofika

kwenye Kijiji cha Nadonjukin wataalam wanatoa sababu ya kupindisha barabara ile isipite Terrat kuelekea Orkesmet wakidai kwamba kuna wanyamapori wanaopita kwenye ile barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukijaribu kuangalia kwenye nchi yetu barabara ya Morogoro –Mikumi – Ilula – Iringa, pale katikati panapita wanyamapori. Pia barabara ya kutoka Minjingu kwenda Babati, kuna Mbuga ya Tarangire na Manyara katikati. Kimataifa, kuna barabara ya *Kruger Park* inayopita katikati ya *National Park* ya Afrika Kusini ya *Kruger National Park*. Barabara hizi zote zinapita katikati ya Mbuga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa *TANROAD* wanapitisha barabara ile wakiiacha Simanjiro yenye vijiji vya Terrat, Sukro, Narkawo, Loiborsiret. Huu ni uonevu na ubaguzi wa hali ya juu. Naiomba Wizara, Mheshimiwa Waziri kwa kitabu chake hiki, ajaribu kuangalia upya kwamba lazima barabara ile ipitike. Tunavyosema nyumbu anapita kwa miezi mingapi; wanakuja mwezi wa Tatu tu kuzaliana pale. Kwa hiyo, naomba ubaguzi huu usifanyike hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Manyara tangu barabara zake zipandishwe hadhi, mara ya mwisho ni mwaka 2009. Kuna barabara ya kutoka Msitu wa Tembo kwenda Korongo kuelekea mpaka Vijiji vya Nyumba ya Mungu mpaka Ngage. Barabara hizi kwa fedha za ndani za Halmashauri na *TARURA* haiwezi kuhudumia barabara hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wajaribu kuangalia namna gani Mheshimiwa Waziri apandishe hadhi barabara zetu ili *TANROADS* waangalie barabara hiyo yote inaenda mpaka *Ruvu-Remit*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye *ATCL*. Kwenye ripoti ya Ofisi ya Msajili wa Hazina ukurasa wa nne, Afisa huyu anasema *ATCL* hesabu zake hazijawahi kukaguliwa kwa muda mrefu sana, lakini sababu hiyo hiyo ndiyo inatupelekea sisi tuseme kwamba inawezekana *one point five trillion*

ambayo haionekani kwenye Hazina ya Serikali, inawezekana imetumika kwa sababu ya kutokagua mahesabu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda muafaka, wale wanaomshauri Mheshimiwa Rais, washauri vizuri. Mheshimiwa Magufuli hatadumu milele, ataondoka kwenye madaraka. Ninyi ambao hamumwelekezi kwamba anakosea saa nyingine, kama yeye ndio kachukua hizo fedha, ni muhimu ndugu zangu mumshauri vizuri. Fedha za umma ni za umma na mtu huwezi kuzichukua kama unavyotaka fedha zako za mfukoni. Kuna taratibu za kuchukua fedha hizi. Ni vizuri mshauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wanafanya hivyo Waheshimiwa Mawaziri, wakumbuke kwamba akina Yona walikuwa Mawaziri, wakumbuke kwamba akina Mramba walikuwa Mawaziri iko siku Watanzania watakuja kuwaulizeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nafanya Mahakama ya Kimataifa, Rwanda, watu waliokuwa wakimzunguka Rais Habyarimana mwaka 1994, walimshauri vibaya na ndiyo maana mauaji ya Kimbari ya Rwanda ya mwaka 1994 yakatokea. Nawaomba Waheshimiwa Mawaziri, watu wa karibu walioko karibu na Mheshimiwa Rais, washauri Mheshimiwa Rais kwamba nchi hii ni nchi yenye sheria, haiwezekani ukaweza kuchukua fedha zote kutoka kwenye Hazina ya Taifa ukapeleka mahali ambapo hazionekani. Ni muhimu ufuate sheria ili nchi hii iweze kuwaheshimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi...

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu Mheshimiwa Millya, naomba subiri kidogo.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Millya amevunja kanuni ya 64(1)(a) na (b) kwamba hatatumia jina la Rais kwa lengo la kulishawishi Bunge kufanya maamuzi yoyote yale. Asome mpaka kipengele cha (e) ataelewa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge anayezungumza amejaribu kutumia jina la Rais na kutaka kutoa ushauri kwa ...

**T A A R I F A**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, taarifa moja, moja, taarifa.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yeye ni utaratibu ana....

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Wewe unanipaje taarifa wakati naongea kuhusu utaratibu?

**MWENYEKITI:** Basi mseme mmoja mmoja, hatuwezi kusema wawili wawili.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini amekosea. Haja-*quote*. Anachoki-*quote* sicho. 64 (a) na (b) havihusiani na Rais.

**MWENYEKITI:** Sijakupa ruhusa Mheshimiwa Susan.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Ni 64 (1) kanuni ya (e) nimesema asome (a), (b) mpaka (e).

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa umeeleweka.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dada Susan namheshimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachojaribu kusema ni kwamba mzungumzaji aliyekaa anajaribu kutumia fursa inayotolewa na Ibara ya 100 ya Katiba kutu-*convince*

Wabunge kwa kutumia jina la Rais tufanye maamuzi ya kumshauri Rais vinginevyo. Naomba atumie kanuni vizuri, atumie fursa inayotolewa na Katiba yetu ya kusema ndani ya Bunge hili vizuri, bila kukejeli wala kutumia lugha ambazo wengine zinatukera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana ajielekeze kwenye hoja.

**MBUNGE FULANI:** Kaa chini!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Millya, endelea kuchangia bila kutumia jina la Mheshiiwa Rais kwa namna ambayo siyo sahihi.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabila la Kimasai kati ya vitu ambavyo hatuwezi ni unafiki. Najaribu kushawishi kwa nia njema kwamba inawezekana hawa ambao wako madarakani sasa, kama hawamshauri vizuri Rais, nitoe mfano mmoja; *Police Ordinance, Political Parties Act, The Constitution* haimpi mamlaka Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kukataza mikutano ya hadhara na hawa ambao wako karibu naye wanamnyima fursa ya kumshauri vizuri. Hivyo, ni vyema waliomzunguka Mheshimiwa Rais wakamshauri vizuri. *(Makofi)*

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Millya, naomba utulie.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunarudi tu kwenye hiyo kanuni ya utaratibu, kanuni ya (64)(1)(e). Vilevile naomba sasa niongeze na kifungu kidogo cha (a); haya yote mawili. Kwanza ni hilo ambalo tunalisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika michango yetu humu ndani, ili hoja yako ipate uzito tunakatazwa na kifungu cha kanuni cha (e) kutokum-*implicate* Rais ili hoja yako eti ionekane ndiyo ina uzito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Mheshimiwa Mbunge anasema kwamba Mheshimiwa Rais amekataza mikutano ya hadhara.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mmoja mmoja. Mheshimiwa Waziri, endelea.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64 (1)(a) inamtaka Mbunge asiseme uwongo. Ni wapi Mheshimiwa Rais alisimama hadharani akasema mikutano ya hadhara ya vyama haipo?

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua...

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa mtu mmoja mara moja. Hatuwezi kusema watu wote. Mheshimiwa endelea.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Vyama vya Siasa iko wazi na inakitaka chama kinapotaka kufanya mkutano wa hadhara kitoe taarifa Polisi na Polisi watakuwa na mamlaka ya kutoa kibali kwenye mikutano ya vyama.

**MBUNGE FULANI:** Mwenyekiti, taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU):** Kwa hiyo, wote tunajua Wabunge, Madiwani wote wameruhusiwa kuendelea na mikutano katika maeneo yao. Kwa hiyo, ni lazima utaratibu wa kikanuni ufuatwe ndani ya Bunge lako Tukufu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge!

Mheshimiwa Millya naomba umalizie tafadhali.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu waliokaa upande wa pili ambao kwa muda mrefu nimekaa na ninyi CCM, saa nyingine muwe mnakumbuka Kanuni ya 64 hiyo hiyo, mnapojaribu kushawishi Bunge kwa kumsifia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa moyo wa dhati na ninyi ndio mtakaokaa upande wa pili kumpiga mawe baadaye Watanzania wakianza kuuliza maswali. Sisi wengine tuko upande huu... *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umemalizika Mheshimiwa Millya.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka. Hayupo!

**MBUNGE FULANI:** Yupo.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwa vile nina dakika tano tu, naomba niende *straight* kwenye *points* zangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme ukweli kwamba namheshimu sana Waziri Mheshimiwa Profesa Mbarawa, Waziri wa Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Naomba tu kuongezea *facts* ambazo alitoa Mheshimiwa Kitandula, Mbunge wa Mkinga alipoanza kuzungumzia juu ya barabara ya Same – Kisiwani - Mkomazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Mbarawa ajue kwamba barabara hii ina umuhimu wa kipekee. Kwanza ilikuwa barabara ambayo iko kwenye *Great North Road* ikafanyiwa magumashi ikabadilishwa kwa sababu ambazo sitazitaja hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande huu wa Same Mashariki una hazina kubwa sana ya utajiri mkubwa sana wa maji, mvua, mazao na barabara hii inatumiwa na wakazi wa Korogwe Vijijini akiwepo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali anakaa sehemu hiyo; inatumiwa na wenzetu Jimbo la Mkinga aliko Mheshimiwa Kitandula; inatumiwa na wakazi wa Mlalo, Jimbo la Mheshimiwa Shangazi; inatumiwa na Same Magharibi kwa Mheshimiwa Mathayo; na inatumiwa na Same Mashariki kwa Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa haya yote Mheshimiwa Waziri ajue ana *National Park* ambayo Faru mweusi alitolewa kutoka *Czech* akaletwa akawekwa pale Mkomazi *National Park* ili watu wengi waweze kwenda kumwona. Akumbuke kwamba kuna mradi mkubwa unajengwa na *LAPF* ambapo tangawizi yake itatoka kwenye haya Majimbo yote ya hawa Waheshimiwa niliowataja. Akumbuke kwamba nilishasema hapa na Mheshimiwa Spika

aka-*join* akisema katika Mkoa wa Kilimanjaro ni Jimbo la Same Mashariki tu ambalo halina barabara ya lami iliyokamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi mkubwa ambao *UNCDF - Capital Development Fund* wanakuja kuwekeza katika kupandikiza samaki ambapo kuna bwawa ambalo lilitengenezwa tangu Wakoloni walipohamisha wananchi kutoka Mkomazi *National Park,* wakawatengenezea hili bwawa ambalo lina ukubwa wa *24 square kilometers*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *UN Secretary General* anaye-*deal* na *UNCDF Deputy* ali-*fly* kutoka *New York* alikuja *KIA* kuangalia sehemu ule mradi utakapowekwa, akatia *tick.* Akasema huu utakuwa ni mradi mzuri sana ambao utapandikiza samaki wa kisasa kutoka *South America* ambao wataweza kuwa ndio kitovu cha kusaidia Tanzania kupata samaki wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo mafupi namwomba Profesa Mbarawa, ametengea Jimbo hili au barabara hii Sh.265,000,000 kwa kilomita 96.5, lakini hapo hapo upembuzi yakinifu uliofanywa mwaka 2015/2016 ulitumia Sh.595,000,000 kufanya huu upembuzi yakinifu. Mwaka 2016/2017 ulishafanywa tena upembuzi yakinifu; Mwaka 2017/2018 nimeambiwa juzi na Meneja wa *TANROADS* kwamba pia walipita kufanya upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikuwa napiga kelele hapa kwa ajili ya barabara hii nikijua Mheshimiwa Mbarawa anajua umuhimu wa hii barabara ndiyo maana mara tatu unafanyiwa upembuzi yakinifu, ambapo najua gharama zake zitakuwa imefika shilingi bilioni moja. Sasa kama anafanyia barabara, upembuzi yakinifu na upembuzi wa kina kwa kutumia zaidi ya shilingi bilioni moja, lakini atoe shilingi milioni 200 na kitu, kweli hii?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kaboyoka. Tunaendelea na Mheshimiwa Mussa Mbarouk dakika 10 na baadaye Mheshimiwa Devotha Minja na Mheshimiwa Joseph Haule wajiandae kwa dakika tano tano.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nashukuru kwa Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema katika kuchangia bajeti ya Wizara hii ambayo ni muhimu katika maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, niseme tu kwamba kwa ufahamu wangu, Bunge siyo *rubber stamp,* ni kwamba kinacholetwa hapa kinatakiwa kijadiliwe halafu tukubaliane kwa pamoja. Kazi ya Bunge ni kuisimamia Serikali. Sasa siyo lazima kila kinacholetwa hapa tuunge mkono hoja tu, hapana. Wakati mwingine kama kuna marekebisho, lazima yafanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, niseme tu, jana kuna mchangiaji mmoja hapa alitoa taarifa kidogo ambayo nami naungana naye. Kama sikosei alikuwa ni Mheshimiwa Silinde. Alizungumza akasema kwamba kuna barabara hewa ambazo zimetumia shilingi bilioni 252, lakini barabara hizi hazijulikani zimejengwa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa, tupate maelezo ya shilingi bilioni 252 barabara zake zimejengwa wapi? Kama hilo halitoshi, nami ni Mjumbe pia wa *PAC,* tutakuja kuangalia huko katika vitabu tuone hiyo *value for money*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine imezungumzwa pia kwamba tunaboresha Shirika la Ndege, lakini ili lifanye kazi vizuri, lazima liwe na *routes,* lisafiri sehemu mbalimbali, ndani na nje ya nchi. Sasa hapa naiomba Serikali kwamba pamoja na kwamba tunanunua ndege, lakini tujitayarishe katika kushindana na mashirika mengine makubwa ya ndege ili ndege hizi zisije zikaitia hasara Serikali kwa sababu Watanzania wana matatizo mengi sana, lakini

hatukuyaangalia hayo, tumeona kwanza tuanze na ndege. Hilo pia bado taarifa ya *CAG* haipo na hii taarifa ya Shirika la *ATCL* hailetwi Bungeni kujadiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo nianze kuchangia mchango wangu. Nataka kuizungumzia kwanza barabara ya Pangani. Kwa maoni yangu ni kama barabara ya Pangani ni mfupa uliomshinda fisi. Kwa nini nasema hivyo? Hii barabara imepita Marais wanne. Ameanza Mwalimu Nyerere akaweka ahadi; akaja Mheshimiwa Rais Mwinyi, akaweka ahadi, akaja Mheshimiwa Mkapa akaweka ahadi, amekuja Mheshimiwa Kikwete naye ameweka ahadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbarawa namheshimu sana pamoja na wasaidizi wake, lakini mwaka 2017 walituambia kwenye bajeti kwamba wametenga shilingi bilioni nne kwa ajili ya upembuzi yakinifu *(feasibility study)* na mambo mengine. Asubuhi pia nilimpelekea ki-*memo* kutaka kujua ufafanuzi, hii inayozungumziwa katika ukurasa 271 ndiyo hiyo barabara ya Pangani? Naona ile pesa imepungua! Sasa kila siku gharama za ujenzi zinakwenda mbele lakini bajeti ya barabara ya Pangani inapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja anijuze na anishibishe ili nitakaporudi Tanga niwaambie watu wa Tanga kwamba safari hii barabara ya Pangani itajengwa au haijengwi? Kwa sababu tumechoka na ahadi zisizotekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amekuja Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, hata alipokuja kufanya ziara Tanga ya kuweka jiwe la msingi la bomba la mafuta nilimgusia suala hili na akaahidi kama ataijenga, lakini kwenye bajeti siioni. Sasa Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa aniambie hii barabara itajengwa au haitajengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namkumbusha kwamba barabara hii ina Wabunge wanne au watano; imeanza Tanga Mjini, inapita sehemu ya Kigombe ambayo ni Muheza kwa Mheshimiwa Adadi Rajabu, inaingia Pangani kwa

Mheshimiwa Juma Aweso, lakini inaingia vilevile Chalinze kwa Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete. Kwa hiyo, Wabunge watano wote tumekuwa tukiizungumzia hii barabara, lakini inaonekana kama tunatwanga maji ndani ya kinu. Sasa tunataka kujua, hii barabara itajengwa au haijengwi? Kama haijengwi pia utupe jibu, kwa sababu tumechoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara ina historia ndefu. Nafikiri wakati wa miaka ya nyuma, wakati wa enzi za kupigania uhuru, wapo wapigania uhuru ambao waliitumia njia hii, lakini mpaka leo barabara nyingine za karibuni hapa zimejengwa. Hakuna barabara iliyokuwa ndefu kama kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza, imejengwa. Sasa inakuwaje kipande kidogo hiki cha Tanga – Pangani - Bagamoyo mpaka Dar es Salaam kishindwe kujengwa? Marais wanne wote wametoa ahadi mpaka leo barabara hii haijengwi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atakapokuja anieleze hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niseme, kama hakuna fedha, tuitafute ilipo ile *1.5 trillion* ili tuiingize katika barabara ya Pangani tuweze kujenga barabara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niizungumzie Bandari ya Tanga. Bandari ya Tanga ni bandari kongwe, ndiyo bandari ya kwanza kujengwa katika Afrika Mashariki na Kati, lakini bandari hii inapuuzwa. Tarehe 28 mwezi wa Pili nilialikwa katika Kikao cha Bodi ya Bandari wakawepo wafanyabiashara wa Mkoa wa Tanga na mikoa ya jirani pamoja na uongozi wa bandari, lakini ukisikiliza wafanyabiashara wanalalamika, viongozi wa bandari wanalalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari ile haina vifaa vya kisasa vya kushusha na kupakia mizigo. Kwa mfano, *crane* ya kubeba *forty feet container* haifanyi kazi, ni mbovu. Hata wakiomba fedha kwa ajili ya ukarabati pia haufanyiki. Sasa itakuwaje tuwe na bandari lakini haina vifaa vya kushushia mizigo, wakati tunaagiza mizigo kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo pia nitataka nijibiwe, linawezekana au haliwezekani? Ikibidi basi itafutwe fedha au Bandari ya Tanga nayo iingizwe katika bandari ambazo zinapelekewa vifaa vya kisasa na vya kutosheleza kupakia na kupakua mizigo. Kwa sababu Bandari ya Tanga inasemwa, inafanya kazi kwa hasara. Haifanyi kazi kwa hasara, haina vifaa. Hata muwe wengi vipi, hamwezi kubeba kontena la *forty feet* kwa mikono. Kwa nini bandari isifanye kazi kwa hasara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini huu ni mpango wa kuiua makusudi Bandari ya Tanga kwa sababu haiingii akilini kwamba leo bidhaa zetu zote tuziingize katika Bandari ya Dar es Salaam hali ya kuwa Bandari ya Dar es Salaam yenyewe imefanyiwa ziara za kushtukiza. Mheshimiwa Waziri mwenyewe amefanya, Mheshimiwa Waziri Mkuu amefanya na Mheshimiwa Rais amefanya, lakini pana matatizo hayamaliziki. Kwa nini hawabadilishi bandari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie, hata alipokuja Mheshimiwa Rais Tanga katika bomba la mafuta nilipata nafasi ya kuzungumza nikasema lazima tufanye *categories* za mizigo. Haiingii akilini, Bandari ya Mtwara imelala, Bandari ya Tanga imelala, ifanye kazi Bandari ya Dar es Salaam peke yake. Nikaishauri Serikali kwamba baadhi ya mizigo iwe inateremka katika kila bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Mikoa ya Ruvuma, Mtwara kwenyewe, Katavi, Rukwa na Sumbawanga huko pamoja na nchi za Zambia na Malawi mizigo yao ingeshuka Bandari ya Mtwara kwa sababu pana *Mtwara Corridor*. Bandari ya Tanga ishughulikie mizigo ya Tanga yenyewe, Moshi, Arusha, Manyara, Simanjiro na Musoma pamoja na nchi za Uganda labda na Rwanda mizigo yake ingekuwa rahisi kwa gharama kuishushia Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali mnayoisema sikivu, sijui usikivu huo uko wapi? Kwa sababu tunakubali sasa bandari moja ya Mombasa mapato yake kwa mwaka inazishinda bandari nne za Tanzania. Bandari ya Zanzibar,

Dar es Salaam, Mtwara na Tanga, mapato yake ukiyajumuisha vyote kwa pamoja hayafikii Bandari ya Mombasa. Kwa nini? Wenzetu wameamua kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalozungumzia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mussa.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Devotha Minja dakika tano na Mheshimiwa Joseph Haule dakika tano.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia dakika tano hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia watu wanasifu Wizara inafanya vizuri, lakini kwa wananchi wa Manispaa ya Morogoro hawawezi kuwasifia hata mara moja. Ni kwa nini nasema haya? Kuna barabara ya Tubuyu – Kichangani katika Manispaa ya Morogoro. Barabara ile ina kilometa nne tu imejengwa, kilometa moja imejengwa kwa shilingi bilioni 3.4; kilometa nne zimejengwa kwa shilingi bilioni 13.6. Barabara imenyooka kama chuma cha pua; barabara unaweka rula unanyoosha, haina milima, mabonde wala mito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Madiwani wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) ambao waliungana nami pamoja na baadhi ya Madiwani wa CCM. Mwaka 2017 nilisema na kwa bahati nzuri baada ya kuona kwamba hela hizi zimepigwa; tuliamua kwenda kwa wataalam wa *TANROAD* tukawaambia hebu tuambieni, sisi sio wataalam, tunataka kujua barabara hii kwa nini imejengwa kwa gharama hizi nyingi kiasi hiki? Nao wakawa wanashangaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakatuambia kilometa moja *standard* yaani barabara *concrete* inajengwa kwa shilingi milioni 800 mpaka shilingi bilioni moja tena kwenye maeneo ambayo ni korofi. Tukawaambia hapa zimetumika shilingi bilioni 13.6. Wakatuambia hatujawahi kuona, pengine ni kwenye barabara za ahera ndiyo zinaweza kuwa na gharama kubwa kiasi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukaanza kupambana ndani ya Halmashauri yetu, tukajaribu kuuliza matumizi ya fedha hizi. Ikumbukwe fedha hizi ni mkopo wa *World Bank* ambao uliletwa kwenye nadhani Halmashauri kadhaa kama saba hivi na Halmashauri ya Morogoro ikiwemo, ambazo tunategemea kwamba Watanzania watakuja kuzilipa kwa jasho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuja na hoja hiyo Halmashauri, viongozi wa Halmashauri wakaanza kutembeza rushwa kwa Madiwani na Madiwani wakasema hawakubaliani na hali hii, wakaandika barua kwa Mkuu wa Mkoa kuthibitisha wamepewa rushwa ili wanyamaze kwenye jambo hili. Nakala wakapeleka kwa *DSO* na *RCO* wakasema sisi hatupo tayari, tupo tayari kuhakikisha kwamba tunataka kujua hatma ya fedha hizi. Ukimya mpaka leo, hakuna kilichoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukuishia hapo, tukaja Bungeni, nikazungumza, nikamwomba Mheshimiwa Jafo wakati huo akiwa Naibu Waziri. Akaenda Morogoro akaiona barabara ile, akaunda Tume. Hata Tume aliyoiunda mwaka 2017 mpaka sasa hivi hakuna kitu ambacho kimefanyika mpaka sasa.

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

## TAARIFA

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa anayesema, Usalama wanahangaika na Lijualikali na Mama Kiwanga wakati kuna wizi kama huu. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Devotha Minja.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea. Nimefurahi sana kupata hizo taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Jafo alikuja ameunda Tume akashangaa barabara kutumia fedha nyingi kiasi hiki, lakini mpaka sasa amekuwa Waziri ni kimya.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**T A A R I F A**

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ni Diwani wa Halmashauri hiyo, naomba athibitishe kama na mimi nilipata rushwa au wote walipata rushwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Devotha Minja.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Ngoja apokee taarifa moja moja, Mheshimiwa Devotha Minja.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema baadhi ya Madiwani na ambao walikwenda TAKUKURU kutoa ushahidi kabisa kwamba wamepewa ili wanyamaze. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**T A A R I F A**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan taarifa.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba ndani ya Mkoa wa Morogoro siyo Manispaa tu, hata Kilosa barabara ya lami imejengwa lakini sasa inatimka vumbi, hata miezi sita haijatimia. Kwa hiyo, huu ni mwendelezo wa Mkoa wa Morogoro kupiga hela za barabara. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mnachangia. Mheshimiwa Devotha Minja.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa. Watu wamefanya Mkoa wa Morogoro ni shamba la bibi, ni lazima tuseme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukawa tunavizia tukutane kwenye Kikao cha *RCC* tuweze ku-*raise* hoja zetu kuhusu barabara hizi, lakini tumepigwa ile inaitwa nini?

**MBUNGE FULANI:** Kata funua.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Chenga ya mwili. Mkoa wa Morogoro haukufanya kikao cha *TANROAD* wala hatukufanya kikao cha *RCC.* Tumekuja Bungeni tunakutana na vitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkuu wa Mkoa anakwepa kujibu hoja hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalipeleka wapi Taifa hili?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Devotha Minja. Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Haule baada ya hapo, Mheshimiwa Sixtus Mapunda ajiandae.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa sababu nina dakika tano, nami ni mwanamuziki bora kabisa wa *hip hop* nitakwenda kwa *style* ya *rap* kidogo, yaani mbio. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikazie alipoishia mwenzangu Mheshimiwa Devotha Minja. Ni masikitiko makubwa sana kwa Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Morogoro na wadau wote wa maendeleo Mkoa wa Morogoro kwa kitendo cha Mkoa wa Morogoro kushindwa kukaa katika Bodi ya Barabara na kushindwa kukaa katika Kamati ya Mashauriano ya Mkoa, ni aibu kubwa sana kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikwambie, tumekuja hapa Dodoma ndiyo tunaletewa makabrasha makubwa yaani kama hivi ili tuanze kuyasoma wakati hatujapitisha na hatujui bajeti ya Mkoa wa Morogoro imepitishwa na nani? Mnaweza mkapata picha, Waheshimiwa Wabunge mnajua umuhimu wa *Road Board* na mnajua umuhimu wa *RCC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisogeza hilo kwa Mheshimiwa Waziri ili aweze kuangalia jinsi atakavyotusaidia kama inawezekana kweli wanasema wanaweza kutumbuana, wajaribu kuangalia hili jambo watali-*handle* vipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema nitakwenda haraka kidogo. Jambo la kwanza ninalotaka nianze nalo, kilio cha wana Kilosa na Mikumi ni barabara ya kutoka Dumila kwenda Kilosa kuishia Mikumi. Hii barabara ni muhimu sana na mpaka sasa imejengwa kwa kilometa 45 tu. Nimeona kwenye kabrasha la Wizara hapa, wanasema wametenga shilingi bilioni sita na zenyewe ni kwa sababu ya kulipa madeni ya mwanzo huko ya watu wengine. Hatujui kimetengwa kiasi

gani cha kukamilisha kilometa 24 za kutoka pale Ludewa mpaka Kilosa, lakini pia kilomita 78 za kutoka Kilosa mpaka Mikumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni barabara ni ya msingi, inakwenda kuunganisha watu wa kaskazini wanaopita Korogwe wanaokuja kutokea Turiani wanakuja Dumila, wanatokea Kilosa – Mikumi wanakwenda kwa Mheshimiwa Lijualikali kule Kilombero, wanakuja kutokea Mlimba lakini wanaenda kuingia Njombe pamoja na Songea. Unaweza ukaona jinsi ambavyo barabara hii ni ya muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tumeomba pia kupandishwa hadhi kwa barabara yetu inayotoka pale Ruaha Mbuyuni, inaenda Malolo – Uleling'ombe inakuja kutokea Kibakwe kwa kaka yangu Simbachawene, lakini mpaka leo hatujapata majibu hii barabara itakuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu Daraja la Ruhembe. Nilishaongea mara nyingi hapa, hili daraja ni la muhimu, ndugu zetu wanakufa mara kadhaa. Mheshimiwa Waziri alisimama na kuniambia kwamba wametenga shilingi milioni 700, sizioni sehemu yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walituambia watatupa daraja la muda pale kutoka Kiberege, limeshakuja, machuma yamewekwa chini, ndugu zangu wa kule Ruhembe bado wanaendelea kufa, watu na mama zetu wanataabika sana. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, akija atuambie mpango gani wanao kuhusu Daraja ya Ruhembe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu uchukuzi. Jimbo la Mikumi mnajua ni la utalii lakini sasa hivi ukimaliza tu pale kwenye vibao vya kuingia Mikumi, upande wa kulia wote *Railway* wamepiga X, maana yake nyumba zote na vitega uchumi vyote na mahekalu yote yaliyojengwa kule inabidi yabomolewe. Wananchi wa Mikumi wanaishi kwenye taharuki kubwa sana. Hii siyo Mikumi peke yake, bali

Kata ya Kidodi na Kata ya Ruaha ambayo ni Kata mama katika Jimbo la Mikumi, nao wanaishi katika sintofahamu hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilijaribu kuwasiliana na viongozi wa *Railway* wakatuambia kwamba wanajua kwamba pale Mikumi kulikuwa na reli inatoka Kilosa kuja pale kwenye kiwanda cha sukari, lakini hiyo reli yenyewe mpaka leo mataruma yameshang'olewa. Hakuna dalili ya reli yoyote, wanawafanya wananchi wa Mikumi wanaishi kwa wasiwasi, wanashindwa kuendeleza biashara zao, watalii wanashindwa kuwekeza kwa sababu ya kuwa na alama za X na tunaambiwa tutabomolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mheshimiwa Waziri wawaambie watu wa *TRL* waje kukaa na watu wa Mikumi kwa sababu watu wamepewa hati na wamejenga pale wamewekeza kwa ajili ya utalii, lakini wanakuwa katika hali ya sintofahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu suala la *TARURA.* Tunajua umuhimu wa *TARURA.* Mama yangu Mheshimiwa Kiwanga hapa amegusia kuhusu barabara ya pale Kilosa Mjini, shilingi milioni 600 imepigwa, lami imewekwa pale miezi sita haijafika inatimka vumbi, lakini bado hakuna kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA* Kilosa bado wana hali ngumu sana, fedha zinazokwenda ni ndogo lakini pia hawana usafiri. Wilaya ya Kilosa ni Wilaya kubwa sana, lakini pia jiografia yake ni mbaya sana. Tujaribu kuangalia jinsi ya kuwawezesha hawa *TARURA* ili waweze kufanya kazi nyingine za kutosha kusaidia wananchi wa Mikumi, maana kuna barabara zime... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Haule.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sixtus Mapunda na baadaye Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro na Mheshimiwa Mendrad Kigola wajiandae.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa na mimi nafasi ya kuchangia jioni hii ya leo. Naomba tu nikwambie kwamba nimeongea na Mheshimiwa Mlinga ameniambia nitakapoishia, dakika zake tano nitaendelea kuongea mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takriban miongo miwili na nusu, yaani miaka 25 Shirika letu la Ndege la Taifa lilikuwa linafanya vibaya sana. Watu wote tulikuwa tunalitazama kwa aibu na kuna baadhi yetu walilalamika na kusema tunazidiwa na kanchi kidogo kama Rwanda, tunazidiwa mpaka na Msumbiji ambao wana ndege yao kwa wiki inakuja Tanzania mara moja. Hayo yote yalitukwaza wengi sana ambao tulikuwa na nia ya kuiona Tanzania ikisonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee sana, nampongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kuamua kwa makusudi kututoa kwenye msukosuko wa miaka 25 ambapo shirika letu la ndege la Taifa lilikuwa linayumba... *(Makofi)*

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**T A A R I F A**

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpe taarifa mzungumzaji asitumie jina la Mheshimiwa Rais kushawishi, maana yake anatoa

pongezi kwa Mheshimiwa Rais, anataka kutumia jina la Rais kushawishi Waheshimiwa Wabunge. Tunaomba sana asiendelee kutumia jina hilo... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ameshafahamu, Mheshimiwa Six tafadhali.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anavunja kanuni za Bunge. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikuombe unitunzie muda wangu, halafu pili sitaijibu hiyo, inanipotezea muda wa kushusha yale ninayopaswa kuyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie, mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Ni ninyi ambao mlikuwa mnasema shirika hili halifai; ni ninyi mliokuwa mnasema kwamba hatuna ndege hata moja. Juzi tumenunua ndege, nyie mnakuwa tena wa kwanza kuturudisha nyuma kwa nini tumenunua ndege?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe ... *(Makofi)*

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Inaelekea kuna watu humu ndani wana matatizo ya akili.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa tafadhali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Heche naomba ukae.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa kwa sasa basi kwa sababu zinapoteza muda, tunakosa kuchangia mambo ya maana. Mheshimiwa Sixtus naomba uendelee.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sio mnyonge. *(Kicheko)*

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na nikuombe tu wala wasipate shida, waambie tu watulie niongee nikimaliza watatoa taarifa zao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Heche naomba ukae. Hicho ni Kiswahili, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Haki yake mpeni! Ni Kiswahili safi. Hivi nani asiyejua kwamba Rais wetu amekuwa na ujasiri mkubwa wa kulifufua shirika la ndege?

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Taarifa.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Nani asiyejua humu ndani? Kinachowakwaza nini kulisema jina la Rais kwenye mambo yaliyo mema? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu ni kawaida yao, wana macho lakini hawaoni; wana masikio lakini hawasikii; na wana roho zenye chuki zisizoweza kutenda jema lolote. Sasa tukisifia mambo mazuri wanataka tuseme nini? Ni wao walikuwa wanasema hayo*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme neno moja, mchana...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mchana Mheshimiwa Halima Mdee...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa mnapoteza muda taarifa hizi hazina msingi.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sixtus naomba uendelee.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mchana Mheshimiwa Halima Mdee alilidanganya Bunge. Nataka nimpe taarifa mchana ule, lakini kwa sababu nilijua nitapata muda sasa hivi, nikasema niutumie muda huu kwanza kumpa hiyo taarifa na kuwapa taarifa watu wengine wote ambao wanaona lakini wanajifanya hawaoni; wanasikia na wanajifanya kuwa hawasikii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Halima Mdee mchana alisema *ATCL* haina *strategic plan* na haina *business plan.* Mwaka 2017 tukiwa kwenye Kamati ya *PIC* tuliliita Shirika la *ATCL.* Mimi nilikuwa Mjumbe na cha kushangaza wengine waliokuwa wanapiga makofi kwenye uongo huo nao walikuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba moja, Mheshimiwa Frank Mwakajoka tulikuwa naye; namba mbili, Mheshimiwa Esther Bulaya, tulikuwa naye; namba tatu, Mheshimiwa Maftaha, tulikuwa naye; namba nne, Mheshimiwa Kwandikwa tulikuwa naye; na namba tano, Mheshimiwa Edwin Sannda tulikuwa naye. Kwenye taarifa yao, sio yangu. Walisema mwezi Juni, 2016 Serikali iliamua kulifufua upya shirika la ndege. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Katika kulifufua Shirika la Ndege... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sixtus...

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kulifufua Shirika la Ndege lilikuwa na mambo mawili ilibidi yote yafanyike kwa wakati mmoja. Jambo la kwanza kurudisha hadhi ya *ATCL* kipindi inaelekea kufa; na suala la pili kuifanya iendelee kwenda kwa muda mrefu ili tusirudi kwenye upungufu uliofanya shirika life. Katika kipindi cha mwaka mmoja kilikuwa mwezi Juni, 2016 na Julai, 2017 *ATCL* walikuwa wana mpango wa muda mfupi ulioitwa *Turn Around Strategy. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2017/2018 wakaja na mpango wa miaka mitano ambao ni *Corporate Strategic Plan* iliyokuwa na malengo yafuatayo:-

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mnafanya vurugu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Hapana, Waheshimiwa Wabunge mnafanya vurugu hatusikilizani!

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mnafanya vurugu siwezi kusikia nani anasema nini? Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Sixtus uendelee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

*(Hapa baadhi Wabunge Waliongea bila mpangilio na kuzomea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa naomba utulivu, tunaomba amalizie.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unitunzie muda wangu.

**MWENYEKITI:** Endelea Mheshimiwa.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Jamani kinachowawasha nini? Pilipili msiyoila yawawashia nini? Acheni niongee.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mkakati wa miaka mitano...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hatusikilizani, kwa sababu sijui nani anataka taarifa. Sasa mnamsemea Mheshimiwa Halima Mdee?

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mnamsemea? Haya Mheshimiwa Halima Mdee nakupa. Mkiendelea kufanya vurugu na yeye namwambia akae. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Halima Mdee nakupa. Mkiendelea kufanya vurugu naye namwambia akae. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo ambao tunaita unafiki. Kwa watu ambao wako Kamati ya *PIC* ambayo Mheshimiwa Sixtus alikuwepo, wanajua majadiliano yao walizungumza nini na msimamo wake ulikuwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia sijatoa maneno yangu mdomoni, nimetoa Taarifa ya Ofisi ya Msajili wa Hazina ya tarehe 29, Machi, 2017; nimetoa rejea ya Shirika la Ndege lenyewe ya Machi, 2017; nimetoa rejea ya Taarifa ya *PIC* ambayo Mheshimiwa Sixtus alikuwepo kabla hajatimuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu hapa ni kwamba...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima, unachangia ama unampa taarifa?

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nampa taarifa, afute kauli yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa, kama anataka kujipendekeza kwa Serikali asitaje jina langu. Nimetoa rejea ya Serikali. Tumetoa pesa... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Umeeleweka Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetoa shilingi mbilioni 500 mwaka 2017/2018 wakati hakuna mpango wa biashara. Wanasema...

**MWENYEKITI:** Umeshaeleweka. Mheshimiwa Sixtus, naomba umalizie.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Acha kujipendekeza, zungumza mambo...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niombe, zimechezewa...

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, zimechezewa dakika zangu sita, naomba unilindie.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa sitaki taarifa, kwa sababu hakuna taarifa ambayo mnatoa yenye msingi wa kuweza kuelewana, tunakwenda kubomoana.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sixtus, naomba umalizie muda wako.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza anazidi kuongopa, anasema amepata Taarifa ya Msajili wa Hazina ya Mwaka 2007 na wakati mimi naongea *strategic plan*...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Acheni mambo ya kisenge ninyi. Mnafikiri sisi mambo ya hivyo hatuwezi?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, upande huu huku mmechangia mpaka mmemaliza hamjafanyiwa vurugu, naomba mtulie. Mheshimiwa Sixtus, naomba umalizie.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

## TAARIFA

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Napenda kumpa taarifa ndugu yangu anayezungumza na wanaochangia; mara nyingi nimekuwa nikizungumza humu Bungeni. Bunge hili linaendeshwa kwa

Kanuni, nawaangalia wanaopiga kelele humu wote ni wasomi, wengine wanasheria na vyeti vyao ni vikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapa taarifa kwamba haya maneno ambayo huwa nayaongea kila siku, naomba Kiti chako kiyafanyie kazi tukaguliwe vyeti vya shule humu ndani. Sina uhakika kama haya mambo yanafanywa na wasomi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sixtus, naomba umalizie dakika zako mbili.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango mkakati wa mwaka 2017 - 2022, shirika liliamua kwa makusudi kufanya mambo matatu. Jambo la kwanza, kuhakikisha wananunua ndege mpya ambayo wamefanya; jambo la pili, ilikuwa ni kuendeleza marubani ili itakapofika ndege zote tusipate anguko ambalo lilipatikana miaka 25 iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa Shirika la Ndege, kutokana na mikataba mipya ya kununua ndege mpya, inasomesha marubani 62. *On top of that,* inasomesha marubani 12 kutokana na makubaliano ya Shirika la Ndege la Taifa la Tanzania pamoja na Shirika la Ndege la Ethiopia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, naomba niseme kuhusu faida zinazoweza zikapatikana na *ATCL.* Wengi wamesema wakiangalia hasara ya uendeshaji wa Shirika la Ndege kwa kuangalia ununuzi wa tiketi na huduma ambazo ndege inatoa ndani ya ndege kipindi abiria wanasafiri. Shirika la Ndege ukiondoa hizi faida zinazoonekana moja kwa moja ina faida tatu kubwa ambazo dunia nzima...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, faida ya kwanza ni *ancillary services.* Kuna muda ukimsafirisha

abiria nchi inapata faida kwa huduma ambazo katika nchi husika zinatolewa. Naomba nitoe mifano ya mashirika ya ndege ambayo hayakuwahi kupata faida ya moja kwa moja ya tiketi, lakini yalipata faida kutokana na *ancillary revenue...*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ya kwanza ni Shirika la Ndege la *EasyJet* la Uingereza...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2006 walipata faida ya jumla ya *Euro* milioni 189; Shirika la pili ni *Aer Lingus* ya Ireland... *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** ...ilipata faida ya Euro milioni 63; Shirika la Tatu ni *AirAsia* ya Malaysia, lilipata faida ya *Euro* 22... *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne ni *United Airlines* la *United States of America,* mwaka 2009 lilipata faida ya bilioni 1.5 nje ya kuuza tiketi.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa. Mzungumzaji anasema uongo.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema, watu wasiojua hii *industry,* wakasome waijue, wasibishe vitu wasivyovijua.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sixtus muda wako umekwisha.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Damas Ndumbaro, baadaye Mheshimiwa Mendrad Kigola ajiandae.

**MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona na kunipa nafasi hii ili nami nichangie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kutoa pongezi za dhati kabisa kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kutekeleza ipasavyo Ilani ya Chama cha Mapinduzi, hasa katika sekta hii ambayo tunaiongea hivi leo. Ni wazi kwamba Ilani ya Chama cha Mapinduzi na Ilani ya CHADEMA zote zinaongelea kufufua Shirika la Ndege la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza hilo, Serikali ya Chama cha Mapinduzi kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imenunua ndege sita. Siyo hilo tu, katika bajeti ambayo Mheshimiwa Waziri ameisoma hapa, kuna viwanja 16 vya ndege ambavyo vitatengenezwa. Viwanja hivi vitasaidia hizi huduma za ndege. *(Makofi)*

Mheshimwa Mwenyekiti, sisi wengine Majimbo yetu yako mbali sana, umbali wa kutoka hapa Dodoma kwenda Songea ni mkubwa, hizi ndege zitatusaidia sana kufanya mawasiliano. Kama kuna mtu anaona ndege hizi hazimsaidii, basi tuweke bayana kwamba viwanja vya ndege katika Jimbo lake visitengenezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sisi watu wa mikoa ya kusini tuna kila sababu ya kuipongeza Wizara; Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri, kwa kukamilisha Barabara muhimu sana inayojulikana kwa jina la *Mtwara Corridor.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa ukitoka Mtwara unapita Masasi, Tunduru, Namtumbo, Songea, mpaka Mbinga, barabara hiyo imekamilika kwa kiwango cha lami. Kipande kilichosalia cha Mbinga – Mbamba Bay tayari mkandarasi ameshasaini na tunaamini barabara hiyo itakamilika haraka ili kufungua fursa zilizopo katika Kanda ya Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hiyo barabara ya *Mtwara Corridor* kuna kipande kidogo kimoja kimebaki cha kilometa 11, nayo ni *bypass* ya Songea Mjini kutoka Kata ya *Seed Farm* kupitia Kata ya Msamala na hatimaye Kata ya Luwiko. Ili kuhakikisha kwamba *Mtwara Corridor* inakamilika kwa ukamilifu kabisa, lazima kipande hicho kikamilike. Mheshimiwa Waziri, nimesoma hotuba yako kwa makini sana, sijaona hizo kilometa 11. Hivyo, ni rai yangu kwamba kilometa hizo 11 ziweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa usafiri katika Ukanda wa Kusini kuna mpango wa kujenga reli kutoka Bandari ya Mtwara mpaka Mbamba Bay ili kuweza kuhudumia Liganga na Mchuchuma, Miji ya Songea, Miji ya Masasi na miji mingine. Fedha iliyotengwa katika kitabu hiki kwa mradi huu bado ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wote wa Ukanda wa Kusini wakiongozwa na wananchi wa Jimbo la Songea Mjini wana hamu ya kuiona reli hii ikijengwa, ikifanya kazi, ikitoa huduma na ikiunganisha Tanzania na nchi mbili; ya Msumbiji pamoja na ya Malawi. Kwa hiyo, tunatarajia hili nalo Mheshimiwa Waziri atalichukua alifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Songea, wananchi ambao wameachia maeneo yao wanadai fidia katika upanuzi huo. Naomba kumkumbusha Waziri, Mheshimiwa Profesa Mbarawa na Naibu Mawaziri, kwamba naomba hilo nalo litiliwe maanani ili tuondoe kero hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, niipongeze tena Serikali ya Chama cha Mapinduzi, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Dkt. Ndumbaro. Tunaendelea na Mheshimiwa Kigola na baadaye Mheshimiwa Bupe Nelson ajiandae.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na pongezi, Serikali inafanya vizuri sana. Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Mawaziri wanafanya kazi vizuri sana. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe ushauri kidogo. Kila mwaka tunasoma hiki kitabu, bahati nzuri kitabu kinaandikwa vizuri sana, lakini kuna barabara ambazo zinafanyiwa upembuzi yakinifu kila mwaka na kuna barabara nyingine zimeshafanyiwa upembuzi yakinifu, imeshapita hata miaka mitatu, minne lakini ujenzi bado haujaanza. Nataka niishauri Serikali, kwa barabara zile ambazo zimeshafanyiwa upembuzi yakinifu, naomba zianze kujengwa sasa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, barabara ile ya Mafinga mpaka Mgololo, barabara ya Nyololo mpaka pale Mtwango, upembuzi yakinifu ulishafanyika toka mwaka 2013, ulishakamilika. Kwa hiyo, ujenzi bado. Mheshimiwa Waziri, naomba hiyo barabara kwa sababu Serikali iliahidi kwamba itajenga kiwango cha lami na ukizingatia kule kuna viwanda vingi sana, naomba ianzwe kujengwa kwa kiwango cha lami kama ilivyokuwa imeahidiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara moja kubwa ambayo inatoka Mafinga kwenda Igawa, naishukuru sana Serikali imeanza kuitengeneza barabara hiyo vizuri sana.

Naiomba Serikali, ile barabara kuna sehemu naweza nikasema inapita kwenye vijiji vikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, pale Nyololo pana wafanyabiashara wengi sana, wanafanya biashara kuanzia asubuhi mpaka usiku. Sasa naomba wakitengeneza pale, ile barabara iwe pana halafu itengenezwe kama stendi, halafu ziwekwe na taa za barabarani kwa sababu pale pana wafanyabiashara wengi sana, itawasaidia sana wafanyabiashara wa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu naiomba tena Serikali kwa barabara hiyo hiyo, nadhani hata Mheshimiwa Rais atakuja kuifungua ile barabara. Pia pale Mbalamaziwa ni sawa na Nyololo, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri pale Mbalamaziwa basi patengenezwe stendi kubwa ambayo iko ndani ya barabara ili magari makubwa yanapopaki pale ajali zipungue, kwani kuna ajali huwa zinatokea mara nyingi sana. Kwa hiyo, naomba stendi ziimarishwe, zitengenezwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sehemu nyingine kuna vijiji vinaingia kwenye barabara, sasa kuna stendi ndogo; naomba na zile stendi ndogo basi zioneshwe vizuri ili tuhakikishe kwamba kwenye stendi ndogo ili kupunguza ajali, basi tupanue zile barabara ziwe pana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo la Mufindi Kusini kuna barabara ambazo ni za *TANROADS.* Zile barabara kwa kweli Serikali inatengeneza vizuri sana na ukizingatia kule Mufindi tuna mvua nyingi na tunaenda kwa kalenda; kuanzia mwezi wa Sita huu mpaka mwezi wa 12 barabara ndiyo zinatengenezwa. Sasa naomba ile bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 ambayo inaishia, naomba basi zile barabara za *TANROADS* zianze kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, barabara ya kutoka Nyololo mpaka pale Mtwango ambayo Serikali iliahidi kwamba itajenga kwa kiwango cha lami, lakini itaendelea kuboresha kwa kujenga kiwango cha changarawe mpaka

pesa itakapopatikana, basi mwaka huu mwezi wa Sita tuanze kuitengeneza ikae vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ya kutoka pale Mgololo inaenda mpaka Nyigo inapitia Nyihawaga na yenyewe ni barabara ya *TANROADS,* naomba basi Serikali na yenyewe ianze kuijenga. Kuna barabara ya kutoka Mbalamaziwa mpaka kule Kwatanga ni barabara ya *TANROADS,* naomba ianze kutengenezwa. Kuna barabara ambayo nairudia tena ya kutoka Mafinga hapa mpaka pale Sawala, imeharibika sana, naomba ianze kutengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utengenezaji wa barabara, naomba twende kiutaalam, ile mifereji *(outlets)* ya kutoa maji itengenezwe kiwango kizuri, kama kuna uwezekano tuweke hata kiwango cha kokoto ili maji yaweze kupita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na barabara zile za Wakala wa Barabara Vijijini *(TARURA).* Kuna barabara kwa mfano kule Idete bado hazijatengenezwa kwa viwangovizuri. Kuna barabara ya kutoka Luhunga mpaka kule Iyegeya, haijatengenezwa vizuri. Kuna barabara ambayo inatoka Maguvani mpaka pale Mtambula mpaka Kasanga, wananchi wanalalamika sana ile barabara. Naomba sana waweze kuitengeneza ile barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni mawasiliano. Serikali iliahidi kwamba itajenga mnara katika Kata ya Idete, Kata ya Maduma, Kata ya Kasanga, pale Udumuka hakuna mawasiliano kabisa na pale Kiyowela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua mawasiliano ni ya muhimu sana. Sasa katika kata hizi nilizotaja, mawasiliano hakuna kabisa. Naomba Serikali kama ilivyokuwa inaahidi iweze kujenga minara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, naipongeza sana Serikali. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kigola. Mheshimiwa Bupe.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika Wizara hii ya Ujenzi. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima, nasi kuweza kuchangia katika Wizara hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anazozifanya. Mwenye macho haambiwi tazama; na mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni. Mheshimiwa Dkt. Magufuli Mungu yupo pamoja nawe, pamoja na Serikali yako, pigeni kazi. Watanzania wote wako nyuma yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeze pia Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Profesa Mbarawa pamoja na Naibu Mawaziri wake wote wawili kwa kazi kubwa wanazozifanya. Hakika Wizara hii wanaitendea haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze sasa kwenye suala la Uwanja wa Ndege wa Sumbawanga. Kwanza kabisa naishukuru sana Serikali kwa kutenga fedha. Nimeona katika ukurasa wa 154 zimetengwa fedha karibu shilingi bilioni 12 kwa ajili ya Uwanja wa Sumbawanga wa Mkoa wa Rukwa. Pamoja na shukrani hizi, bado nina hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanaouzunguka uwanja, wananchi wa Mkoa wa Rukwa walifanyiwa tathmini ya muda mrefu. Tumepiga kelele sana; Mheshimiwa Aeshi, Mbunge wa Jimbo la Sumbawanga Mjini amepiga kelele sana hapa, lakini bado wananchi wale hawajalipwa. Bajeti ya mwaka 2017 pesa zilitengwa, lakini wananchi hawakulipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo yote Serikali inayofanya, naomba sana katika fedha hizi

zilizotengwa kipaumbele kiwe kuwalipa kwanza wale wananchi. Wanatia huruma sana wale wananchi. Wengine wamekufa wameacha watoto yatima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba zile hawawezi tena kuchukulia mikopo, zimebaki tu zimewekwa X. Katika hii fedha iliyotengwa, pamoja na kwamba Serikali inakwenda kujenga uwanja, lakini ichukue kipaumbele kwanza cha kuwalipa wale wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali yangu na Mheshimiwa Waziri kwa kununua ndege. Ni kazi kubwa sana waliyofanya Serikali, lakini pamoja na ununuzi wa ndege naipongeza sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi. Tunaomba Mkoa wa Rukwa hizi *Bombardier* nasi tupate angalau *route* kwa wiki hata mara moja, *Bombardier* ishuke pale Rukwa, wananchi wafurahie matunda ya Rais wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze sasa kwenye suala la barabara. Naipongeza sana Wizara, inafanya mambo mengi makubwa, lakini bado barabara ya kutoka Sumbawanga Mjini kwenda Kala. Ile barabara imekatika kabisa, yaani wananchi sasa hivi magari yakifika pale kwenye daraja wanapeana zamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado barabara ya kutoka Katongolo kwenda Namansi, imekatika; barabara ya kutoka Marongwa kwenda Kasura *Junction* imekatika; na barabara ya kutoka Nkana – Kala imekatika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Rukwa Jimbo la Nkasi Kusini kwa Mheshimiwa Mipata hali ni mbaya sana. Mheshimiwa Mipata amekuwa akihangaika sana kutafuta hata pesa za dharura, lakini imeshindikana. Tunaomba watuangalie, watoe hata pesa za dharura ili kutengeneza hizi barabara.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zimekatika kabisa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bupe, subiri kidogo, taarifa.

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uchangiaji mzuri unavyoendelea, kwa kweli imenigusa sana, nimeshtuka alivyotaja barabara hii ya Nkana – Kala. Naifahamu, nilikuwa Mkuu wa Mkoa kule, yaani nazidi kusema kwamba ni vyema akasaidiwa. Ndiyo taarifa niliyotaka kumpatia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bupe.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea kwa mikono miwili, tena namshukuru sana kwa kunisaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi barabara yaani tuna hali mbaya sana. Ninavyosema hivi, Mheshimiwa Mipata ameomba pesa ya dharura mpaka sasa hivi bado hajapata majibu. Wananchi kule wanampigia simu, wanapiga simu kwa Wabunge wote lakini hakuna majibu. Tunaomba sana angalau *TARURA* au Wizara itoe pesa za dharura ili barabara hizi na haya madaraja yajengwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze sasa kwenye mtandao. Wilaya ya Nkasi tunashukuru Serikali ilituletea mtandao katika Kata ya Wampembe, lakini bado Kata za Kala, Sintari, Ninde, wananchi wanapanda kwenye mti, hasa wanawake usipovaa bukta sasa unapandaje kwenye mti ili ukaongee na simu? Wanakwenda kwenye milima, vichuguu kwenda kuongea na simu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wizara hii iliangalie hili suala watuletee mtandao kwenye hizi Kata. Wanawake tunashindwa sasa kupanda kwenye ile miti

maana miti mingine ni mirefu, mtandao unapatikana juu kabisa. Kwa hiyo, suala hili lichukuliwe kwa umuhimu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee barabara za hapa Dodoma. Sisi tunaokaa *Area D,* barabara zinazotoka kwenye yale maghorofa wanayokaa Wabunge zimeharibika sana kiasi kwamba wakati mwingine tunaweza tukapata ajali hapa hapa mjini. Tunapita hii njia ya kwenda Morogoro tunakatisha kwenye vichochoro mpaka tukafike kule *Area D* Sengia unakuwa umepata shida sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba wangetufungulia japo kwa muda tuwe tunakatisha pale kwenye uwanja ule wa ndege ambao wamefunga, sisi Wabunge tuwe tunapita kwa muda kwa sababu tunavyopita kwenye vichochoro tunaweza tukakabwa. Vile vichochoro tunapita kwenye nyumba za watu, kwenye milango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bupe.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, zile nyumba za *TBA* zimechoka, *TBA* hawazifanyii ukarabati. Sisi tunaoishi kwenye zile nyumba tunapata shida. *TBA* waje watufanyie ukarabati zile nyumba, tunalipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bupe kwa mchango wako huo mzuri.

Waheshimiwa Wabunge, huyo ndio mchangiaji wetu wa mwisho, muda wetu umemalizika kwa siku hii ya leo.

Nawashukuru wote ambao mmechangia michango mizuri kwa maslahi ya Taifa letu, Mwenyezi Mungu awabariki sana kwa kazi yenu nzuri mliyoifanya.

Baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho, tarehe 25 Aprili, 2018, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano Tarehe 25 Aprili, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*